# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TATU

Kikao cha Hamsini na Nne – Tarehe 30 Juni, 2016

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## DUA

*Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae, Katibu!

*(Hapa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni waliondoka Ukumbini)*

**NDG. RAMADHANI ISSA – KATIBU MEZANI:** Hati za kuwasilisha Mezani.

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofiis ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)!

Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu. Mheshimiwa Naibu Waziri!

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2015 (*The Annual Report and Audited Accounts of the National Environment Management Council (NEMC) for the Year Ended 30th June, 2015)*.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Mwaka ya Mfuko wa *PPF* kwa Mwaka Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2015 *(The Annual Report of PPF Pensions Fund for the Year Ended 30th June, 2015)*.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Taarifa ya Shughuli za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 *(Report of the Activities of the Open University of Tanzania for the Financial Year 2014/2015)*.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Kuhusu Shauri la Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Kuhusiana na Kutoa Ishara ya Matusi Bungeni.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Khatib Said, Mbunge wa Konde, kwa niaba yake namwita Mheshimiwa Venance Mwamoto.

Na. 461

### Viwango vya Mishahara kwa Makampuni Binafsi

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. KHATIB SAID HAJI)** aliuliza:-

Kumekuwa na mfululizo wa migomo, misuguano na migongano ya mara kwa mara kwa wafanyakazi wa viwandani na Kampuni binafsi zinazotokana na malalamiko ya mishahara na maslahi ya wafanyakazi:-

Je, ni mfumo upi na viwango gani vilivyowekwa kisheria wanavyotakiwa kulipwa wafanyakazi wa viwanda na Kampuni binafsi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo unaotumika katika kupanga viwango vya chini vya mshahara unasimamiwa na taratibu zilizoainishwa katika Sheria Na. 7 ya Taasisi za Kazi ya mwaka 2004 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, sheria imetoa madaraka kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya kazi, kuunda Bodi ya kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi. Bodi hii inaundwa na Wajumbe 17 ikiwa na Wawakilishi wa Wafanyakazi, Waajiri na Serikali. Majukumu ya Bodi hii ni kupanga kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha chini cha mshahara kilichopangwa na kinachoendelea kutumika hadi sasa katika Sekta ya Viwanda ni shilingi 100,000/= kwa mwezi na viwango vingine vya mshahara katika sekta 12 vimetajwa kwa GN.196 ya mwaka 2013.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venance Mwamoto, swali la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kwa kuwa kiwango hicho ni kidogo ambacho kinapelekea hata nauli; kwa mfano, hata katika mabasi ya mwendo kasi ukipiga hesabu hayamtoshelezi huyu mfanyakazi; hawaoni sasa wafanyakazi hawatafanya kazi kwa moyo na tija kwa sababu ya mshahara mdogo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kuna wenzetu wawekeza wa nje hasa Wachina wameingia, wanafanya kazi ambazo Watanzania wanazifanya, tena kwa bei nafuu; sasa Serikali haioni ni wakati wa kuwabana kuhakikisha kwamba zile shughuli zinazoweza kufanywa na Watanzania zifanywe na Watanzania badala ya wawekezaji wanaouza mpaka vocha ambao wameshaingia nchini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA, NA WENYE ULEMAVU – MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la kwanza Mheshimiwa Mbunge amehoji juu ya viwango hivyo kwamba ni vidogo na katika jibu langu la msingi nimeeleza vyema ya kwamba, Serikali kila baada ya miaka mitatu kupitia Waziri mwenye dhamana, amekuwa akitoa kitu kinaitwa *wage order*. *Wage order* ndiyo mshahara wa kima cha chini kwa sekta binafsi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge *wage order* ya mwaka wa mwisho ilikuwa ni ya mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa hivi tayari Mheshimiwa Waziri ameshaunda Bodi ya watu 17 ambao wanaanza kushughulikia suala hilo la mshahara wa kima cha chini. Bodi hii itafanya uchunguzi kutoka na sekta husika

na wataangalia maisha ya leo jinsi yalivyo na gharama zilivyo na baadaye sasa watapendekeza kwa Mheshimiwa Waziri kima kingine cha chini cha mshahara kutokana na sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu zoezi hili ndio linaendelea sasa na Mheshimiwa Waziri ameshakamilisha kazi yake, tunasubiri mapendekezo kutoka kwenye Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Waajiri pamoja na Serikali ili baadaye Mheshimiwa Waziri aweze kutoa amri kwa maana ya *order.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukuwe fursa hii kuwasisitiza wenzetu wa Vyama vya Wafanyakazi kuhakikisha kwamba wanasimamia majukumu yao ipasavyo ili waendelee kufanya vikao na waajiri ili katika yale ambayo bado wanaweza wakazungumza na waajiri katika kuboresha maslahi ya wafanyakazi, basi wafanye hivyo kwa niaba ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Mbunge aliuliza kwamba wako wafanyakazi wengi sana wa kigeni ambao wanaendelea kufanya kazi ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 Bunge hili lilipitisha Sheria ya Kuratibu Ajira kwa Wageni na ninyi wenyewe ni mashahidi, Serikali kupitia Wizara ya Kazi, tumekuwa tukisimamia sana sheria hii kuhakikisha kwamba zile kazi zote ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania na ambazo zina ujuzi ndani ya nchi hii ziweze kufanywa na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi kama Wizara, tutaendelea kuimarisha kaguzi mbalimbali ili kuwabaini watu wote ambao wanafanya kazi ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania ambapo kwa namna moja ama nyingine kumekuwa kuna tatizo kubwa sana la udanganyifu kwa maana ya kwamba, watu wakiomba vibali wanadanganya nafasi anayokuwa, lakini baadaye unakuta amechukua nafasi ambazo zinaweza zikafanywa na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi kama Serikali tutahakikisha kwamba tunaimarisha ukaguzi ili jambo hili lisiendelee kuwepo na tumekuwa tukichukuwa hatua stahiki pale inapobainika.

**NAIBU SPIKA:** Faida Bakar, swali la nyongeza!

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na matatizo ya mishahara kwa wafanyakazi wengi wa viwandani, lakini pia kuna tatizo moja sugu la ukatiwaji

wa bima, yaani wafanyakati wa viwandani kupatiwa bima. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuvilazimisha viwanda viwakatie bima za maisha wafanyakazi wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA, NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Serikali imegundua kwamba yapo matatizo ya namna mbalimbali ambayo wafanyakazi wanatakiwa wahifadhiwe kwa kufuata mifumo inayotakiwa katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua tatizo hilo, Serikali imeanzisha ule Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi na baada ya kuanzisha mfuko huo na kuwalazimisha waajiri watii takwa la kisheria la luchangia mfuko huo, sasa tunauhakika na ninaomba niwahakikishie wafanyakazi watulie kwa sababu sasa Serikali itakuwa ikiwafidia kupitia kwenye mfuko huo ambao umeanzishwa na Serikali na sisi tutaendelea kuusimamia kuhakikisha wafanyakazi wanafidiwa katika viwango vinavyostahiki kulingana na sheria ilivyo na namna mbalimbali ambazo zitakuwa zimetokea katika sekta zao za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali imelisimamia hilo na tutaendelea kulifanyia kazi vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Ulega, swali la nyongeza!

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Jimbo langu la Mkuranga liko tatizo la wafanyakazi wanaofanya kazi katika viwanda hivyo vya Wachina, kulipwa malipo madogo kwa muda mrefu wa kazi. *(Makofi)*

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kuja Mkuranga kuonana na vijana wale wanaofanya kazi katika viwanda vile na kuzungumza nao na hatimaye kuweza kuwapa matokeo ya kuweza kuwasaidia kama Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Wziri Mkuu, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA, NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ulega (Baba Tulia) kama ifuatavyo:- *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Ulega, ni kweli amewaleta hao wafanyakazi mpaka ofisini kwangu na anafuatalia sana suala hilo. Nami kama Waziri, naomba nimhakikishie kwamba tutampa ushirikiano. Tutaangalia Sheria inataka nini na hao wawekezaji ni kwa kiasi gani wanavunja sheria ambazo ziko katika nchi yetu, basi ninathubutu kusema kwamba nitaongozana na Mheshimiwa Ulega (Baba Tulia) kwenda katika maeneo hayo anayoyasema na tutapanga utaratibu. Ila tu tutamwomba mtoto Tulia asiingilie utaratibu wa ziara yangu na Mheshimiwa Ulega kwenda kuangalia matatizo hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sitaingilia Mheshimiwa Jenista! *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

Na. 462

**Wajasiriamali Wanaosumbuliwa na Mgambo – Dar es Salaam**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA (K.n.y. MARIAM N. KISANGI)** aliuliza:-

Wajasiriamali katika Mkoa wa Dar es Salaam hususan Machinga na Mama Lishe wamekuwa wakisumbuliwa sana na Mgambo wa Jiji hali inayowafanya kushindwa kujitafutia riziki ya kila siku:-

Je, Serikali inawasaidiaje Wajasiriamali hao wadogo wodogo ambao hujipatia riziki zao kupitia biashara ndogo ndogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inathamini sana mchango wa wafanyabiashara wadogo katika kukuza ajira na kipato. Hata hivyo, wafanyabiashara wadogo wote wanatakiwa kuendesha biashara zao katika maeneo yaliotengwa rasmi kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale wanaokiuka utaratibu huu, Halmashauri hulazimika kuwatumia Mgambo kwa ajili ya kuwaondoa wafanyabiashara hao na kuwaelekeza kwenda katika maeneo yaliotengwa

rasmi. Aidha, katika kutekeleza wajibu huo, mgambo wanatakiwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwatengea maeneo ya kufanyia biashara, Serikali inatekeleza mpango wa kurasimisha biashara katika mfumo usiokuwa rasmi ili kuzitambua, kuzisajili na kuongeza mchango wake katika ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kuzikumbusha Halmashauri zote kutenga maeneo kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo ili biashara hizo zifanyike katika maeneo rasmi ambayo itakuwa rahisi kuwatambua na kuwahudumia.

Aidha, wafanyabiashara wadogo wanashauriwa kuunganisha mitaji yao midogo na kuunda kampuni ndogo za biashara ili waweze kukopesheka katika Taasisi za fedha na hivyo kuongeza tija katika biashara hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya namna ambavyo Serikali imejipanga katika kuhakikisha wafanyabiashara ndogo ndogo, machinga, mama lishe na wengine wanaofanana na biashara hizo wanatengenezewa mazingira mazuri ya kibiashara; lakini tungependa hasa kufahamu kwa mfano, habari za uwezeshaji wa mitaji inawezekana ikawa ni njia rahisi sana ya kuwa-*contain* machinga hawa pamoja na maeneo wanayopewa ili waweze kufanya biashara zao kwa uhakika kwa sababu tayari wanakuwa na kipato kizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa sababu matatizo ya haya ya Dar es Salaam yanafanana sana na matatizo yaliopo Jiji la Mwanza, Wilayani Nyamagana, ambako pia kumekuwa na changamoto kubwa sana. Pamoja na maeneo mengi kupangwa, lakini Halmashauri zimefika sehemu zinakuwa zinabeba mzigo mzito kuona namna ya kuwawezesha hawa wafanyabiashara ndogo ndogo. Yako maeneo mengi yamepangwa, lakini uwezo wa wafanyabiashara hawa kwenda kule kutokana na miundombinu ambayo inakuwa siyo rafiki sana, maana Halmashauri inaweza ikatengeneza eneo vizuri, lakini miundombinu mingine ili iweze kufikika sawasawa inahitaji nguvu ya ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali na Wizara inatuhakikishia kwamba iko tayari kushirikiana na Halmashauri hizi kuwatengenezea wafanyabiashara ndogo ndogo, machinga na mama lishe ili waweze kupata kipato na maeneo yao yawe sahihi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI), majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla sijajibu swali hili, napenda kumpongeza kwanza Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Mheshimiwa Angelina Mabula. Siku sita zilizopita, nilikuwa Mkoani Mwanza, lakini jukumu langu kubwa kule lilikuwa ni suala zima la kuwa *cheque* ya karibu shilingi milioni 900 wajariamali wa Mwanza ambao wamejiunga pamoja kwa ajili ya kuhakikisha kwamba katika makampuni yao walioyaanzisha yalikuwa takribani 24 waweze kufanya kazi vizuri. Mheshimiwa Mabula naomba niwapongeze sana, mmefanya kazi kubwa sana! *(Makofi)*

MheshimiwaNaibu Spika, sasa katika suala la mitaji, naomba niseme kwamba mitaji hii malengo yetu katika Serikali ya Awamu ya Tano itatoka katika maeneo tofauti. Eneo kubwa kwanza la mtaji katika hivi vikundi vidogo vidogo, tulisema hata katika bajeti yetu ya TAMISEMI kwamba mwaka huu tumeelekeza asilimia tano ya vijana na asilimia tano ya akina mama ambao takriban kuna karibuni shilingi bilioni 56.4. Imani yangu ni nini? Imani yangu ni kwamba, kama Halmashauri zetu zitahakikisha zile *own source,* ile *ten percent* ambayo tano kwa akina mama na tano kwa vijana, tukizielekeza vizuri shilingi bilioni 56.4, zitaleta mafanikio makubwa sana katika Halmashuri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ni eneo moja la mtaji. Sambamba na hilo katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kuna suala zima la uwezeshaji. Eneo hili nalo litaweza kufanya kazi kubwa kuwawezesha vijana waweze kuwa na *skills* za kutosha katika suala zima la uwekezaji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, Serikali imejipanga na juzi tulikuwa na Benki moja inaitwa *Covenant Bank,* ambayo iko tayari kushirikiana na wadau mbalimbali. Lengo kubwa ni kukuza mitaji kwa watu wa eneo la chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikiri kwamba, sasa tunahakikisha kwamba hii mitaji sasa, wananchi wapate fursa, lakini sambamba na kupata elimu ilimradi waweze kupata mitaji kuweka uchumi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo la pili, kwa suala zima la kuboresha miundombinu. Ni kweli, maeneo mengine miundombinu inakuwa ni changamoto kubwa.

Kwa hili, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote, lakini nawapongeza wale ambao tayari wameshajenga masoko kuhakikisha kwamba wanawa-*accommodate* wafanyabiashara mbalimbali. Sambamba na hilo, tubainishe; inawezekana kweli maeneo mengine masoko yapo, lakini hayapitiki vizuri, barabara siyo rafiki na hata maeneo ya mama ntilie hayajakuwa sawa sawa. Basi naomba tuibue mambo haya katika Halmashauri zetu, tushirikiane kwa pamoja, bajeti zetu zinazokuja tuweke kipaumbele jinsi gani tutafanya hawa akina mama ntilie, wauza mitumba na watu wa kada mbalimbali waweze kupata fursa kwa ajili ya uchumi wa nchi yao na maendeleo yao binafsi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Keissy!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Hii Awamu ya Tano, kila siku namsikia Mheshimiwa Rais anazungumza haya mambo, kwamba ukinunua kitu dukani omba risiti; ukienda hotelini, omba risiti, je, Serikali imejipangaje kuhusu hawa wauza mitumba na wanaotembeza mali (machinga) na mama ntilie kwa ajili ya kutoa risiti ili tupate kodi ya Serikali yetu? Serikali imejipangaje hapo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI), majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Keissy, kwa nyakati tofauti amekuwa akihimiza sana suala la ulipaji kodi. Naomba tukiri kwamba hii nchi haitaweza kwenda bila watu kulipa kodi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, 2015 ametudokeza sehemu moja, mfanyabiashara mmoja anaingiza karibu shilingi milioni saba kila dakika. Kwa hiyo, kuna watu wakubwa wanakwepa kodi na wadogo wakati mwingine kodi hazikusanywi vizuri.

Mheshimiwa Keissy naomba nikuhakikishie, Ofisi ambayo inaongozwa na kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Mpango imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba inafanya utaratibu mzuri, kila mtu atalipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize tena; na sababu ni kwamba katika kada zote, kila mtu atawekewa utaratibu mzuri ilimradi kodi tupate shilingi trilioni 29.54 kutimiza matakwa ya bajeti yetu. Naomba tushirikane na Serikali kwamba wale wenye sheli za mafuta waweke mashine za mafuta na kila mtu atumie mashine za *EFD* katika Halmashauri zote, tutumie elektroniki na kila utaratibu, kwamba Mheshimiwa Dkt. Mpango ametuwekea utaratibu kuona jinsi gani tutafanya tukusanye kodi kila mtu alipe kodi bila kukwepa kodi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo!

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Tatizo la kusumbuliwa akina mama lishe limekuwa kubwa sana katika maeneo mbalimbali ndani ya nchi yetu. Siyo siri, tunapozungumzia mama lishe, sana tunawagusa akina mama na wale wajasiriamali wadogo wadogo. Wewe, mimi na Waheshimiwa Wabunge wote tutakuwa mashahidi kwamba hawa akina mama ndio wapigakura wa Chama cha Mapinduzi. Ni nini sasa agizo la Serikali kuhakikisha hawa akina mama lishe wanatengewa maeneo maalum ya kufanyia biashara zao katika Halmashauri zote ndai ya nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI), majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli akina mama lishe wakati mwingine wanapata changamoto kubwa sana. Kibaya zaidi ni pale utakapoona Mgambo anakwenda kuchukua jungu la mama lishe halafu wanakusanyika pembezoni wanakwenda kula kile chakula cha mama lishe. Hili jambo linakera sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana siku moja nilipokwenda katika Soko lile la Ilala pale nilitoa maelekezo kwamba tuone jinsi ya kuwarasimisha vizuri tuwaweke katika utaratibu mzuri. Hilo ni moja.

Sehemu nyingine hata wakati mwingine kunaweza kuwa na utaratibu mzuri, Halmashauri zimejenga vibanda kwa akina mama lishe, lakini kuna baadhi ya watumishi wasiokuwa waadilifu, wanatumia vile vibanda wanakodisha akina mama lishe kwa pesa kubwa sana. Jambo hili tumelikemea pale Ilala na sehemu mbalimbali, lakini suala la upangaji wa haya maeneo ni kama nilivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane na Halmashauri zetu, tutenge haya maeneo, tuyaweke vizuri ilimradi kwanza wale akina mama waliokuwa wanafanya kazi zao katika maeneo ya jua; waliokuwa wanafanya kazi zao katika maeneo yasiyo rafiki; bajeti zile zikifika katika mwaka huu wa fedha tutakaokuja nao, katika Ofisi ya Rais TAMISEMI ambao ndiyo jukumu letu kubwa kuzisaidia Halmashauri, hatutasita kuipa mipango ili kipaumbele ilimradi hawa akina mama waweze kupata fursa ya kufanya kazi zao katika mazingira rafiki; kwa sababu hata katika suala zima la afya itasaidia kupambana na magonjwa ya kipindupindu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Sikudhani, naomba nikwambie kwamba nitashirikiana na wewe na ninajua kwamba Tunduru ndiko unakotoka, kule

bainisheni hilo, tutaweka kipaumbele ilimradi wananchi waweze kupata fursa na akina mama wapate fursa nzuri za kiuchumi.

**NAIBU SPIKA:** Kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa, ni Mheshimiwa Sikudhani Chikambo. Mheshimiwa Zacharia Issaay!

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Pamoja na jitihada nzuri za Mheshimiwa Rais wetu; na pia pamoja na harakati kubwa ya kuwajengea Watanzania nia njema ya kulipa kodi; kwa kuwa Mheshimiwa Rais wakati wa Uchaguzi na katika Kampeni zake aliahidi kuondolewa kwa tozo ndogo ndogo kutokana na wafanyabiashara wadogo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni kuwa ina kila sababu ya kutazama upya Ilani ya Chama cha Mapinduzi na makundi gani yanasamehewa katika hizo tozo ndogo ndogo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI), majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, katika vipindi tofauti, Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais na timu zote tulipokuwa tukinadi ilani na Mheshimiwa Rais aliahidi kundoa hizi tozo ndogo ndogo ambazo zimekuwa kero kwa wananchi; kwamba mboga mboga, nyanya nini imekuwa ni kero kubwa zaidi. Kwa sababu kodi hizi zinatozwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa Sura Na. 290, ndiyo maana tumefanya maelekezo sasa; kuna mchakato unakwenda kwa ajili ya kurekebisha sheria zetu tuone ni jinsi gani sasa tutakusanya katika kodi zile kama *crop cess* na maeneo mengine lakini kuondoa usumbufu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili lipo katika mchakato na wadau mbalimbali ndiyo wanaweka maoni yao sawasawa na mwisho wa siku sheria hiyo itakuja katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; tuipitishe sisi sote kwa pamoja, tufanye *amendments,* tushauri, turekebishe, mwisho wa siku ni kwamba mwananchi wa kawaida atakuwa ameguswa na matamko ya Mheshimiwa Rais alipokuwa akinadi na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kama tulivyoelekeza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, sasa aulize swali lake.

Na. 463

**Kuliendeleza Bonde la Mto Ruhuhu – Ludewa**

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA** aliuliza:-

Bonde la Mto Ruhuhu lililopo katika Kata ya Ruhuhu Wilaya ya Ludewa ni eneo muhimu sana, linaweza kuzalisha mazao mengi na kupunguza uhaba wa chakula Tanzania:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza bonde hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Francis Ngalawa, Mbunge wa Jimbo la Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Bonde la Mto Ruhuhu linalojumuisha Kata ya Manda, Wilayani Ludewa Mkoa wa Njombe na Kata ya Lituhi Wilayani Nyasa katika Mkoa wa Ruvuma kwa kilimo cha mazao ya aina mbalimbali yakiwemo mpunga, mahindi, mihugo na mboga mboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maandalizi ya uendelezaji wa bonde hilo, upembuzi wa awali ulifanyika kati ya mwaka 2013 na 2014 na kubaini uwezekano wa kujenga bwawa kubwa katika eneo la Kikonge kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kudhibiti mafuriko katika Bonde la Mto Ruhuhu, kuendesha kilimo cha umwagiliaji kwa eneo la takriban hekta 4,000 na kufua umeme mkubwa utakaounganishwa kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika ipo katika hatua ya kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa eneo hili pamoja na kuweka miundombinu ya umwagiliaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deogratias Ngalawa, swali la nyongeza!

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na umuhimu mkubwa wa bonde hili ikiwa ni pamoja na kufua umeme ili kuweza kupeleka katika Gridi ya Taifa: Je, ni lini Serikali itaona kuna umuhimu wa kuitengea hela bila kutegemea ufadhili?

La pili; katika Wilaya ya Ludewa kuna mabonde kama ya Bonde la Mkiu na Bonde la Lifua: Je, ni lini Serikali itaiwekea mpango mkakati ili mabonde haya yaweze kutumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza, Mheshimiwa ameshauri kwamba ni lini Serikali itaacha kutegemea wafadhili katika kutekeleza miradi yake. Nimfahamishe Mheshimiwa Ngalawa kwamba mwaka 2006/2007 tulianza programu ya utekelezaji wa maendeleo ya Sekta ya Maji kwa kushirikiana na marafiki na wadau mbalimbali wenye nia nzuri ya kutusaidia sisi Watanzania. Programu hiyo ya kwanza iliisha mwezi Desemba, 2015. Januari mwaka huu, tayari tena tumesaini *memorandum* ya utekelezaji wa maendeleo ya maji kwa kushirikana na wadau hao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hatua hii, kwa sababu tuna *memorandum* tayari, hatuwezi kusema Watanzania tujitenge peke yetu. Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana nao katika utekelezaji wa miradi ya maji ikiwemo ya umwagiliaji kwa kushirikiana na fedha ya Seikali ya Tanzania ambayo ni kodi ambazo Mheshimiwa Rais amesisitiza kwamba tulipe ili tufanye miradi ya maendeleo pamoja na wafadhili. Pia Mheshimiwa Mbunge ujue, bila wewe mwenyewe kutenga fedha, wafadhili hawawezi kukusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ni kwamba ni lini sasa? Yapo maeneo mengi yanayofaa kwa umwagiliaji, Serikali itahakikisha kwamba inajenga miundombinu. Ni kwamba nchi yetu tayari ilishafanya utafiti kwamba tuna hekta zinazofaa kwa umwagiliaji milioni 29.4 na kati ya hizo, hekta 461,000 zimeshaendelezwa na zinafanya kazi. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba hekta zote tumezikamilisha tumeziwekea miundombinu ya umwagiliaji ili tuweze kuondokana na tatizo la maji pamoja na tatizo la njaa. Katika hiki kipindi cha miaka mitano cha Awamu ya Tano, tumepanga kuhakikisha kwamba tunajenga miundombinu, tunapata hekta milioni moja kuendeleza Sekta ya Umwagiliaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saddiq!

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa maeneo ya Ludewa yanafanana sana na maeneo ya Mvomero katika kilimo na kwa kuwa tuna miradi mingi ya umwagiliaji katika maeneo ya Kata za Kanga, Mkindo, Sungaji, Lukenge, Dakawa na Mlali; na baadhi ya miundombinu ilishajengwa, lakini Serikali haijatoa fedha za kumalizia miradi hiyo: Je, Mheshimiwa Waziri, uko tayari kufuatana nami mara baada ya Bunge hili, uende ukaone fedha ambazo zimetumika na nyingine zinazohitajika ili miradi ile ikamilike na ilete tija kwa wananchi wa Mvomero na Taifa kwa ujumla? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu!

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anasema kama tuko tayari kwenda kuangalia maeneo ambayo yanafaa kwa umwagiliaji. Hiyo tuko tayari. Nataka niongezee, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, anasema ni lini Serikali itaacha kutegemea wafadhili? Katika bajeti ya mwaka huu ambayo Waheshimiwa Wabunge mmepitisha kwenye Sekta ya Maji, asilimia 75 ni fedha ya kwetu wenyewe. Kwa hiyo, huo ndiyo mwelekeo, kwamba wafadhili wameshaanza kupunguza misaada katika miradi yetu ya maendeleo. Kwa hiyo, tunakwenda huko. Tutafika mahali tutafanya miradi yetu kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ignas Malocha, swali la nyongeza!

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Katika Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji ya 2016/2017, miradi mingi ya umwagiliaji iliyokuwa imeanza katika hatua za awali katika Halmashauri zetu na kuombewa fedha haikupangiwa fedha; kwa mfano, katika Jimbo langu, mradi wa Nkwilo, mradi wa Uzia, mradi wa Nzogwe, mradi wa Mkanga na mradi wa Momba.

Je, Serikali ina mpango gani mbadala wa kuifanya miradi hii iweze kuondelea ili wananchi waweze kuondokana na tatizo la njaa na kukuza uchumi wao na Taifa zima kwa ujumla?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu!

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mipata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli miradi mingi haikupangiwa fedha kwa mwaka huu na tulifanya hivyo kwa sababu ndiyo kwanza tumeanzisha hii Tume ya Umwagiliaji.

**MHE. MBUNGE FULANI:** Ni Mheshimiwa Malocha sio Mheshimiwa Mipata!

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Tukasema kwanza tumalize miradi ambayo tayari ilikuwa inaendelea. Katika mwaka utakaofuata, miradi hiyo yote tutakwenda kuiangalia na kuipangia fedha ili iweze kumalizika. Kwa hiyo, lazima twende kwa hatua, lakini kwa sababu ya ufinyu wa bajeti tulianza kwanza na miradi ambayo ilikuwa inaendelea, lakini nikuahidi kwamba katika mwaka utakaofuata tutakwenda kuikamilisha miradi iliyobakia.

**MHE. MBUNGE FULANI:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika!

**NAIBU SPIKA:** Kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa, anaitwa Mheshimiwa Ignas Malocha. Mheshimiwa Hamida Abdallah, swali la nyongeza!

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kuna dharura kubwa iliyojitokeza katika Manispaa ya Lindi; na juzi niliizungumzia hapa ndani ya Bunge lako tukufu; lakini taarifa ambazo anapewa Mheshimiwa Naibu Waziri wetu, siyo sahihi kwa sababu dharura hii ni kubwa sana na wananchi wa Lindi wanahangaika, hawana sehemu nyingine ya kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba Kisima cha Mitwero pampu imekufa na chanzo cha Mambulu kimejaa matope kiasi kwamba hakiwezi kutoa maji, wananchi leo wanahangaika na wananunua dumu moja shilingi 1,000/=. Hili ni tatizo kubwa sana! Namwomba Mheshimiwa Waziri wetu atuambie, atatusaidiaje ili kutatua hii kero ya maji wananchi waweze kuondokana nayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu!

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli pale Mji wa Lindi kumekuwa na matatizo kwa sababu ya uchakavu wa miundombinu ya maji ya muda mrefu, ndiyo maana Serikali imebuni na inaendelea kujenga mradi wa kumaliza tatizo hilo. Tatizo la maji kwa Mji wa Lindi litakwisha ikifika mwezi wa Kumi, huu mradi ambao unaendelea utakuwa umekamilika.

Mhesimiwa Naibu Spika, kwa hii dharura ambayo imejitokeza, kwa sababu yale mabomba yanapita chini ya maji na hatuwezi ku-*control* kwa sasa nguvu ya maji kwenye ile bahari, kwa hiyo, mara kwa mara yale mabomba yamekuwa yanakatika. Ninapeleka wataalam wangu wakasaidiane na wataalam walioko pale Lindi ili tumalize angalau kwa dharura wananchi wa pale waendelee kupata maji. Ufumbuzi wa kudumu ni ule wa kukamilisha mradi ambao tunaendelea kuusukuma kwa nguvu zote tuweze kuumaliza wananchi wa Lindi waweze kupata maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, hapo ndiyo umeshawaagiza hao wataalam ama utawaagiza lini ili waende huko Lindi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba wapo tayari wanashughulikia hilo tatizo, hivi sasa wapo huko.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hamida, nadhani umepata hiyo taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri ameshawatuma wataalam huko.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati na madini, Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Magomeni, sasa aulize swali lake.

Na. 464

**Bei za Umeme**

**MHE. JAMAL K. ALI** aliuliza:-

Kwa miaka mingi nyuma *TANESCO* ilikuwa ndicho chombo kilichohusika katika kuuza na kupanga bei za umeme kwa wateja wake katika makundi tofauti ya wateja wake katika nchi yetu mpaka pale *EWURA* ilipoanzishwa na kuanza kufanya kazi:-

(a) Je, ni vigezo gani ambavyo *EWURA* inavitumia katika kupanga bei hizo?

(b) Je, kuna unafuu gani wanaopata kwa wateja wanaochukua umeme katika mikondo mikubwa ya KV 11, KV 33 na KV 132?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Magomeni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, *EWURA* hupanga bei ya umeme kwa kuzingatia gharama halisi za uendeshaji wa biashara kama ilivyobainishwa kwenye Sheria ya Umeme ya mwaka 2008. Bei hiyo ya umeme hupangwa kulingana na makundi ya watumiaji ili kila kundi libebe gharama zake.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* ina wateja mbalimbali ikiwa ni pamoja na wateja wa majumbani ambao ni *D1* na *T1*. Wateja wa viwanda vidogo vidogo ambao pia wanatumia msongo wa volti 400 na matumizi kwa mwezi ni zaidi ya uniti 7,500 ambao ni *T2,* lakini wateja wakubwa waliounganishwa katika msongo wa kati wa *medium voltage* yaani *T3* na *MV* na wateja wakubwa waliounganishwa katika msongo mkubwa *(high voltage: T3-HV)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, unafuu wanaopata wateja wanaounganishwa katika msongo mkubwa wa umeme ni kuwa na bei ya chini *(energy charge)* ukilinganishwa na wateja wadogo, hasa majumbani ambao ni *T1*. Unafuu huo unatokana na ghrama za usambazaji na upotevu wa umeme kuishia kwenye mfumo wa *HV* na *medium V,* yaani kilovoti 220, Kilovoto 132, KV 66, KV 33 pamoja na KV 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana bei za umeme zilizopo hivi sasa, mteja wa *T1* analipa shilingi 292/= kwa *unit* moja; mteja wa viwanda vidogo vidogo *(T2)* wanalipa shilingi 195/= kwa *unit* moja na mteja wa *T3-MV* analipa shilingi 157/= kwa uniti moja; na mteja wa *T3* yaani *high voltage* ikiwemo migodi mikubwa ya madini kama *GGM* na mingine, pamoja na *ZECO* wanalipa shilingi 152/= kwa *unit* moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, h□Hata hivyo, wateja wadogo wadogo, hasa wa majumbani ambao ni *D1* wanaotumia chini ya *unit* 75 kwa mwezi wanalipa shilingi 100/= kwa unit moja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, swali la nyongeza!

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nitakuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Moja, kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba kila mteja katika kila ngazi anabeba gharama zake. Je, Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba bei ambayo inatozwa Shirika la Umeme la Zanzibar yaani *ZECO*, ambaye ni mteja wa jumla *(bulk purchaser)* kwa *unity* moja ya *KVA* ambayo ni shilingi 16,550/= ambayo ni bei kubwa kuliko wale wateja wa reja reja wa ngazi ya kati na ngazi ya chini kuwa hii bei siyo stahiki kutozwa *ZECO*. Je, lini Serikali itaitaka *EWURA* sasa kufanya maboresho ya bei hii na kuitoza *ZECO* bei stahiki? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Jamali kwa kutukumbusha kwamba gharama za umeme zinatakiwa zishuke. Nimhakikishie tu kwamba kuanzia mwezi wa Nne tulipofanya marekebisho ya bei watumiaji wakubwa kabisa wakiwemo *ZECO* tuliwapunguzia kwa asilimia 2.4, ilikuwa ni punguzo kubwa kweli kweli ukilinganisha na wateja wengine wadogo wadogo. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Jamal kwamba bei za gharama kama nilivyosema, zinategemea hasa mambo mawili:-

Jambo la kwanza ni vyanzo vya kuzalisha umeme. Vyanzo vinapokuwa vya bei nafuu na bei ya umeme inapungua. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Jamal kwamba ni kweli kabisa kwa *unity* moja kwa sasa kwa watumiaji wakubwa ni shilingi 16 na 55 *unit,* lakini zitaendelea kupungua kulingana na gharama ya uzalishaji wa umeme unavyoshuka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jamal nakuhakikishia tutaendelea kulifanyia kazi na *EWURA* bado

wanaendelea na mchakato wa ku-*review* bei kulingana na gharama za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni lini sasa *EWURA* watafanya marekebisho hayo? Kwa sasa hivi tunazalisha umeme mwingi sana wa kutumia gesi na kwa kiasi kingine kikubwa kwa kutumia maji. Tumeeleza sana vyanzo vya gesi na jinsi ambavyo bei inaendelea kupungua. Kwa sasa hivi atupe muda tuendelee kuzalisha kwa vile ambavyo mmetupa bajeti, siyo muda mrefu, *EWURA* tena wataingia uwanjani kuanza ku-*review* bei. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jamal nikuhakikishie kwamba bei itaendelea kuangaliwa wakati hadi wakati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Seif Gulamali, swali la nyongeza!

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Naibu Waziri. Kwa kuwa tatizo la umeme lililopo Zanzibar linafanana sana na tatizo la umeme lililopo Igunga, sasa kwa sababu Naibu Waziri anatambua vizuri sana: Je, nini kauli ya Serikali juu malipo ya fidia kwa Kata za Chabutwa, Simbo pamoja na Mwisi ili waweze hasa kujua watapata lini hiyo fidia yao? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Niabu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Gulamali, jana na juzi tumehangaikia sana suala la fidia ya wananchi wako. Kama ambavyo tumelifikisha, kwanza nikupongeze. Sasa hivi mthamini wa ardhi wa Mkoa anapitia viwango vya fidia vya wananchi wa Manonga na hasa katika vijiji vya Chabutwa Simbo na maeneo ya jirani ambapo umetaja, ni kweli kabisa kuna wananchi 722 ambao hawajafidiwa na malipo hayo yako katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba jana wakati tunapitia, tulipoongea na Mkuu wa Mkoa wa Tabora nadhani alikwambia kwamba kabla ya mwezi ujao na miezi miwili ijayo wananchi wako watalipwa fidia. Kwa hiyo, nakuomba sana wafikishie taarifa waendelee kuwa na subira jambo la fidia yao linafanyiwa kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salum Rehani!

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na bei ya umeme bado Shirika la Umeme la Zanzibar *(ZECO)* halijapunguza bei ya umeme kitu ambacho kinawanyima fursa wananchi wa Zanzibar kuweza kutumia nishati hii au rasilimali hii kwa ukubwa zaidi kuliko hali inavyokuweko sasa hivi. Kwa sababu wengine wanashindwa kuunga umeme kutokana na hali

ya bei. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kukaa na *ZECO* ili kuona na kwamba na wao viwango vile vinaweza kupungua na kuwanufaisha wananchi wote kwa bei ya chini zaidi kama ilivyokuwa huku Tanzania Bara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kule *ZECO* kama ambavyo mnajua, wanajua umeme wa jumla na kwa vile wananunua umeme wa jumla, siyo rahisi sana wakaona punguzo la bei ya umeme. Hata hivyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko tayari kukaa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na *ZECO, TANESCO* na *EWURA* ili kuona ni jinsi gani sasa gharama za umeme zinaweza kupitiwa upya. Nitoe tu angalizo, gharama za umeme zinazingatia sasa vyanzo vyetu pamoja na gharama nyingine za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko tayari, tutakaa pamoja na wewe pamoja na *EWURA* ili pia kuangalia upya bei za umeme huko Zanzibar.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hongoli

**MHE. JORAM ISMAEL HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Lupembe, Kata ya Kidegembye tuna tatizo kubwa sana la umeme hasa tatizo la *low voltage*. *Transformer* iliyopo pale haiwezi kuzalisha umeme wa kutosha na hivyo kutoweza kusambaza umeme sehemu nyingi na wananchi wa pale hawawezi kufanya shughuli za kiuchumi kama vile *welding* na shughuli nyingine za kusaga nafaka. Je, ni nini kauli ya Serikali kutatua tatizo hili? Maana nimewaona watu wa *TANESCO* muda mrefu lakini mpaka leo hii tatizo hilo bado lipo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kama mlivyoona katika maeneo mengi, sasa hivi bado tunaendelea na harakati ya kusafirisha umeme wa msongo mkubwa wa *Kilovolt* 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Wizara yetu ina jumla ya miradi 42 sasa. Kati ya miradi 42, miradi 16 ni kwa ajili ya uzalishaji umeme wa gesi pamoja na usambazji wake; lakini miradi 11 ni kwa ajili ya miradi ya maji na kusambaza umeme wa maji. Miradi mingine minane ni kwa ajili ya vyanzo vingine na miradi saba ni rasmi kwa ajili ya usambazaji umeme mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukisema sana kwamba kuanzia sasa Wakandarasi wako *site* na kazi kubwa hasa maeneo ya Iringa, Njombe

Dodoma, Sumbawanga na mengine, tunaanza sasa mradi wa kusafirisha umeme wa *Kilovolt* 400. Kazi ya mradi huu kuongeza nguvu kubwa ili umeme sasa usiwe unakatikakatika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa sasa hivi tunatumia umeme wa *low voltage,* lakini tutakapokamilisha miradi hii mwaka 2018/2019 *low voltage* sasa itakuwa imekwisha kwa sababu itakuwa na umeme mkubwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wa Njombe pamoja na maeneo ya Lupembe na mengine ni kuhakikishie kwamba taratibu wa umeme kukatika zinachangiwa pia sasa na *low voltage* lakini kwa sababu tuna umeme mkubwa gharama hizo pia zitashuka lakini na umeme utakuwa haukatiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kama nilivyosema, maeneo mengine umeme unakatika siyo kwa sababu ya *low voltage* tu, ni kwa sababu ya miundombinu kuwa mibovu. Sehemu ya miundombinu ni pamoja na *transformer.*

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, mmepitisha Sheria ya Manunuzi na tumeshasema, kuanzia sasa *transformer* tutakuwa tunanunua hapa nchini kwa sababu shirika letu na kampuni yetu ya *TANELEC* sasa itakuwa na uwezo wa kutosha wa kutengeneza *transformer* na Serikali itanunua, kwa hiyo, matatizo ya *transformer* yatarekebika na kupunguza kabisa tatizo la kukatika kwa umeme. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Lucy Simon Magereli Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Mangungu.

Na. 465

**Kufungwa kwa Machimbo ya Madini ya Ujenzi**

**MHE. ISSA A. MANGUNGU (K.n.y MHE. LUCY SIMON MAGERELI)** aliuliza:-

Machimbo ya Madini ya ujenzi yaliyoko Kigamboni yanatoa malighafi muhimu sana inayosaidia ujenzi katika jiji la Dar es Salaam; machimbo haya yanatoa ajira kwa zaidi ya wakazi 6,000 na ndiyo machimbo yenye mwamba laini kwa Mkoa wa Dar es Salaam ukilinganishwa na madini yanayotoka Goba:-

(a) Je Serikali haioni kuwa utaratibu wa kuratibu zoezi la kufunga machimbo haya utakosesha ajira kwa watu zaidi ya 6,000?

(b) Je, kwa kufunga machimbo hayo, Serikali haioni kuwa inawanyima fursa wananchi wa Dar es Salaam na Pwani kupata madini ya bei nzuri na kuwapunguzia gharama za ujenzi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini hapa nchini hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010. Sheria hiyo imeweka utaratibu Maalum wa uchimbaji wa madini ikiwemo kuacha umbali wa mita 200 kutoka makazi ya watu yaani *bufferzone*.

Umbali huo umekadiriwa kitaalam kuzuia madhara yanayoweza kutokea kutokana na shughuli za uchimbaji hasa maeneo ya makazi. Kwa sababu hizo sasa, Wizara ya Nishati na Madini inafanya mipango wa kutathmini namna bora ya kuendelea uchimbaji madini ya ujenzi katika mkoa wa Dar es Salaam hasa bila kuathiri mazingira, afya pamoja na maeneo ya wakazi kama nilivyoeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaona umuhimu sasa wa kupanua fursa na kuwezesha wananchi wengi kushiriki katika shughuli za uchimbaji wa madini haya. Hata hivyo Serikali inachukua fursa hii kutoa wito kwa Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote kwa wachimbaji wote ili kuzingatia sheria zilizowekwa kwa mujibu wa sheria na kuongeza pato la Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu, swali la nyongeza!

**MHE. ISSA A. MANGUNGU**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, maeneo haya ambayo yanachimbwa madini yako mbali na makazi ya watu mfano Kimbiji na Chamazi, lakini Serikali imezuia. Je, umbali upi unaotakiwa kiasi kwamba mkafikia kufunga yale machimbo ya maeneo yale?

Swali la pili, madini haya sasa hivi yanatoka katika Mkoa wa Pwani hasa Wilaya ya Mkuranga. Je, kuna tathmini gani mmefanya kwamba machimbo haya sasa hivi hayataleta athari katika maeneo mliyoyapeleka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa maeneo ya Kigamboni kwa sasa yana madini aina ya ujenzi na hasa ya changarawe pamoja na kokoto. Maeneo yanayochimbwa kwa Kigamboni hasa hasa ni maeneo ya Mjimwema pamoja na Kijisu. Hata hivyo, eneo alilotaja la Kimbiji pamoja na Chamazi ni kweli kabisa kuna wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba siyo kweli kwamba tumesimamisha au tumefunga eneo la Kigamboni. Tulipofunga ni eneo la Kunduchi ambapo sasa wachimbaji tena ambao walikuwa kidogo ni haramu wanachimba kuelekea upande wa barabara. Kwa hiyo, pale Kunduchi tulisimamisha tena miaka minne iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimtahadharishe tu Mheshimiwa Mbunge kama nilivyosema, lakini namshukuru kwa kuwaulizia wananchi wa Kigamboni. Taratibu za Sheria ya Madini zinataka uache umbali wa mita 200 kutoka makazi, lakini kadhalika zinataka uache umbali wa mita 100 kutoka vyanzo vya ziwa au bahari kama *ferry* ya Kigamboni ilivyo na inataka uache umbali wa mita 100 kutoka umbali ambako sasa kiwanja cha ndege kitajengwa au *city* itajengwa. Sasa kwa Kigamboni kuna eneo kubwa ambalo limeainishwa kwa ajili ya *satellite city.* Eneo lile tumezingatia Sheria ya Madini kuacha umbali wa mita 100 usiopungua 100 hadi 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu sasa kule kigamboni tunatenga eneo rasmi la Mjimwema pamoja na maeneo ya Mkuranga aliyosema ya Visiwasiwa, pamoja na maeneo mengine ya kule Kibaha kwa Mathias na kwa Mfipa. Maeneo hayo tunayatenga kwa ajili ya wananchi wa Dar es Salaam ili wapate maeneo rasmi sasa ya kuchimba madini ya mchanga kwa ajili ya shughuli za ujenzi.

Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Mbunge, tutakaa pamoja na utendaji wako ili tubainishe maeneo ambayo tutachimba kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa Kigamboni.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, swali la nyongeza!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Wakala wa Madini (*TMAA)* wanafanya kazi nzuri sana. Mwaka 2010 na mpaka mwaka 2015 waliweza kukamata madini yenye thamani ya Dola bilioni mbili, lakini pia kwa upande wa shilingi, jumla ya shilingi bilioni 64 zilikamatwa. Je, kwa utaratibu huo huo Serikali

ina mpango gani wa kuzuia wachimbaji katika migodi hasa katika usafirishaji wa ule mchanga kwenda kupimwa nje?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kabisa sasa hivi mchanga wote wa *concentrate,* yaani *copper concentrate* na hasa unaotoka kwenye mgodi mkubwa wa Bulyanhulu unasafirishwa kwenda ama China ama Japani. Sababu kubwa ya kufanya hivyo ni kwa sababu hapa viwanda vya kuchenjua dhahabu na kuachanisha madini, havijajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namwambie Mheshimiwa Ndassa, ni kweli kabisa uwekezaji huu unahitaji mitaji mikubwa; na siyo chini ya Dola 1,000 kuanzisha mradi wa kuchenjua madini hapa nchini. Hata hivyo, kama Serikali, tunatambua sana mchango wa *TMAA* mamlaka yetu. Kweli kabisa kwa kutumia *TMAA* imedhibiti asilimia kubwa sana ya upotevu wa madini ambao ulikuwa unatokea hapo nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkumbushe tu Mheshimiwa Ndassa kwamba ni kweli, mwaka 2015, migodi mikubwa kama *GGM* ililipa shilingi milioni 117 kama dola kwa ajili ya *royalty.* Hii kutokana na kazi ya *TMAA*. Pia *local levy* iliyolipwa ni dola bilioni 4.7 za Marekani, hiyo ni kutokana na udhibiti wa *TMAA*.

Kwa hiyo, Serikali tunaendelea sasa kuangalia uwezekano wa kuhamasisha wawekezaji wakubwa kuanza sasa kujenga viwanda vya kuchenjua dhahabu hapa nchini. Hata hivyo, itachukua muda, bado Serikali tunalifanyia kazi. Hii ni kwa sababu inahitaji mitaji mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la Mheshimiwa Ndassa tumelichukua, tutalifanyia kazi kama ambavyo Mheshimiwa Ndassa tunashirikiana, tunakushukuru sana. *(MakofI)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Bashe, swali la nyongeza!

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nataka kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mgodi mkuu uliokuwepo katika Mji wa Nzega wa *Resolute* ulishafungwa na kwenye ripoti ya *TMAA* inaonyesha Mwekezaji huyu aliondoka na fedha za Halmashauri ya Mji wa Nzega, *ten billion shillings* ambazo zilikuwa ni *service levy:* Je, kama Wizara, imefikia wapi kulifuatalia suala hili kuhakikisha haki hii ya wananchi wa Mji wa Nzega inarudi? ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Bashe nakushukuru sana. Kama unatukumbusha kwamba kampuni iliondoka na *ten billion* sasa umetupa taarifa, tutalifanyia kazi. Mimi na wewe pamoja na wataalamu na vyombo vingine tutashirikiana pamoja, tutalifanyia kazi ili pesa ziweze kurejea. Kwa hiyo, nakushukuru Mheshimiwa Bashe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 466

**Viwanda Vinavyozalisha Nguo aina ya Khanga**

**MHE. AMINA NASSORO MAKILAGI** aliuliza:-

(a) Je, Viwanda vinavyozalisha nguo aina ya khanga vipimio vyake na ubora wake vinafaa kwa matumizi ya wanawake wa Kitanzania?

(b) Je, upande wa khanga kwa kila kiwanda ni mita ngapi?

(c) Je, malighafi gani inayotumiwa kuzalisha khanga kati ya pamba, uzi wa katani, uzi wa nailoni, au uzi wa sufi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vipimo vya ubora wa khanga zinazozalishwa na viwanda hapa nchini, vinafaa sana kwa matumizi ya wanawake hapa Tanzania. Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia shirika la viwango Tanzania *(TBS)* limetoa viwango elekezi vya uzalishaji wa khanga kwa kutumia pamoja na nyombo vingine ni 16165 ya 2009. Viwango hivi vimezingatia mahitaji ya watumiaji na matakwa ya wataalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa khanga kwa kila kipande unatofautiana kutoka kiwanda kimoja hadi kingine.

Aidha, kiwango cha *centimeter* 165 cha 2009 kinaelekeza upande wa khanga uwe wa kipimo kisichopungua urefu wa *centimeter* 165 na upana wa

*centimeter* 116. Hata hivyo, kila kiwanda kinachozalisha khanga kinapaswa kuzingatia vipimo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, khanga husokotwa kwa kutumia malighafi za nyuzi pamoja na pamba. Hata hivyo, katika umaliziaji wa kipande hicho hutengenezwa kwa kutumia asilimia 100 lakini *polyester* kwa asilimia 100 au mchanganyiko wa pamba pamoja na *polyester*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, swali la nyongeza!

**MHE. AMINA NASSORO MAKILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa khanga hii ni vazi ambalo mwanamke wa Kitanzania analivaa akiwa nyumbani, ni vazi ambalo analivaa akiwa shambani analima, ni vazi ambalo analivaa anapokuwa kwenye shughuli za kijamii kwenye misiba na kwenye shughuli za harusi, ni vazi ambalo mama anakuwa nalo hata anapokwenda leba. Ni vazi ambalo linampokea mtoto hata anapotoka leba. Ni vazi rasmi la Mwanamke wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanga ambazo zinatengenezwa katika viwanda vyetu vya Tanzania kwa kiwango kikubwa hazikidhi mahitaji ya wanawake wa Tanzania na hasa kwa kuzingatia kwamba vipimo vinavyotumika na ukilinganisha upana na viwango walivyonavyo wanawake wa Tanzania. Wanawake wa Tanzania wanaishi kwa amani na utulivu wako sawa katika afya zao, kanga wanazozivaa haziwatoshi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna baadhi ya viwanda hata hizi sentimita zilizozungumzwa hawafikii; unakuta urefu ni wa mita 100, sentimita 120 kwa kweli ukiangalia hata wewe mwenyewe haikutoshi hata kwa urefu peke yake. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa swali langu la kwanza, kwa kuwa vazi hili kwa kweli ni vazi la mwanamke wa Kitanzania. Matokeo yake wanawake wameanza kuvaa kanga zinazotoka India na China, wanawake sasa wamehamia kwenye madera, jambo ambalo kwa kweli hawakuzoea, ningependa kujua sasa Serikali inamkakati gani wa kuhakikisha inaielekeza *TBS* (Shirika la Viwango Tanzania) ili kufuatilia vazi hili, liendane na ubora halisi wa maumbo ya wanawake wa Kitanzania na hasa kwa kuzingatia kwamba kanga hii hata ukiivaa inateleza haifungiki sasa hivi; kwa hiyo hata malighafi wanayoitumia siyo pamba. *(Makofi)*

Swali la pili, ningependa kujua sasa kwa sababu hili vazi la kanga limekuwa ni dogo, na wanawake wameamua kuachana nalo kwa kuwa

haliwatoshi, wameamua sasa kuhamia kwenye madera na kanga kutoka China na India. Ningependa sasa kujua Serikali ina mkakati gani kwa sababu sasa vazi la dera limekuwa likiwapendeza wakina mama na ni vazi la heshima, ina mkakati gani sasa la kuhamasisha viwanda vya hapa nchini vitengeneze dera badala ya kuwanufaisha mataifa ya mbali? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri huyu mama alipewa upendeleo maana alikuwa anaongea kwa niaba ya wamama Tanzania nzima. *(Kicheko/Makofi/Vigelegele)*

Kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amina Makilagi, Mbunge maalum na machachari kwa akina mama kama ifuatavyo:- *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kama Serikali ni kweli, kwanza nitambue viwanda tulivyonavyo hapa nchini vingi kabisa tulivirithi toka ukoloni na vichache tulivijenga miaka ya 1970 na vingine miaka ya 1980. Viwanda ambavyo tunavyovitambua kama *Mwatex, Murutex,* Urafiki, ni vya Nida ndiyo vimeongezeka hivi karibuni. Kwa hiyo ni kweli kabisa viwango vyake ni vya chini na hiyo ninakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hatua ambazo Serikali imechukua sasa kwa kutambua mabadiliko ya maendeleo siyo mabadiliko ya uchumi tu hata makuzi ya binadamu. Kwa hiyo ninatambua *size* za kina mama na hata akina baba, akina baba na nyie mko wapi? Na zenyewe zinakuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kwanza ambayo Serikali imechukua viwango vilivyowekwa na *TBS* vinavyotumika sasa kwa upande wa nguo za kanga kama nilivyosema ni urefu wa sentimita 165 na upana sentimita 116. Lakini kwa upande wa vitenge urefu wa sentimita 200 na upana wa sentimita 116; lakini ni viwango vya mwaka 2009. Kwa hiyo sasa *TBS* mkakati wa kwanza kabisa inafanyia maboresho viwango hivyo, akina mama sasa mkae tayari kuvaa viwango vikubwa vya nguo. Viwango vinapitiwa na vitaanza kutumika mwezi Juni, mwakani.

Kwa hiyo akina mama Mheshimiwa Mwakilagi nikupongeze sana; Mheshimiwa Naibu Spika hata wewe nadhani unaendelea kukua utavivaa mwaka 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Pili ambao sasa Serikali inafanya, imetenga maeneo maalum kwa ajili ya viwanda vitakavyokuwa vinazalisha sasa nguo aina mbalimbali, vikiwemo vitenge vya kuvaa lakini hata ambavyo vimeshonwa, wametenga hekta 2100 kule TAMCO - Kibaha, pamoja na hekta 431 kule Kigamboni. Kwa hiyo Waheshimiwa akina mama taratibu za kiserikali zinafanyika kuwahakikishia sasa mtavaa nguo bila wasiwasi.

Kuhusiana sasa na madera ni kweli kabisa hata sisi akina baba tunashangaa, unaona akina mama wanavaa madera kila sehemu, kumbe ni kwa sababu hata nguo za kuwabana sasa siyo *fashion* tena. Sasa hatua za Serikali za makusudi kabisa ambazo imezichukua, sasa hivi vipo viwanda vitatu vinavyozalisha nguo za kuvaa, kiwanda cha kwanza ni cha *TUKU* ambacho kipo pale Mabibo, lakini viwanda vingine pamoja na *Sunflag*, pamoja na kile kiwanda cha Mzava karibu na maeneo ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mavazi aina ya madera Serikali imekaribisha wawekezaji wa Kichina na Kihindi ili waje wawashonee nguo sasa aina ya madera akina mama mnayoyataka. Kwa hiyo Serikali imeshachukua hatua asante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani swali la kanga limejibiwa kwa kirefu sana, tunaendelea Waheshimiwa. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe sasa aulize swali lake.

Na. 467

**Barabara ya Butego Lumasa – Iparamasa – Mbogwe mpaka Masumbwe**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Barabara ya Butengo Lumasa – Iparamasa – Mbogwe – Masumbwe ni barabara muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wa Wilaya ya Mbogwe na Mkoa wa Geita kwa ujumla:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia usanifu wa kina na upembuzi yakinifu barabara hii na hatimaye kuijenga kwa kiwango cha lami?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Butengo Lumasa – Iparamasa – Mbogwe hadi Masumbwe yenye urefu wa kilometa 95 ni barabara ya mkoa inayounganisha barabara kuu za Isaka – Lusahunga na Usagara – Biharamulo na pia inaunganisha Wilaya za Mbogwe na Chato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sasa haijafikiria kuiingiza barabara hii katika mpango wa kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na hatimaye kuijenga kwa kiwango cha lami barabara hii. Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Geita inaendelea kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali barabara hii kadri ya upatikanaji wa fedha ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya shilingi milioni 100 zilitumika katika matengenezo ya kawaida na katika mwaka 2015/2016 kiasi cha shilingi milioni 300 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya kawaida na shilingi milioni 345 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara hiyo na kazi zinaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele swali nyongeza.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri nazoendelea kuzifanya za Taifa letu. *(Makofi)*

Swali la kwanza kutokana na umuhimu wa barabara hii katika Mkoa wa Geita; je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutembelea katika Mkoa wa Geita na kuipitia hii barabara ili aone uwezekano wa kuiingiza barabara hii katika kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili hatimaye iweze kujengwa kwa kiwango cha lami?

Swali la pili, Mheshimwia Rais wetu kwa nyakati tofauti akiwa Waziri wa Ujenzi na alipoteuliwa kuwa mgombea wa Chama chetu cha Mapinduzi, aliahidi ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilometa tatu katika Mji wa Masumbwi; je, Serikali ina mpango gani sasa kutimiza ahadi hizi za Mheshimiwa Rais wetu?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Masele amenialika nitembelee katika mkoa wake, nataka kumuhakikisha nitatembelea nitatembelea mkoa huo na kuangalia barabara anayoisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kipindi kifupi nilichoingia kwenye Wizara hii, tumetembelea takribani mikoa kama 23 ya Tanzania Bara kuangalia barabara mbalimbali. Tunaamini baada ya miezi miwili inayokuja tutatembelea

mikao yote ya Tanzania na kuangalia barabara zetu kuhakikisha kwamba tunazitengeneza kama tunavyopanga mikakati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, alitaka kufahamu Mheshimiwa Rais, aliahidi kujenga kilometa tatu (3). Ni kweli Mheshimiwa Rais ameahidi maeneo mbalimbali kujenga, kwingine kilometa tatu (3), kwingine kilometa tano (5); sisi kama Wizara tumezichukua ahadi zote hizo za Mheshimiwa Rais na tumeziweka kwenye mpango wetu na tunahakikisha kwamba barabara hizo tutazijenga kwa awamu, itategemea upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia muda wa kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema amefika mikoa hii 23, kwanza nimshukuru sana kwa kuweka *plan* ya kujenga barabara ya Mbulu - Karatu, Mbulu - Haydom - Singida kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini sasa Serikali itaanza kujenga barabara hii kwa kuanzia na upembuzi yakinifu? Ahsante sana.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwenye mpango wetu tumeweka barabara hii na hatua inayofuata sasa hivi ni kufanya *feasibility study* na *detail engineering design* tutafanya tu pale tutakapopata hela sasa hivi tupo katika mchakato wa kutafuta hela mara hela hizo zitakapopatikana nataka kuhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutakuja kuifanya kazi hiyo ili hatimaye tuijenge kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mipata.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Nakusukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Awamu ya Nne alitoa ahadi ya ujenzi wa barabara kutoka Kitosi kwenda Wampembe na barabara kutoka Nkana kwenda Kala na alitoa ahadi kwamba barabara hizi zitapandishwa hadhi ili ziweze kupitika kipindi chote cha mwaka, na kwa bahati mbaya sana katika mwaka huu barabara hizi bado hazi bado hazikutengewa fedha za kutosha na Halmashauri haina uwezo wa kutosha kuzihudumia.

Je, Serikali ina mpango gani katika kuhakikisha kwamba ahadi ya Rais huyu inabaki na heshima na fedha ziweze kupatikana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mpatakama ifuatavyo:-

Ni kweli kuna barabara nyingi Tanzania ambazo zinahitajika kupandishwa hadhina tuna barabara pale ofisini, karibu 150 ambazo zinatakiwa kupandishwa hadhi. Barabara hizi ukizipandisha hadhi maana yake ni kutafuta fedha ili uweze kuweka katika viwango vya barabara za *TANROADS*.

Lakini nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, wakati tutakapoanza mchakato wa kuzipandisha hadhi barabara hizo na barabara zako tutaziangalia kwa sababu tunaamini kwamba barabara zako ni muhimu sana kwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Doto Biteko.

**MHE. DOTO M. BITEKO**:Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema mpango wa kujenga ile barabara ya Butengo Lumasa kwenda Masumbwe haupo kwa sasa na kwa sababu Mkoa wa Geita barabara ya Katoro - Ushirimbo ambayo inaunganisha Wilaya tatu za Mkoa wa Geita iko kwenye ngazi ya *TANROADS.*

Je, Serikali haioni muda umefika sasa barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Katoro - Lulemba - Ushirombo yenye kilometa 56 ni barabara muhimu ambayo inaunganisha Wilaya tatu za Mkoa wa Geita. Sisi kama Serikali tumeitengea pesa barabara hii kila mwaka; kwa mfano mwaka huu wa fedha 2016/2017 tumeitengea takribani shilingi bilioni 1.25 kwa matengenezo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge hapo baadaye tutakapopata fedha ya kutosha tutaifanyia *feasibility study* na *detail engineering design* barabara hii na hatimaye tuijenge kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha Mbunge wa Serengeti, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Wabunge wasiotii Bunge lako Tukufu na waliotoka nje, naomba swali namba 468 la Mheshimiwa Marwa Chacha Ryoba, Mbunge wa Serengeti lijibiwe.

Na. 468

**Kuwepo kwa Vifo Vyenye Utata wa Kisiasa**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA (K.n.y MHE. MARWA R. CHACHA)** aliuliza:-

Kumekuwepo na vifo vyenye utata wa kisiasa lakini inapotokea mpinzani kupoteza maisha havipewi kipaumbele katika upelelezi na hatua zinazochukuliwa:-

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi Tanzania inathamini maisha ya raia wake wote bila kujali rangi, kabila, itikadi za kidini na itikadi za kichama. Jeshi la Polisi linafanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo ambapo katika utekelezaji wa majukumu yake hatua mbalimbali huchukuliwa ili kuhakikisha haki inatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikichukua hatua stahiki za kisheria kwa kila aina ya mauaji yanayotokea kwa raia na endepo mazingira ya mauaji yatakuwa yanalihusu Jeshi la Polisi basi Tume huru huundwa ili kuchunguza na kutoa ushauri kwa mamlaka husika na hatua stahiki huchukuliwa dhidi ya wahusika hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutimiza wajibu wake wa kuwalinda wananchi wake pamoja na mali zao bila upendeleo wowote.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Upinzani vimekuwa vikileta vurugu, kutotii amri ya halali za Serikali na Jeshi la Polisi na wakati mwingine kuleta vurugu, kwa mfano, katika Jimbo langu la Ulanga kwenye kijiji cha Iputi - Nambuga walichoma nyumba sita za wananchi. Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na suala hili, ili kutokomeza kabisa tabia hii.

Pili, kumekuwa na Wabunge, wakileta uchochezi wa kisiasa katika maeneo yetu ya makazi. Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na Wabunge kama hawa?*(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Jeshi la Polisi limekuwa likitekeleza kazi zake kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni kama ambavyo nimeeleza katika jibu la msingi. Kwa maana hiyo basi, katika kutekeleza wajibu wake huo Jeshi la Polisi halibagui mtu yoyote na lina thamini vilevile maisha ya Watanzania wote kwa mujibu wa Ibara ya 14 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na limekuwa likichukua hatua stahiki mbalimbali kwa uhalifu wa aina yoyote iwe kutoka katika Vyama Vya Siasa ama raia wa kawaida.

Kwa hiyo, nilitaka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mlinga kwamba kuna hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa na viongozi ambao wamekuwa wakitoka katika vyama vya siasa wakishiriki katika vitendo vya uhalifu. Mfano halisi ni katika matukio ambayo yanajitokeza sasa hivi Pemba, miongoni mwa watu ambao wameshikiliwa na polisi kwa tuhuma za kuchochea vurugu Kisiwani Pemba wapo ambao walikuwa na nafasi kubwa za uongozi katika vyama vya siasa na katika chombo cha kutunga sheria.

Kwa hiyo, hiyo inadhihirisha kwamba Jeshi la Polisi halibagui mtu na atashughulikiwa mtu kwa mujibu wa matendo yake na siyo kwa mujibu wa *affiliation* yake ya siasa ama rangi, dini, kabila la mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana na Wabunge kushiriki katika vitendo vya kihalifu ni kama nilivyozungumza katika swali la nyongeza la mwanzo kwamba iwe Mbunge, mwanachama wa kawaida, kiongozi wa chama cha kisiasa kitakachoamua hatua za kuchukuliwa ni matendo yake na niseme tu kwamba kwa kuwa umegusia suala la Wabunge wao wana haki zao kwa mujibu wa Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge yanamlinda Mbunge kwa kila ambacho anakisema Bungeni lakini haimlindi Mbunge kwauhalifu wa aina yoyote wa jinai iwe ndani ya Bunge ama iwe nje ya Bunge.

Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kuwasihi sana wanasiasa hasa viongozi ikiwemo Wabunge kuwa makini sana na kauli zao na matendo yao kwani yanaweza kuchochea uvunjifu wa amani katika nchi yetu.

Lakini pia nichukue fursa hii kuwanasihi wananchi kuwa makini sana na kauli za wanasiasa ikiwemo viongozi wa siasa katika kuhakikisha kwamba wanafuata misingi ya sheria ya nchi yetu ili waweze kuepuka madhara yanayoweza kuwatokea katika maisha yao. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu sahihi na majibu yanayokidhi. Niongezee tu kipengele kile alichosemea kuhusu Wabunge na viongozi wa vyama vya kisiasa kuwa vyanzo vya vurugu na nieleweke wazi kwamba utaratibu ambao tutautumia kuanzia sasa kwa kupima kwamba kila kiongozi anawajibu wa kuhimiza amani katika Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikitokea uchochezi wa aina yoyote ambao na kiongozi yupo tutashughulika na kiongozi aliyewapeleka watu wengine kwenda kwenye matatizo hayo. Kwa sababu mara nyingi viongozi wamekuwa wakiwatanguliza watu wengine na kupata madhara kwa sababu wao hawaguswi na madhara yale. Kwa hiyo, tutakachofanya na nitaaambia vijana wangu kwamba kunapotokea na uchochezi hangaikeni na mzizi wa tatizo ambaye ni kiongozi aliyesababisha watu waende katika matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisema kwamba watanzania pamoja na hao ambao hawajasoma vitabu vya historia vinavyoelezea udikteta ni nini wasichanganye udikteta na msimamo wa kusimamia sheria. Mimi niwape taarifa tu kama hawawajui madikteta niwape kwa taarifa zao dikteta huwa hatoi fursa hata ya kuambiwa wewe ni dikteta, huwezi ukamsema mtu wewe ni dikteta na ukaendelea kutembea kwenye *disco* upo, kwenye unywaji upo, kwenye sherehe upo, yaani kile kitendo kwanza cha kupewa fursa za aina zote zile zinaonyesha kwamba nchi yetu inafuata utawala wa sheria na demokrasia. Wale waliozoea maisha ya *deal deal* wanatakiwa tu waachane na mambo ya *deal deal* na wafuate sheria na wataishi kwa usalama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, hili swali linaonekana lina majibu mengi sana, Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri napenda kuongezea kama Waziri ninayesimamia utawala wa sheria *(rule of law)* nchi hii kwamba kimsingi swali hili halikutakiwa hata kuwemo kwenye *Order Paper* kwa kuwa linakiuka masharti ya Kanuni ya 40 ya Kanuni zetu za Kudumu.

Kanuni ya 40 inasema; "Swali lolote la Bunge halitaruhusiwa kuulizwa Bungeni kama (d), limekusudiwa kupata maoni ya kisheria ya kinadharia au kutoa mapendekezo juu ya jambo la kubahatisha tu."

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ukilisoma hili swali la msingi ni nadharia tupu na hoja zakubahatisha, linasema kumekuwepo na vifo vyenye utata wa kisiasa, vifo vipi hivyo vilivyothibitishwa kitaalamu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kifo kikitokea, vijana wetu wa polisi wakishirikiana na mamlaka nyingine kama Mkurugenzi wa Mashtaka wanatumia muda mrefu kufikiri hiki kifo kimetokana na nini, wanatafuta ile *blameworthy state of mind* au unavyopeleka mahakamani kinachotafutwa ni *malice aforethought* sio tu unakaa kwenye jukwaa unasema hii ni siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, (b) inasema; linatokana na habari za kubahatisha tu, linasema inapotokea mpinzani kupoteza maisha suala halipewi kipaumbele. Ushahidi upo wapi tuletee huo ushahidi hapa sisi kama Serikali tutajibu, lakini sio maswali *generalized,* yanaleta tu hisia mbovu katika jamii ya Watanzania.

(f) inasema linaulizwa kwa njia inayoonyesha jibu lake au kutambulisha mkondo fulani wa maoni na hapa unaona bayana mkondo fulani wa maoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusisitiza tu kwamba Watanzania siasa zisitufikishe huko; kibaka anakamatwa tunaanza kukimbilia kwenda mfukoni ana kitambulisho cha CHADEMA au cha CCM, hatutajenga Taifa hili kwa njia hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri umetoa maelezo marefu kuonyesha kwamba swali hili haliruhusiwi kuulizwa Bungeni, lakini swali lilipitiwa na Kitengo cha Sheria cha Bunge wakajiridhisha, pengine wakati mwingine ni vizuri Serikali pia kabla haijatoa majibu ya yenyewe ijiridhishe.

Kwa kuwa swali limeulizwa hapa Bungeni tutaendelea na utaratibu na kwa sababu sio swali la nyongeza ni swali la msingi, kwa hiyo Serikali ilikuwa na muda wa kuweza kulifuatilia hilo jambo na kuona namna ya kulishauri Bunge. Mheshimiwa Kangi Logola.

**MHE. KANGI. A. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Kwa mujibu wa Ibara ya 14 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kila raia wa nchi hii anayo haki ya kuishi na katika Ibara hiyo haikuainisha haki ya kuishi kwa kutumia vigezo vya itikadi za vyama, wala kigezo cha ukabila, wala kigezo cha udini, wala kigezo cha umri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatoa kauli gani kwa Watanzania na hata Wabunge ambao wamekuwa na tabia ya kuhusisha kila vifo vinavyotokea na masuala ya itikadi za kisiasa ili liwe fundisho kwa wananchi wenye tabia hiyo kwa sababu maswali kama hayo yanaleta uchochezi na yanaweza yakasababisha maafa na hata uhasama wa kudumu kati ya koo ambazo yule mwananchi amekufa? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri na niseme kitu hiki na Watanzania wasikie na wapokee.

Moja, Mtanzania hawi na madaraja kutokana na chama chake, dini yake ama kabila lake. Hakuna nusu Mtanzania kwa sababu ya chama alichonacho na hakuna Mtanzania daraja la pili kutokana na chama alichonacho. Watanzania wote ni Watanzania daraja la juu na wana haki sawa za kuishi na viongozi wanaowagawa Watanzania na kuwatengenezea chuki hata wakadhuriana kwa misingi ya kisiasa wanapaswa kupuuzwa na ndio maana sisi tukiona kiongozi anayefanya vitu vya aina hiyo tunachukua hatua.

Kwa hiyo, wao kwa watanzania maeneo popote pale walipo wasije wakagawanywa kwenye misingi hiyo na niliwahi kuisema eneo moja na ninarudia tena wasije wakaenda kwenye kuuana kwa misingi ya vyama ile hali sisi ambao tunakuwa viongozi huku na wakati mwingine tunawasukuma kufanya hivyo tukija huku wakishatuchagua tunagongesha *glass* za *juice* marazote tunapoonana hapa ili hali wao kule wameshasababisha yatima, wajane na kusababisha matatizo katika familia. Kwa maana hiyo nitoe rai kwa Watanzania na nitoe rai kwa kila mmoja wetu kuhakikisha kwamba tunalinda Utanzania wetu na undugu wetu ambao tumeachiwa na hawa waasisi wetu na ili Taifa letu liweze kupata heshma inayolinda utu. *(Makofi)*

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nilikuwa naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Jeshi la Polisi pamoja na kazi nyingine kazi yake kubwa ni kulinda mali na raia, nilitaka kufahamu kuna ukweli gani kuhusiana na raia kupigwa na polisi huko Pemba? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Niabu Spika, sio kweli kwamba polisi wamekuwa wakipiga raia huko Pemba na ninaomba

nichukue fursa hii mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa mfano halisi ambao ulijitokeza siku za hivi karibuni kule Pemba kwa kitendo cha maigizo na usaniii kilichofanywa na watu kutoka chama cha upinzani cha kisiasa kwa makusudi kabisa ili kupotosha jamii na dunia kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati polisi imefanya kazi yake ya kuwakamata wahalifu ambao wanafanya vitendo vya uhalifu Pemba kuna mhalifu mmoja alijifanya kwamba amekufa na amepigwa na baada ya kuhojiwa na polisi alikimbia na kukamatwa, mtu ambaye amekufa anawezaje kukimbia.

Kwa hiyo, huo ni ushahidi wa usanii ambao unafanywa kwa kulipaka matope jeshi la polisi. Naomba dunia na Watanzania watambue kwamba polisi hata siku moja hawezi kufanya kazi kinyume na sheria, maadili yake na weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kauli hiyo sio kweli kinachofanyika ni kwamba kuna raia ambao wamefanya vurugu za makusudi na polisi inachukua jitihada za kuwakamata na kupeleleza na baadae kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimalizie tukwa kuendelea kutoa wito kwamba tuendelee kuhakikisha kwamba tunalinda amani ya nchi yetu lakini vilevile tusitumie kauli ama vitendo vilivyokuwa sio vya kweli kulipaka matope Jeshi la Polisi na kuipaka matope nchi yetu mbele ya Watanzania na mbele ya Jumuiya za Kimataifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola Mbunge wa Mufindi Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 469

**Vijana Waishio Katika Mistu wa Serikali Mufindi**

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

Jimbo la Mufindi Kusini linazungukwa na msitu wa Serikali na vijana wanaishi humo hawana ajira.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa vibali vya kupasua mbao ili kwa kazi hiyo wajiajiri?

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuwapa vijana hao mtaji ili waanzishe viwanda vidogo vya mbao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mufindi Kusini linapakana na msitu wa shamba la miti la *Sao Hill* ambalo ni miongoni mwa mashamba ya misitu ya kupandwa 18 nchini. Upasuaji wa mbao ni sehemu moja tu ya mchakato mzima wa uvunaji wa mazao ya misitu unaotekelezwa na Wizara yangu kwa mujibu wa mwongozo wa uvunaji endelevu na biashara ya mazao ya misitu yanayovunwa katika mashamba ya miti na misitu ya mikoko kwa mwaka 2014, chini ya Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002 na Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998. Mwongozo huo umeweka vipaumbele mbali mbali katika uvunaji wa mazao ya misitu ikiwemo vikundi vya vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua changamoto za kiuchumi na kijamii kwa vijana katika maeneo husika Serikali imekuwa ikishirikiana na umoja wa vikundi vya kijamii Wilayani Mufindi kwa kuwapatia vibali kwa ajili ya kuwezesha kupata mitaji ili kuwekeza katika miradi mingine ya kiuchumi. Kwa miaka mitatu mfululizo 2013/2014 hadi 2015/2016 vijana kupitia umoja huo wamekuwa wakigawiwa mita za ujazo 200 kila mwaka. Fedha inayotokana na vibali hivi huratibiwa na umoja wao, na imewawezesha kuanzisha shughuli mbalimbali ikiwemo kununua mizinga ya ufugaji nyuki, ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, ufugaji wa kukuna hata mitaji kwa ajili ya biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha uwezeshaji wa vijana wanaoishi jirani na msitu kwa namna endelevu, shamba la miti *Sao Hill* hutoa miche ya miti kwa ajili ya kupanda kwenye mashamba wanayomiliki wenyewe ili waweze kuvuna na kuuza mbao na kujipatia mfanikio ya kiuchumi na kijamii ikiwemo upatikanaji wa ajira. Kwa mfano katika mwaka 2015/2016 shamba lilitoa bure miche 600,000 yenye thamani isiyopungua shilingi 120,000,000 kwa ajili ya kuwawezeshavijana hao.

Aidha, ili kuhakikisha kuwa jamii inanufaika na uwepo wa shamba hilo na kuwapunguzia adha ya michango kwa shughuli za maendeleo vijiji vinavyozunguka shamba hilo vinapatiwa vibali vya kuvuna miti kwa ajili ya shughuli za kimaendeleo ikiwemo kutengeneza madawati, kazi ambayo pia hupewa mafundi ambao ni vijana wanaishi katika vijiji vinayozunguka shamba hilo. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 hadi 2014/2015 jumla ya meta za ujazo 40,000 zilitolewa kwa vijiji vya jirani na kwa mwaka 2013/2014 pekee baadhi ya vijiji vilitumia mgao huo kutengeneza jumla ya madawati 2,469.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatoa ushauri kwa vijana kuungana pamoja na kuunda ushirika ambao utawezesha kupata mikopo kutoka taasisi mbalimbali za fedha na hatimaye kujenga uwezo wa kuendesha shughuli zao za kila siku ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika viwanda vya mbao yaani *saw mills* ili waweze kuomba vibali vya uvunaji kajadiliwa kama wateja wengine wenye viwanda.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuja kule Mufindi hakufika kwenye Jimbo la Mufindi Kusini kuzungumza na wananchi na ukizingatia Jimbo la Mufindi ndilo lililozungukwa na misitu sasa wananchi wanakuuliza, je, utaenda lini ili uweze kuongea na wale wadau wanaozunguka msitu ule? *(Makofi)*

Swali la pili, kuna makundi ya vijana wameshajiunda tayari ambao wazazi wao waliacha maeneo makubwa sana ambayo yalichukuliwa na watu wa Maliasili na vikundi hivyo Igowole kuna vijana 60, Mninga 60, Kihanga 60, Nzigi 60, Mtwango 60, Sawala 60, Kasanga 60, Mabaoni 60, Kitasengwa 60, Kiyowela 60, Nyororo 60, Kibao 60, Mkalala 60, Mbala Maziwa 60, Malangali 60, Mtambula 60, Ihowanza 60, Logolofu 60 na Luhunga 60. Hawa ni vijana waliojiunga kwenye vikundi tayari na ukitokea moto wanakimbia mbio na bodaboda kwenda kuzima moto katika msitu ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa viko vikundi 20 tu na wanaomba kila kikundi kipewe kibali kimoja, Mheshimiwa Naibu Waziri upo tayari mgao huu kuwapatia vibali vyao vijana? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kuhusu ziara ile niliyoifanya na maelezo kwamba baadhi ya maeneo ambayo yanapakana na shamba la *Sao Hill* sikuweza kufika. Kwanza ni kweli kutokana na ratiba niliweza kufika tu kwenye baadhi ya maeneo lakini nataka nimthibitishie kwamba bado umuhimu wa kutembelea kwenye maeneo yaliyobaki uko pale pale. Jitihada za Serikali za kuweza kutekeleza Ilani ya CCM, ya kuhakikisha kwamba Hifadhi za Taifa zikiwemo hifadhi za misitu zinawanufaisha wananchi wanaoishi jiraniau wanaopakana nazo iko pale pale na kwa hiyo, napenda tu nimhakikishie na nimpe ahadi tu kwamba nitafika kwenye maeneo hayo na safari hi sitafanya kikao pale Mufindi Mjini nitakwenda kufanya kikao kule kule mashambani porini niweze kuzungumza na wanavijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu vikundi alivyovitaja na idadi ya vijana ambao wako kwenye vikundi hivyo. Kama nilivyojibu kwenye swali la

msingi, nani vyema tukaenda kwa pamoja na Mheshimiwa Mbunge kwanza nikupe pongezi kwa kuwatetea na kuwazungumzia vijana hao na wananchi kwa ujumla katika maeneo hayo. Lakini vilevile niseme kwamba ni nia ya Serikali sasa kwamba hatutasubiri vijana wasubiri tu kunufaika na uvunaji wa mazao ya misitu kutoka kwenye misitu ya Taifa. Lakini sasa mwelekeo ni kuweza kuwafanya vijana na wenyewe waweze kumiliki mashamba yao ndio maana tunagawa mbegu kama vile ambavyo nimesema kwenye jibu la msingi miche karibu laki sita iligawiwa kwenye matukio ya pale awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendeleza utaratibu wa kuwezesha vikundi hivyo ili baadae viweze kusimama vyenyewe kwa kuwa na mashamba ya kwao ya miti. Nitoe wito na ushauri kwa Halmashauri inayohusika kuweza kuwagawia maeneo vijana hao ili waweze kupata miti, wachukue miche kutoka kwenye Wizara yangu na waweze kupanda katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maombi yake kwamba katika maombi ya mwaka huu kuweza kuzingatia maombi ya vijana wake kwenye eneo lile ninalichukua nitalifikisha kwa wataalam. Lakini litaenda kutazamwa sambamba na maombi mengine ambayo yamekwishapokelewa kwa mujibu wa muongozo ambayo nimeutaja hapo awali.

**MHE. ROSE C. TWEVE**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa asilimia kubwa ya wanawake hapa Tanzania wako kwenye vikundi vya ujasiriamali hususani Mkoa wangu wa Iringa na changamoto kubwa ya hivi vikundi havina miradi endelevu ambayo ingekuwa msaada mkubwa sana kuwasaidia hawa akinamama kuendelea kupambana na hizi changamoto zao wanazopambana nazo kila siku.

Sasa Mheshimiwa Waziri huoni hii ni fursa kubwa pamoja na kazi nzuri ambayo mmewasaidia vijana. Huoni hii ni fursa nzuri sasa kuwasaidia akina mama wote sio tu wale wanaozunguka ule msitu bali akina mama wote wa Mkoa wa Iringa na Wilaya zote, Iringa Mjini, Iringa Vijijini, Kilolo na Mufindi ili waweze kunufaika na msitu huu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubaliana naye kabisa na huo ndiyo mwelekeo wa Serikali kuongeza ajira miongoni mwa vijana, lakini pia kuongeza ajira miongoni mwa akina mama. Sasa misitu ni eneo moja ambalo Serikali inaweza kufikia malengo yake ya kuweza kufanya vijana na akina mama wakaweza kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na mwelekeo wa Serikali nitoe wito kwa Halmashauri zinazohusika katika Mkoa wa Iringa, baada ya akina mama

kuwa wamejiunga katika vikundi basi waweze kupewa maeneo, halafu baada ya pale kwa shughuli zile za kiutaalam na utoaji wa mbegu na pia hata usimamizi wa kutoa utaalam na kuhakikisha kwamba mashamba hayo yanastawi vizuri wataupata kutoka Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuanzia sasa tuwe na mwelekeo wa kuhakikisha kwamba sekta ya misitu ichangie sana kwenye lengo la Serikali kuweza kutoa ajira za kutosha upande wa akina mama na kwa vijana. *(Makofi)*

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Wilaya ya Lushoto ina misitu ya Shume Magamba na mingine midogo midogo na vijana walio wengi Lushoto hawana ajira, je, Serikali haioni sasaimefikia wakati wa kuwapatia vijana hao vibali ili na wao waweze kuwa na ajira? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi na kama nilivyojibu kwenye maswali ya nyongeza yaliyotangulia, ni kweli kwamba, kama Taifa sasa tunakwenda kuhakikisha kwamba tunapunguza kwa kiwango kikubwa na kwa kadri itakavyowezekana jinsi jitihada zinavyozidi kuendelea ni nia ya Serikali ikiwezekana kumaliza kabisa changamoto hii ya ajira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nimesema kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia sekta zilizoko chini ya Wizara hii na sekta ya misitu ikiwa ni mojawapo tunaweza kutoa mchango mkubwa na ndio mwelekeo kwamba tunaenda kutoa mchango mkubwa wa kuweza kutoa ajira kwa ajili ya makundi mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kusubiri vibali kwa ajili ya kuvuna misitu ya Taifa haliwezi peke yake likawa ni suluhisho la ajira katika Taifa, isipokuwa kupitia vibali hivyo vidogo au vichache vikundi vinaweza vikapata mitaji. Lakini kutokana na vyanzo vingine vikundi hivyo baada ya kujiunga viweze kujenga uwezo wa kuwezesha kuweza kupata mikopo kutoka kwenye benki mbalimbali ili waweze kujiunga na kuweza kuanzisha mashamba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mashamba yao wenyewe wataweza kuwa na misitu ambayo itakuwa ni mikubwa, lakini pia wataweza kutokana na biashara ya misitu hata wakaanzisha viwanda vidogo vidogo vya mbao *(saw mills)*. Kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi na baada ya pale ajira itakuwa ni ya uhakika kwa ajili ya wao wenyewe kwenye vikundi lakini pia wanaweza kuajiri hata wengine ambao watakuwa wako jirani nao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hapo tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu. Nitaleta matangazo kwenu tuliyonayo asubuhi hii alafu tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la kwanza ni la wageni waliotufikia Bungeni asubuhi hii, tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika na hawa ni wageni wa Naibu Spika na wanatoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa makofi hayo ninaamini kwamba mnatambua umuhimu wa hilo kundi lililopo hapo juu kabla sijasoma majina yao. Hawa ndiyo watu waliosaidia katika uchaguzi wa mwaka jana mpaka kufikia mahali ambapo sasa tuna Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitawasoma, yupo Mheshimiwa Jaji Mstaafu Damian Lubuva ambaye ni Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi *(NEC)*, yupo pia Mheshimiwa Jaji Mkuu Mstaafu wa Zanzibar Mheshimiwa Hamid Mahmoud Hamid Makamu, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, yupo pia Mheshimiwa Profesa Amon Chaligha ambaye ni Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi, yupo Mheshimiwa Jaji Mstaafu John Mkwawa ambaye ni Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi, yupo Mheshimiwa Mchanga Mjaka ambaye ni Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi, yupo Mheshimiwa Jaji Mstaafu Mary Longway, Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi, yupo pia Mheshimiwa Asina Abdillah Omary ambaye ni Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi, yupo pia Ndugu Kailima Ramadhan ambaye ni Katibu na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Uchaguzi. *(Makofi/Vigelegele)*

Karibuni sana wageni wetu mnaotoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi lakini wageni hawa wameambatana na watumishi wengine katika Tume ambao ni Ndugu Hamidu Mwanga ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Sheria, kuna ndugu Clarence Nanyaro ambaye ni Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Habari, yupo pia Ndugu Athman Masesa ambaye ni Afisa wa Tume. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama mmeona Mheshimiwa Asina Omary amesimama pale nilikuwa nafundisha naye Kitivo cha Sheria ambacho siku hizi kinaitwa Shule Kuu ya Sheria, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Waheshimiwa wabunge na hao ni wageni 13 wa Mheshimiwa *Engineer* Gerson Lwenge ambaye ni Waziri wa Maji na Umwagiliaji na hawa ni kikundi cha wanakwaya kutoka Kanisa la *New Life in Christ* Wilaya ya Wanging'ombe, Kata ya Udonja, Mkoa wa Njombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli ambao ni makada wa Chama cha Mapinduzi kutoka

Lupembe, Mkoa wa Njombe wakiongozwa na ndugu Keneth Swale, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ambao ni familia yake wakiongozwa na ndugu Madam Magreth Luoga ambaye ni dada yake na ndugu Irene Lucas Kunambi ambaye ni mtoto wake, karibuni sana.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia mgeni wa wa Mheshimiwa Goodluck Mlinga ambaye ni msaidizi wake kutoka jimboni kwake na huyu ni ndugu Neema Josia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima ambaye ni rafiki yake na huyu ni Mwalimu Mhoja Kulwa, karibu sana mwalimu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir ambao ni ndugu Shekha M. Salum ambaye ni mke wake, lakini pia ameambatana na mtoto wake ambaye ni ndugu Mohamed H. Ali na ndugu yake ambaye ni Ali Abdallah Ali, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Omary Mgumba ambao ni ndugu Salma Jazzaa ambaye ni Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Morogoro Mjini. Huyu ameambatana na wageni wengine ambao ndugu Mohamed R. Peera ambaye ni Meneja wa Kampuni ya *City Furniture* ya Dar es Salaam. Lakini pia wameongozana na Mohamed H. Mohamed ambaye ni Afisa Masoko wa kampuni ya *City Furniture* ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni sita wa Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani ambao ni watoto wake wakiongozwa na ndugu Mwaisha Salum. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Mhagama ambao ni ndugu Sophia Gama ambaye ni mke wake na ameongozana na ndugu Lusia Njelekela ambaye ni mama mzazi, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 16 wa Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria na hawa wanatoka kanisa la *New Life in Christ* Wilaya ya Kyela, Mkoani Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Selemani Jafo ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI na huyu ni Mwalimu Ayoub Said kutoka Shule ya Sekondari Minaki, Kisarawe karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni kumi wa Mheshimiwa Martin Msuha ambao ni familia yake kutoka Dar es Salaam wakiongozwa na Mwalim Stella Msuha ambaye ni mke wake, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt...., samahani Mheshimiwa Martin Msuha pia anao wageni wengine ambao ni wanafunzi wanne kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu ambao ni Viongozi wa Chama cha Ushirika cha Mwamapuli kutoka Igunga, Mkoa wa Tabora, na hawa ni ndugu Robert Lufunga ambaye ni Mwenyekiti amengozana na ndugu Grace Mfundi ambaye ni Makamu Mwenyekiti na ndugu Asha Mloka ambaye ni mwanachama, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu pia anao wageni wengine ambao ni wanafunzi 114 na walimu watano wa Shule ya Msingi ya Mtakatifu Leo iliyopo Igunga, Mkoa wa Tabora wakiongozwa na *Sister* Paschalina Ombay ambaye ni mlezi wa shule, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 13 wa Mheshimiwa Dotto Biteko ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Jimbo la Bukombe Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi ambao ni ndugu Jackson A. Maleko ambaye ni mdogo wake ndugu Faliee A. Murah ambaye ni mdogo wake, lakini hawa wameongozana na ndugu Agaton J. Lazima ambaye ni mwanafunzi anayesioma Bangarole, India, lakini na ndugu Keith Nabora ambaye ni mwanafunzi anayesoma Bangarluor india, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Suleiman Saddiq ambao ni watumishi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro wakiongozwa na ndugu Lugembe Maiga, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Mheshimiwa Bonnah Kaluwa ambao ni familia yake na nitawataja, anao watoto wake wawili, ndugu Damian Kaluwa na Brian Kaluwa, hawa wameongozana na sioni wamekaa

wapi lakini wameongozana na ndugu Sanje Juma na Rebecca Mdoe, sijui wamekaa wapi, lakini wanakaribishwa sana. *(Makofi)*

Wageni wengine waliotutembelea leo ni wale waliokuja kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 74 na walimu wakuu 18 kutoka shule mbalimbali za Mkoa wa Arusha,karibuni sana wageni kutoka Arusha. *(Makofi)*

Waheshimiwa wabunge, hawa ndio wageni waliotufikia leo lakini yapo matangazo mengine; tangazo la kwanza, ni tangazo la Kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba anawatangazia kwamba siku ya leo tarehe 30 Juni, 2016 mtakutana katika ukumbi wa Msekwa mkubwa. Ukumbi wa Msekwa mtakutana leo mara baada ya kuhairisha shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ambaye anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji kwamba muudhurie kikao baada ya kumalizika kikao cha Bunge leo na hakutaja mahali lakini nadhani mtakutana yale maeneo ya Msekwa mpate chumba cha kuweza kukutania hapo.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, anawatangazia kwamba, leo saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati kwa ajili ya kupitia mambo muhimu ya kazi za Kamati kwa mwaka 2016/2017. Anawatangazia kwamba, kikao hicho kitafanyika katika ukumbi namba 227 mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka, aa..., hili nadhani linarudia tena tangazo la Mheshimiwa Mary Nagu. Lakini kwa sasa limesema muda ni saa saba na watakutana ukumbi mdogo wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu anawatangazia kwamba, Wajumbe wa Kamati hii mtakutana ukumbi wa Msekwa C mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge mchana wa leo.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka Ofisi ya Utawala na wanawatangazia kwamba saa ya mkononi aina ya *coach* imeokotwa jana muda wa saa 11 jioni katika maliwato ya wanaume iliyopo ghorofa ya pili Jengo la Utawala. Aliyepotelewa na saa hiyo afike mapokezo yani *reception* iliyopo *ground floor* Jengo la Utawala ili aweze kupatiwa saa yake.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa na anawatangazia Wajumbe wa kamati hii kwamba watakutana leo saa saba katika ukumbi namba 229 chumba ambacho kipo ghorofa ya pili Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo yalikuwa matangazo yetu kwa leo. Kwahiyo baada ya hayo matangazo tutaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**KAULI ZA MAWAZIRI**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya Jumanne tarehe 21 Juni, 2016 nilikiomba kiti kiniruhusu nitoe maelezo kuhusu kesi ya jinai namba 100 ya mwaka 2016 ya Jamhuri dhidi ya Isaac Habakuk Emily iliyoamuliwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha kufuatia mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Juma Nkamia, Mbunge wa Chemba na kurejewa tena na Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mbunge wa Mtera. Kiti kilielekeza Wizara yangu iandae maelezo kuhusu suala hilo chini ya Kanuni ya 49 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la kesi hii ni kwamba tarehe 17 Machi, 2016, mshtakiwa Isaac Habakuk Emily, mkazi wa Olasite-Arusha, alituma ujumbe katika *account* yake ya *facebook* iliosema:-

*"Hizi siasa za maigizo, halafu mnamfananisha huyu bwege na Nyerere wapi buana".*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuishia hapo akaurusha ujumbe huo kwenye ukurasa wa *facebook* wa mtu aitwaye Ole Mushi ukasambaa lakini ukawakera baadhi ya washiriki katika mitandao hiyo ya kijamii ambao waliitaarifu *TCRA* ichukue hatua stahili kukomesha matamshi ya kejeli yaliyokosa staha na yasiyoendana na sheria, utamaduni na maadili ya nchi yetu. Bila kuchelewa *TCRA* walitoa taarifa Polisi-Kinondoni kutaka uchunguzi ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchunguzi wa Polisi na *TCRA* kukamilika na kuthibitisha tuhuma dhidi yake, mshtakiwa alikamatwa na kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi-Arusha kwa kosa la kumkshifu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa njia ya mtandao. Tarehe 8 Juni, 2016, kesi ilipoanza kusikilizwa, mshtakiwa alikubali mara moja ushahidi wote uliokusanywa dhidi yake na kukiri kosa ambapo Mahakama ikamtia hatiani na kuingia hatua ya kumpa adhabu. Kama ilivyo ada, Mahakama ikataka kujua kama mshtakiwa ni mhalifu mzoefu ndipo Wakili wa Serikali

akaitaarifu Mahakama kuwa mshtakiwa hakuwa na rekodi ya kuhukumiwa huko nyuma. Ikafika zamu ya Wakili wa mshtakiwa kuomba unafuu wa adhabu kwa mteja wake ndipo alipojenga hoja tatu zifuatazo:-

(i) Kosa hilo lilikuwa la kwanza kwa mshtakiwa;

(ii) Mshtakiwa alikiri kosa na kuonyesha ushirikiano mkubwa kwa mamlaka; na

(iii) Mshtakiwa ana umri wa miaka 40 na ana familia inayomtegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na msingi huo, Wakili wa mshtakiwa akaomba mambo mawili yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa sheria inaruhusu adhabu ya kulipa faini au kwenda jela basi mteja wake apewe adhabu ya kulipa faini tu badala ya kwenda jela; na

(ii) Katika kumuadhibu mshtakiwa basi kifungu cha 330(3) cha Sheria ya Uendeshaji Mashtaka *(CPA)* kitumike ili mshtakiwa alipe faini kwa awamu na ndani ya miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakili wa Serikali alipopewa fursa ya kujieleza kuhusu ombi la malipo ya faini kwa awamu hakupinga, akaiachia Mahakama iamue. Ndipo Mahakama ikaamuru mshtakiwa alipe faini ya Sh.7,000,000 kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilipwe hadi tarehe 8 Julai, 2016 na ya pili ifikapo tarehe 8 Agosti, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nisisitize hapa kuwa mfumo wetu wa Kikatiba unaheshimu mgawanyo wa madaraka kati ya mhimili wa utendaji wa utoaji haki na mhimili wa kutunga sharia. Hivyo, maamuzi yaliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha hayawezi kurekebishwa au kusahihishwa hapa ila kwa kukata rufani *(appeal)* au kwa njia ya masahihisho ya Mahakama ya juu zaidi *(revision)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinacholalamikiwa hapa pamoja na masharti ya adhabu yanayoonekana mepesi mno ukilinganisha na uzito wa shauri lenyewe, ni utekelezaji wa hukumu iliyotolewa usioendana na dhana na dhamira ya adhabu. Hoja ya Waheshimiwa Wabunge niliowataja awali ni kwamba mhukumiwa analifanyia siasa suala hili na hivyo kuigeuza adhabu rafiki aliyopewa kuwa burudani ya kisiasa kwenye mitadao ya kijamii naamini kinyume na matarajio ya Mahakamana upande wa Jamhuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejiridhisha na kilichotokea, madhara ya mwelekeo huu mpya katika haki jinai ni kuchochea vitendo zaidi vya ukaidi kwa

mamlaka za nchi na hivyo kujenga msingi wa vurugu. Hili halikubaliki katika utawala wa sheria na mdharau mwiba mguu huota tende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kosa kama hili lilitokea Kenya mwaka jana ambapo mwanafunzi wa chuo kikuu nchini humo, Alan Okengo, umri wa miaka 25 alihukumiwa kifungo cha mwaka mmoja na kulipa faini ya dola 2,000 kwa kumtukana Rais wa Kenya kwenye mitandao ya kijamii. Pamoja na kwamba umri wake ulikuwa mdogo alikuwa hana rekodi ya uhalifu huko nyuma na alikuwa mwanafunzi asiye na kipato kuweza kulipa faini kubwa, dhana na dhamira ya adhabu ilibaki pale pale, mkosaji ajutie kosa lake asije akarudia tena, jamii ijisikie salama zaidi kutokana na funzo alilopata na wengine wasidiriki kujaribu kutenda kosa kama hilo. Dhana na dhamira ya adhabu kama nilivyoelezea vikiondolewa kwenye adhabu ni kukaribisha mizaha ya hatari ambayo hatimaye huwa na gharama hasi na kubwa kwa ustawi na amani ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa awamu ya kwanza ya malipo ya faini inaishia tarehe 8 Julai, 2016 na awamu ya pili ni tarehe 8 Agosti, 2016, nimemuwasilishia Mkurugenzi wa Mashitaka *(DPP)* suala hili kwa hatua stahili ili kulinda dhana na dhamira ya adhabu katika mfumo wetu wa haki jinai kwani matarajio ya kwamba mhukumiwa atajutia kosa lake na wengine wajifunze kutoka kwake hayawezi kufikiwa kwa mwenendo huu wa kuingiza siasa katika utekelezaji wa hukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwakumbusha waendesha mashtaka wote nchini kuwa wawe macho na waweke mbele weledi na maslahi mapana ya Taifa na kamwe wasiyumbishwe na mihemko ya kisiasa katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

### Taarifa ya Awali Kuhusu Tukio la Ujambazi lililotokea Tarehe 28 Juni 2016 huko Rufiji - Mkoani Pwani

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 49(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili mwaka 2013, naomba kuwasilisha taarifa ya awali kuhusu tukio la ujambazi lililotokea tarehe 28 Juni 2016, saa 1.00 jioni huko Rufiji, Mkoani Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 28 Juni 2016 majira ya saa 1:30 jioni katika Kijiji cha Nyamwege, Kata ya Mbwara, Wilaya ya Rufiji, watu wapatao

watatu waliosadikika kuwa majambazi walivamia mabanda na magenge katika kijiji hicho na kupora simu za mkononi ambazo idadi na aina bado haijajulikana na kiasi cha pesa ambacho hakikufahamika mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tukio hilo, watu wawili waliuwawa ambao ni Ndugu Masoud Mayonga wa miaka 33 ambaye ni mfanyabishara wa Tigopesa ambapo alipigwa risasi ya kifuani na kufariki hapo hapo na mtu wa pili ni Ndugu Hamisi Njora, umri wa miaka 28, mfanyabiashara wa genge ambaye alishambuliwa kwa kukatwakatwa mapanga na kufariki dunia akipatiwa matibabu katika hospitali ya Misheni ya Mchukwi. Aidha, Ndugu Juma Said Ayoub wa umri wa miaka 25 mmiliki wa *salon* alijeruhiwa kwa kupigwa risasi ya mguu wa kushoto eneo la pajani wakati anajaribu kupiga kelele kuwaita majirani kutoa msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya Jeshi la Polisi kupata taarifa ya tukio hilo walifika eneo la tukio wakiongozwa na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Rufiji ambapo walikuta wahalifu hao walikuwa wametokomea kusikojulikana. Jeshi la Polisi limetuma Kikosi chake Maalum kutoka Makao Makuu ya Jeshi hilo kushirikiana na Makachero wa Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Rufiji kufanya msako mkali wa kuwakamata wahalifu wote waliohusika na tukio hilo. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Jeshi la Polisi liko imara na litawatia mikononi wahalifu wote waliohusika na tukio hili na kuwafikisha kwenye mkono wa sheria kama ambavyo wamekuwa wakifanya katika matukio mengine ya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai ya Serikali kuwa wananchi wote wanaotegemea uhalifu kuendesha maisha yao waache mara moja kwani Serikali haitafumbia macho uhalifu na wahalifu wa aina yoyote ile. Aidha, nitoe rai kwa Watanzania kushirikiana na Jeshi la Polisi na kutoa taarifa mara moja wanapoona kuna dalili ama kuna watu wanaoonesha wanaweza wakawa na nia mbaya katika maeneo yao ili hatua ziweze kuchukuliwa za kuzuia uhalifu wa aina hiyo kabla haujatokea katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu wa ulinzi na usalama wa nchi Kikatiba ni wa kila mwananchi. Kwa hiyo, naomba kutumia fursa hii kuwaasa Watanzania wote hususani wenye mapenzi mema na usalama wa nchi yetu kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ama vyombo vingine vya ulinzi na usalama pale wanapohisi au kusoma viashiria vya uhalifu katika maeneo yao ili hatua za haraka zichukuliwe kuweza kuzuia uhalifu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza katika kutoa taarifa hii. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa taarifa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Tunaendelea, Katibu.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH - KATIBU MEZANI:-**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kutunga sheria ya kuimarisha mfumo wa utafiti wa kilimo, kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, kuweka utaratibu madhubuti, utawala bora, usimamizi na utekelezaji wa utafiti wa kilimo pamoja na mambo mengine yanayohusiana nayo *(A Bill for an Act to provide for the enhancement of an agriculture research system, establishment of Tanzania Agriculture Research Institute, effective coordination, governance, management and conducting of agricultural research activities and to provide for other related matters)*

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kutunga Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania kuainisha mamlaka na utendaji wa taasisi kuhusiana na uendeshaji wa utafiti wa uvuvi na utafiti wa ukuzaji wa viumbe kwenye maji na kuainisha mambo mengine yanayohusiana na hayo *(A Bill of An Act to establish the Tanzania Fisheries Research Institute and to provide for its powers and operations in relations to their conduct and promotion of research in fisheries and aquaculture and to provide for matters incidental thereto)*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Miswada miwili yaani Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo wa mwaka 2016 *(The Tanzania Agricultural Research Institute Bill, 2016)* na Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa mwaka 2016 *(The Tanzania Fisheries Research Institute Bill 2016)* imeshasomwa kwa Mara ya Kwanza, naagiza kupelekwa kwenye Kamati zinazohusika ili iweze kufanyiwa kazi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea, Katibu.

## HOJA ZA KAMATI

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH - KATIBU MEZANI:-**

Hoja ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

**Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu shauri la Mhe. Joseph O. Mbilinyi Kuhusiana na Kutoa Ishara ya Matusi Bungeni**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE - MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa fasili ya 4(3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu shauri la Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kudaiwa kudharau mamlaka ya Spika kwa kuonesha ishara ya matusi Bungeni kinyume cha kifungu cha 24(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge na Kanuni ya 74 (1)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mamlaka uliyonayo chini ya fasili ya 4 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, mnamo tarehe 13/6/2016 ulilifikisha mbele ya Kamati yangu shauri la Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ambaye alilalamikiwa kutoa ishara ya matusi Bungeni ili Kamati iweze kuchunguza na kutoa mapendekezo kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la malalamiko. Mnamo tarehe 6 Juni, 2016 katika Kikao cha 37, Mkutano wa Tatu, Bunge la Kumi na Moja, Mheshimiwa Jacquline Msongozi, aliomba mwongozo wa Spika kwa kutumia Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika mwongozo huo, Mheshimiwa Jacquline alieleza kuwa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, baada kuwasilisha taarifa ya Kambi hiyo kuhusiana na Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Udhibiti Matumizi ya Dawa na Mbinu za Kuongeza Nguvu Michezoni, akiwa anatoka alionesha kidole chake cha kati cha mkono wa kulia kwa kuelekeza kidole hicho kwa juu akiwa amekunja vidole vingine vilivyobaki ishara ambayo ni matusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo huo uliungwa mkono na Mheshimiwa Sixtus Mapunda, ambaye baada ya kupewa nafasi aombe mwongozo wake alilieleza Bunge kwamba mwongozo wake ni kuhusu jambo hilohilo lililoombewa mwongozo na Mheshimiwa Jacquline Ngonyani Msongozi. Baada ya maombi ya miongozo, Mheshimiwa Spika alilieleza Bunge kuwa, binafsi hakuona kitendo hicho na kwamba atalifuatilia suala hilo na kisha atachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo ulilifikisha suala hili mbele ya Kamati ambapo taratibu za kuanza kusikiliza shauri hili lilianza. Kamati ilikusanya ushahidi na iliwaita mashahidi kwa njia ya hati za wito. Katika hati ya wito ya Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, alitakiwa kufika mbele ya Kamati kujieleza ni kwa

nini asichukuliwe hatua kwa kukiuka kifungu cha 24(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 na Kanuni ya 74 (1)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Vilevile Kamati iliwaita Mheshimiwa Jacquline Msongozi na Mheshimiwa Sixtus Mapunda ambao waliomba mwongozo kuhusiana na kitendo cha Mheshimiwa Joseph Mbilinyi cha kutoa ishara ya matusi ili kutoa ushahidi kwa kile walichokilalamikia kuwa walikishuhudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati. Kwa kuzingatia maudhui ya waraka ulioletwa mbele ya Kamati na chimbuko la shauri hili, Kamati ina jukumu la kuchunguza kwa kujiuliza hoja muhimu tatu zifuatazo:-

(a) Je, ni kweli Mheshimiwa Joseph Mbilinyi alionyesha Bungeni kidole chake cha kati cha mkono wa kulia kwa kukielekeza kwa juu huku vidole vingine vikiwa vimekunjwa?

(b) Kamati ilijiuliza, ikiwa hoja (a) imethibitika, je, kuonesha kidole kwa namna hiyo ni ishara ya matusi jambo ambalo ni kukiuka kifungu cha 24(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge na Kanuni ya 74 ya Kununi za Bunge?

(c) Ikiwa (b) itathibitika ni hatua gani inaweza kuchukuliwa na Bunge kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Bunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya uchambuzi wa kina wa kujibu kikamilifu hoja zilizoainishwa hapo juu, Kamati imefanya rejea katika nyaraka na ushahidi uliotolewa na mashahidi mbele ya Kamati. Nyaraka na ushahidi uliotolewa ni kama ifuatavyo:-

(i) Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296;

(ii) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016;

(iii) Picha ya *video* ya tarehe 6 Juni, 2016; na

(iv) Ushahidi wa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Msongozi na Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo ya Mheshimiwa Jacquline Msongozi alieleza kuwa alimwona kwa macho yake Mheshimiwa Mbilinyi akionesha kidole chake cha kati cha mkono wa kulia kwa uelekeo wa kwenda juu ishara ambayo kwa utamaduni wa kimataifa na wa kijamii ya Kitanzania ni tusi. Aliendelea kueleza kuwa maana yake ni kuingiliwa kinyume cha maumbile

kwa mwanamke au mwanamume hivyo ishara hiyo imemfedhehesha sana akiwa kama ni mwanamke na Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, shahidi mwingine alikuwa ni Mheshimiwa Sixtus Mapunda ambaye alieleza kuwa alimwona Mheshimiwa Mbilinyi akinyoosha kidole chake cha kati ishara ambayo ni tusi. Mheshimiwa Mapunda alifafanua kuwa yeye ni mchezaji wa mpira wa miguu *(football)* ambapo tendo hilo limewahi kusababisha wachezaji wengi kupewa adhabu. Alitoa mfano wa hapa Tanzania kwa mchezaji Juma Nyoso wa *Mbeya City Football Club* aliyemfanyia kitendo hicho mchezaji John Boko wa *Azam Football Club*. Kutokana na kitendo hicho alipewa adhabu. Aidha, alieleza kuwa katika sekta ya michezo ngazi ya kimataifa kuna wachezaji wengi ambao wamewahi kuadhibiwa kutokana na kuonesha ishara hiyo. Alipohojiwa kuhusu maana ya ishara hiyo naye alieleza kuwa ni tusi lenye maana ya kuingiliwa kinyume na maumbile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbilinyi aliitwa na Kamati tarehe 19 Juni 2016 ili kutoa ushahidi wake kuhusu tuhuma zilizomkabili. Katika ushahidi wake aliieleza Kamati kuwa mnamo tarehe 6 aliwasilisha taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Udhibiti wa Matumizi ya Dawa na Mbinu za Kuongeza Nguvu Michezoni. Aliendelea kueleza kuwa wakati anatoka alitoa ishara mbalimbali ikiwa ni *body gestures,* miongoni mwa ishara alizozitoa ni pamoja na kuonesha vidole viwili ambavyo alimuonesha Waziri Mkuu. Wakati anakaribia mlango wa kutoka, alisikia Mbunge wa CCM akimtukana matusi ya nguoni kwa kumtukana mama yake, hivyo inawezekana alinyoosha kidole hicho cha kati huku akikielekeza kwa juu na vidole vilivyobaki vikiwa vimekunjwa. Alieleza kuwa suala hilo lilitokana na hasira baada ya kusikia tusi aililosikia kutoka kwa Mbunge wa CCM ambaye hakumuona akitukana bali alisikia sauti tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbilinyi alipohojiwa na Kamati kuhusu maana ya kunyoosha kidole cha kati kuelekea kwa juu alisema kuwa lugha ya alama huwa haina maelezo ya moja kwa moja. Kwa uelewa wake ishara hiyo siyo tusi bali ni alama ya kupinga jambo lililotokea *(resistance).*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea ushahidi huo, Kamati sasa ilijielekeza katika kujibu hoja iliyoibuliwa na Kamati ambayo inahoji, je, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi alionesha kidole chake cha kati cha mkono wa kulia kwa kukielekeza kwa juu huku vidole vingine vikiwa vimekunjwa? Katika utetezi katika utetezi wake Mheshimiwa Joseph Mbilinyi alikiri kuwa alionyesha kidole kimoja kwa kuwa alikasirishwa na Mbunge wa CCM aliyemtukania mama yake matusi ya nguoni. Sehemu ya ushahidi wake unaeleza kama ifuatavyo, nanukuu kutoka *Hansard*:-

*"Nakumbuka nilinyoosha mkono kwa vidole viwili ambayo ni body reaction, kidole cha kati ni resistance sign… inawezekana nilinyoosha kidole cha kati kwa sababu ya temper..."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno yake Mheshimiwa Joseph Mbilinyi anakiri kunyoosha kidole cha kati cha mkono wa kulia. Aidha, kukiri kwake kunaungwa mkono na ushahidi wa sinema (picha ya *video*) iliyochukuliwa siku hiyo na *studio* ya Bunge ambayo inaonesha dhahiri Mheshimiwa Mbilinyi alinyoosha kidole hicho. Vilevile, ushahidi wa Mheshimiwa Jacqeuline Ngonyani Msongozi na Mheshimiwa Sixtus Mapunda nao ulieleza jambo hilohilo ambalo ushahidi wa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ulifafanua ambapo ni kukiri kufanya kitendo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitafakari kuhusu utetezi wa Mheshimiwa Mbilinyi kuwa alitoa ishara hiyo baada ya kutukanwa na Mbunge wa CCM matusi ya nguoni kwa kumtaja mama yake jambo ambalo si la kimaadili kwa Wabunge. Katika mahojiano Kamati iliibaini kuwa Mheshimiwa Mbilinyi hakuwahi kulalamika popote kuhusiana na matusi aliyoyaeleza. Inafahamika wazi kuwa kutukana ni kosa kwa mujibu wa Kanuni zetu na ni kitendo kisichopaswa kukaliwa kimya. Aidha, alipohojiwa kuhusu jina la Mbunge aliyetoa kauli ya matusi anayemlalamikia hakuweza kutaja na alisema kuwa hakumuona Mbunge aliyemtukana. Kutokana na maelezo hayo, Kamati haikukubaliana na maelezo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ushahidi uliokuwa mbele ya Kamati, Kamati iliridhika kuwa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi alionesha kidole chake cha kati kwa juu huku akiwa amekunja vidole vingine vilivyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujibu hoja (a) sasa tujielekeze katika hoja (b) ambayo ni, je, ishara hiyo ni tusi na hivyo kukiuka masharti ya kifungu cha 24(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge na Kanuni ya 74(1)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu hoja hii, Kamati ilizingatia mazoea na utamaduni wa mataifa mbalimbali na mazoea na utamaduni wa jamii ya Kitanzania kuhusu ishara inayolalamikiwa ya kunyoosha kidole cha kati cha mkono wa kulia kwa kuelekeza juu huku vidole vingine vikiwa vimekunjwa. Kamati ilijiridhisha kuwa jamii hizi zote hutambua kuwa kitendo hicho ni tusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kuonesha kidole cha kati kukielekeza kwa juu huku vidole vingine vikiwa vimekunjwa kinatambuliwa kuwa ni tusi katika ngazi ya Kimataifa. Kwa mfano, mnamo tarehe 28/12/2011 mchezaji Luis Suarez aliyekuwa mchezaji wa timu ya *Liverpool* ya Uingereza alikutwa na hatia na kupewa adhabu ya kufungiwa mchezo mmoja na faini ya

*pound* 20,000 kwa kosa la kuwaonesha kidole cha kati mashabiki wa timu ya *Fulham* ya Uingereza wakati wa mchezo wao uliofanyika tarehe 5 Disemba, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendelea kutafuta jibu la hoja hii, Kamati ilipitia Kitabu kiitwacho *"The Definitive Book of Body Language"* kilichoandikwa na Allan & *Barbara Pease* na kuchapishwa na Kampuni ya Clays ya Uingereza, mwaka 2004, kitabu hicho kinatoa tafsiri ya viungo mbalimbali vya mwili wa binadamu ikiwemo vidole. Ishara hizo zina maana tofauti katika tamaduni mbalimbali. Kitabu hicho kinaeleza kuwa, katika baadhi ya mataifa ishara ya kidole cha kati ina maana zifuatazo:-

(a) Katika utamaduni wa *Ancient Rome* ina maana *"Up yours"*.

(b) Katika utamaduni wa Marekani ina maana *"Sit on this! Screw you!"* Anaendelea kueleza kuwa, *American-middle-finger-raised as a main form of insult.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mwandishi huyu kwa utamaduni wa Marekani, kunyoosha kidole cha kati kuelekea kwa juu ni tusi. Licha ya kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi iliyoiga baadhi ya tamaduni za Kimagharibi tafsiri hiyo haina tofauti na utamaduni wa Kitanzania kwa kuwa hapa Tanzania ishara hiyo pia humaanisha tusi. Hivyo basi, Kamati imeridhika kuwa ishara iliyooneshwa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi Bungeni ni tusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbilinyi alitoa ishara hiyo Bungeni wakati shughuli za Bunge zikiendelea, ni dhahiri kuwa alidharau mamlaka ya Spika aliyekuwa anaongoza shughuli za Bunge za siku hiyo. Hivyo, kwa kitendo chake, Mheshimiwa Mbilinyi amekiuka masharti ya kifungu cha 24(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Haki, na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296 na Kanuni ya 74(1)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge inaeleza ni kwa namna gani mtu atachukuliwa hatua ambaye amedharau mamlaka ya Spika. Kwa urahisi wa rejea nanukuu:

"*Section 24.-Any person shall be guilty of an offence who:-*

*(a) N/A*

*(b) N/A*

*(c) N/A*

*(d) Shows disrespect in speech or manner towards the Speaker, or*

*(e) Commits any other act of intentional disrespect to with reference to the proceedings of the Assembly or of a Committee of the Assembly or to any person presiding at such proceedings.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 74(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaelekeza kuwa:-

*"Spika anaweza kutaja jina la Mbunge kwamba amedharau Mamlaka ya Spika na kisha kupeleka jina hilo kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikiwa:-*

*(a) kwa maneno au vitendo, Mbunge huyo anaonesha dharau kwa mamlaka ya Spika; au*
*(b) Mbunge huyo atafanya kitendo chochote cha makusudi cha kudharau Shughuli ya Bunge au Mbunge yeyote anayeongoza shughuli hiyo."*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria na Kanuni tajwa zinaeleza bayana kuwa Mbunge atakuwa anadharau mamlaka ya Spika kwa kufanya kitendo cha makusudi cha kudharau mamlaka hiyo. Katika shauri hili Mheshimiwa Mbilinyi alinyoosha kidole cha kati katika Ukumbi wa Bunge, ishara ambayo ni matusi hivyo alikiuka Sheria na Kanuni hizo za Bunge. Kwa mazingira hayo, Kamati inamtia hatiani Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kwa kukiuka kifungu cha 24(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge pamoja na Kanuni ya 74 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu hoja kuwa ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa dhidi ya Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Kamati ilijikita katika masharti yaliyopo katika Kanuni ya 74(3). Kanuni hiyo inatoa adhabu kwa Mbunge yeyote anayedharau mamlaka ya Spika. Kanuni hiyo inaeleza kama ifuatavyo nanukuu:-

*"Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itajadili suala hilo na ikithibitika kuwa Mbunge husika ametenda kosa inaweza kushauri kwamba:-*

*(a) ikiwa ni kosa lake la kwanza Mbunge huyo asihudhurie vikao vya Bunge visivyozidi kumi; au*
*(b) ikiwa ni kosa lake la pili au zaidi Mbunge huyo asihudhurie vikao vya Bunge visivyozidi ishirini.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza kuwa Wabunge wote waendelee kuheshimu sheria na kanuni tulizojiwekea wenyewe. Itakumbukwa kuwa Mheshimiwa Mbilinyi alidai kuwa alitukanwa ndani ya Bunge ndipo alichukua hatua ya kufanya kosa hili. Endapo Mbunge anayedaiwa kuwa alimtukana Mheshimiwa Joseph Mbilinyi angebainika na akaletwa kwenye Kamati yangu, angechukuliwa hatua kali kwa uvunjifu huo wa Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, Bunge ni chombo cha umma

kinachotazamwa na Watanzania wote pamoja na Jumuiya ya Kimataifa, hivyo, matendo yanayofanywa na Wabunge wakiwa ndani ya Bunge yanatazamwa na sehemu kubwa ya Watanzania. Kamati inawatanabahisha wabunge wote kuzingatia maadili ya jamii ya Tanzania. Wabunge wanapokuwa Bungeni wajiepushe na matendo yasiyofaa ili Bunge letu liwe mfano wa kuigwa katika jamii ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Napenda nitumie nafasi hii tena kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali, kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi unakuwa ndio kipaumbele cha kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kunusuru muda pengine nisiyasome hayo majina, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kuchambua na kutoa haki katika Bunge hili. Aidha, napenda kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashilillah kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kipekee nawashukuru Ndugu Pius Mboya, Kaimu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria na Ndugu Prudence Rweyongeza, Naibu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Sehemu ya Huduma ya Sheria kwa ushauri wa kisheria walioutoa katika kuisaidia Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Ndugu Matamus Fungo na Ndugu Maria Mdulugu, Makatibu wa Kamati; Ndugu Lweli Lupondo na Ndugu Editruda Kilapilo kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ni matarajio yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge wataipokea kwa kauli moja na wataikubali hoja iliyopo mbele yetu ya matokeo ya taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ya uchunguzi wa kitendo cha Mheshimiwa Mbilinyi kudharau Mamlaka ya Spika ili kuimarisha nidhamu ndani ya Bunge letu Tukufu na kuhakikisha kuwa Kanuni za Bunge zinaheshimiwa na kuzingatiwa na Wabunge wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge liazimie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio la Bunge kuhusu adhabu kwa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi aliyedharau Mamlaka ya Spika katika Kikao cha Thelathini na Saba cha Mkutano wa Tatu wa Bunge tarehe 6 Juni, 2016. Azimio hili linatolewa chini ya Kanuni ya *74(3)(a).*

KWA KUWA, Mheshimiwa Spika alipeleka malalamiko dhidi ya Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, kudharau mamlaka ya Spika kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge;

NA KWAKUWA, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa tarehe19 Juni, 2016 na kufanya uchunguzi wa shauri hili ulioiwezesha Kamati kubaini kuwa Mheshimiwa Mbilinyi amekiuka masharti ya kifungu cha 24(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296 na Kanuni ya 74(1)(a) na (b) kwa kuonesha kidole cha kati cha mkono wake wa kulia akielekeza kwa juu huku vidole vingine akiwa amevikunja ishara ambayo ni matusi;

NA KWAKUWA, kitendo hicho kimelifedhehesha Bunge, Wabunge wote na jamii ya Watanzania wote kwa ujumla, kitendo hicho kimefanywa na Mbunge mzoefu wa Bunge letu Tukufu;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kuwa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, asimamishwe na asihudhurie vikao kumi vya Bunge la Kumi na Moja kuanzia kikao cha leo tarehe 30 Juni 2016 ambapo Azimio hili linatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge imeungwa mkono. Kwa mujibu wa Kanuni zetu hoja hii ingeweza kujadiliwa lakini kwa namna nilivyoona makofi yalivyo mengi ni kama Wabunge wote wamekubaliana na maazimio ya Mheshimiwa Mwenyekiti. Mheshimiwa Mwenyekiti kwa makofi hayo basi hata wewe hutakuwa na hoja ya kuja kuhitimisha hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Kamati imetoa taarifa yake lakini pia imeleta Maazimio na Wabunge hapa wameunga mkono hoja hiyo. Kwa maana hiyo Bunge hili linamuadhibu Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kusimamishwa na kutohudhuria vikao kumi vya Bunge la Kumi na Moja kuanzia kikao cha leo tarehe 30 mpaka hapo ambapo hiyo adhabu itakuwa imekamilika. Kwa hiyo, nawahoji sasa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda kwa hiyo, adhabu ya Mheshimiwa Mbilinyi inasimama ya kutokuhudhuria vikao kumi vya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninayo miongozo kadhaa hapa kabla hatujaendelea lakini pia yako maamuzi mbalimbali ambayo nitapaswa kuyafanya. Nitaanza na miongozo iliyokuwa imeombwa na Waheshimiwa Wabunge katika vipindi mbalimbali vya vikao vya Bunge hili.

**Majibu ya Mwongozo wa Mheshimiwa Hussein N. Amar kuhusu majibu ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Vipimo vya Mazao ya Kilimo**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar aliomba mwongozo kuhusu majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu vipimo vya mazao ya kilimo.

Waheshimiwa Wabunge, katika kikao cha Hamsini na Tatu cha Mkutano wa Tatu wa Bunge kilichofanyika tarehe 29 Juni 2016, Mheshimiwa John Peter Kadutu kwa niaba ya Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya aliuliza swali la msingi Na.454 kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambalo pamoja na mambo mengine swali hilo lilihusu wafanyabiashara wa mazao ya kilimo kufanya udanganyifu kwa kuzidisha ujazo wa magunia yaani lumbesa na kutanua madebe. Mheshimiwa Mbunge aliuliza ni kwa nini Serikali inashindwa kuweka matumizi ya mizani rasmi kwa mazao hapa nchini. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji alijibu swali hilo la msingi. Baada ya majibu ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa John Kadutu aliuliza maswali mawili ya nyongeza na swali la pili aliuliza kama ifuatavyo:-

*"Swali la pili, kwa vile suala la vipimo vya kienyeji, kama lumbesa na ndiyo maarufu kama msumbiji limekuwa likilalamikiwa kwa muda mrefu, je, Serikali inaonaje, iweze kutoa tamko ni lini hasa Wakala wa Vipimo na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaanzisha hivyo vituo?"*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri alijibu swali hilo kama ifuatavyo:-

*"Mhesheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, vipimo aina ya lumbesa, msumbiji na wengine wanaita badimanyaira, Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI, wameshatoa maelekezo na mtakuta hata njiani, mimi napokea simu nyingi, watu wengi wanakamatwa. Uuzaji wa mazao unakuwa na vituo maalum na Maafisa Ugavi na Watendaji wa Kata, ni moja ya jukumu lao kufika maeneo yale na mnunuzi yeyote hakikisha unapima kilo zisizidi 100. Nitafanya jitihada za zaidi kuhakikisha kwamba tunawapelekea mizani kadri tutakapopata uwezo wa kuweza kununua mizani hiyo ili kusudi wananchi pamoja na kupima usawa wa gunia lakini wawe na uhakika kwamba ni kilo 100 tu, wasiwanyonye wauzaji".*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kipindi cha maswali na majibu nilipokea mwongozo wa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar chini ya Kanuni ya 68

fasili ya (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu majibu hayo ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na mambo mengine Mheshimiwa Hussein Amar aliuliza kuwa nanukuu:-

*"Mheshimiwa Waziri ameelekeza kwamba lumbesa ni kilo 100 kwa gunia lakini Halmashauri yangu ya Nyang'hwale Wakala wa Vipimo wanawalazimisha wasafirishaji wa mpunga na mahindi kwamba gunia liwe na kilo 75 tu… ninaomba mwongozo wako, Serikali na Halmashauri tuchukue kauli ipi kilo 75 za Halmashauri ama kilo 100 ambazo amezitamka Mheshimiwa Waziri wa Viwanda".*

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu mwongozo huo nilisema kuwa nitahitaji muda ili nifuatilie jambo hilo na kulitolea mwongozo lakini pia nilimtaka Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji aniletee taarifa kuhusu suala hilo ili niweze kuutoa mwongozo wangu kwa usahihi. Nimefuatilia suala hili la vipimo vya mazao ya kilimo na sheria inayosimamia ujazo na nimejiridhisha kwamba taratibu za namna ya kufungasha bidhaa mbalimbali zimeainishwa kwenye Jedwali la Kumi na Moja la Sheria ya Vipimo, Sura ya 340. Sheria hiyo inaeleza kuwa endapo itaonekana mazao husika hayapo kwenye Jedwali la Kumi na Moja la sheria hiyo, mazao hayo yafungashwe ujazo usiozidi kilo 100.

Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji akitoa maelezo yake alifafanua kuwa, wanunuzi wahakikishe kwamba ujazo wa mazao usizidi kilo 100. Vilevile, Mheshimiwa Waziri alieleza kwamba, katika Halmashauri wapo Maafisa mahsusi wanaosimamia suala la vipimo. Naamini maafisa hao wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria ya Vipimo niliyoitaja. Ni rai yangu kwamba, wanaosimamia jukumu hilo la vipimo wazingatie sheria zilizopo na wananchi wanatakiwa wawaamini wataalamu hao na kuheshimu maelekezo wanayopewa.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndio mwongozo wangu kuhusu suala hilo. *(Makofi)*

**Majibu ya Mwongozo wa Mheshimiwa Kangi A. N. Lugola kuhusu kutojibiwa kikamilifu kwa swali lake la nyongeza aliloliuliza kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niliombwa pia mwongozo na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola kuhusu kutojibiwa kikamilifu kwa swali lake la nyongeza aliloliuliza kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Waheshimiwa Wabunge, katika kikao cha Hamsini na Tatu cha Mkutano wa Tatu wa Bunge kilichofanyika tarehe 29 Juni 2016, baada ya kipindi cha

maswali na majibu, Mheshimiwa Kangi Lugola aliomba mwongozo wa Spika, chini ya Kanuni ya 68(7) kwamba swali lake la nyongeza aliloliuliza kwenye swali la msingi namba 452 halikujibiwa badala yake Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alitoa majibu kwa swali ambalo hakuuliza.

Mheshimiwa Kangi Lugola, alieleza kama ifuatavyo:-

*"Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu swali langu kwa kulipua kwa sababu sikuuliza Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya polisi ila niliuliza ni lini Jimbo la Mwibara litapewa hadhi ya Wilaya ya Kipolisi. Kwa hiyo, naomba mwongozo wako kama ni sahihi Mheshimiwa Naibu Waziri kunipa majibu ya swali ambalo mimi sikumuuliza."*

Waheshimiwa Wabunge, ili niweze kutoa mwongozo wangu na kufafanua jambo aliloliombea mwongozo Mheshimiwa Kangi Lugola kama linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge nilisema kuwa nitapitia Taarifa Rasmi za Bunge nione jinsi swali lilivyoulizwa na majibu yaliyotolewa ili nitoe mwongozo wa Spika. Baada ya kuzingatia Taarifa Rasmi za Bunge, Mheshimiwa Kangi Lugola aliuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

*"Kwa kuwa, Jimbo la Mwibara ambalo kwa muda mrefu kulingana na jiografia yake matukio kwenye visiwa ya ujambazi, tulishaomba kuwa na Wilaya ya Kipolisi. Je, Serikali mpaka sasa ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi na kutupa hadhi ya Wilaya ya Kipolisi?"*

Waheshimiwa Wabunge, majibu ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi yalikuwa kama ifuatavyo:-

*"Mheshimiwa Naibu Spika, upo mpango wa kujenga vituo vya Polisi nchi nzima, ambapo kimsingi tuna upungufu mkubwa wa vituo vya Polisi vinavyokadiriwa kuwa zaidi ya 4,500 nchi nzima ikiwemo eneo ambalo Mbunge amelizungumza"*.

Waheshimiwa Wabunge, swali la nyongeza alilouliza Mheshimiwa Kangi Lugola kama nilivyonukuu lina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ya swali alitaka kujua Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo cha polisi katika Jimbo la Mwibara na sehemu ya pili inahusu Serikali kulifanya Jimbo la Mwibara kuwa Wilaya ya Kipolisi. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi katika majibu yake alijikita katika sehemu ya kwanza ya swali kuhusu kujenga kituo cha polisi, ndiyo maana alieleza kuwa Serikali ina mpango wa kujenga vituo vya polisi zaidi ya 4,500 nchi nzima ikiwemo Jimbo la Mwibara la Mheshimiwa Kangi Lugola. Sehemu ya pili kuhusu Jimbo hilo kufanywa Wilaya ya Kipolisi halikujibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, niliombwa mwongozo wa Spika na Mheshimiwa Kangi Lugola kama jambo hilo linaruhusiwa au kama ni sahihi kikanuni. Mwongozo ni kama ifuatavyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 44(2) swali la nyongeza linatakiwa kuwa moja tu, kanuni tajwa inafafanua kama ifuatavyo:-

*"Mbunge anayeuliza swali la msingi ataruhusiwa kuuliza maswali ya nyongeza yasiyozidi mawili na Mbunge mwingine yeyote atakayepewa nafasi ataruhusiwa kuuliza swali moja tu la nyongeza."*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Kangi Lugola lilikuwa na sehemu mbili ambapo kimsingi kila sehemu ilikuwa ni swali linalojitegemea, hivyo ilikuwa ni sahihi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kujibu sehemu moja tu ya swali. Hii ni kwa kuwa kama nilivyoeleza Kanuni tajwa hairuhusu Mbunge kuuliza swali la nyongeza zaidi ya moja.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndio mwongozo wangu. *(Makofi)*

**Uamuzi wa Spika kuhusu shauri la Mhe. Dkt. Hussein A. Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Dhidi ya Mhe. Saed Ahmed Kubenea Aliyelalamikiwa Kusema Maneno Yasiyokuwa na Ukweli Bungeni**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, pia ninao uamuzi hapa kuhusu shauri la Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambalo alikuwa akimlalamikia Mheshimiwa Saed Kubenea kusema uongo Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 10 Mei 2016 katika Kikao cha Kumi na Sita cha Mkutano wa Tatu, Mheshimiwa Saed Kubenea wakati alipokuwa anachangia bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, alitoa tuhuma dhidi ya Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Mheshimiwa Mwinyi kuwa jeshi hilo limeingia mkataba wa ujenzi wa nyumba za makazi ya Wanajeshi na kampuni ya *Henan Guiji Industry Company Limited* lenye ekari 26,082.87 katika *Plot* Na.1255, Masaki Dar es Salaam na kwamba kampuni hiyo itaendesha mradi kwa miaka 40 na baada ya hapo eneo hilo litarudishwa jeshini. Aidha, Mheshimiwa Kubenea alieleza kuwa katika mkataba huo inaelezwa kuwa Mheshimiwa Mwinyi atajengewa nyumba yake binafsi katika kiwanja namba 2455/6 eneo la Upanga Dar es Salaam.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na mchango huo wa Mheshimiwa Kubenea uliotoa tuhuma dhidi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Mwinyi mwenyewe, Mheshimiwa Dkt. Mwinyi aliwasilisha barua ya malalamiko kwa Spika akitaka Kiti cha Spika, kumtaka Mheshimiwa Kubenea

kuthibitisha tuhuma hizo na endapo atashindwa achukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, kufuatia malalamiko yaliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, siku ya tarehe 13 Mei, 2016 nilitoa mwongozo wa Spika Bungeni kwa kumtaka Mheshimiwa Saed Kubenea kufuta sehemu ya mchango wake iliyolalamikiwa kukiuka Kanuni ya 63(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Sehemu ya mwongozo niliyoutoa ilisomeka kama ifuatavyo:-

*"Mheshimiwa Kubenea, sasa ninakupa nafasi ya kufuta kauli yako ama kama hautafuta nitaeleza nini kitafuata karibu, Mheshimiwa Kubenea."*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumpa fursa ya kufuta sehemu ya mchango wake iliyokiuka Kanuni, Mheshimiwa Kubenea alikataa kufuta usemi wake kwa kujibu kama ifuatavyo:-

*"Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa kuwa Hansard ninayo na kwa kuwa hoja niliyojenga ninaamini kwamba kwa kunisukuma hivyo hautakuwa unanitendea haki, siwezi kufuta kauli.*

*Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana"*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Mheshimiwa Kubenea kukataa kufuta kauli yake Bungeni, nilimtaka kuthibitisha maneno aliyoyasema Bungeni kwa maandishi ndani ya siku nne tokea tarehe nilipomtaka kufanya hivyo. Baada ya kuletewa uthibitisho na Mheshimiwa Kubenea kwa mamlaka niliyonayo niliwasilisha uthibitisho huo katika Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili ifanye uchunguzi kwa niaba yangu chini ya Kanuni ya 5(1) na Kanuni ya 72(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambapo Kanuni ya 5(1) inaeleza:-

*"Katika kutekeleza majukumu yake yaliyotajwa katika Ibara ya 84 ya Katiba, Spika ataongozwa na Kanuni hizi na pale ambapo Kanuni hazikutoa mwongozo, basi Spika atafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge pamoja na mila na desturi za Mabunge mengine yenye utaratibu wa Kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania".*

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 72(1) inasema:-

*"Spika atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa utaratibu bora unafuatwa Bungeni, na uamuzi wa Spika kuhusu jambo lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho".*

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikutana ikachunguza suala hili pamoja na kuwahoji Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi na Mheshimiwa Saed Kubenea. Baada ya uchunguzi wake, Kamati imethibitisha kwamba Mheshimiwa Saed Kubenea alisema uongo Bungeni kinyume na Kanuni ya 63(1) na Kanuni ya 64(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwani alishindwa kuthibitisha kama Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ameingia mkataba na kampuni ya Henan *Guiji Industry Company Ltd* kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi ya Wanajeshi pamoja na nyumba ya Mheshimiwa Dkt. Mwinyi mwenyewe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na Mheshimiwa Saed Kubenea kushindwa kuthibitisha maneno aliyoyasema Bungeni na kwa mamlaka niliyonayo chini ya Kanuni ya 63(8), namsimamisha Mheshimiwa Saed Kubenea kuhudhuria vikao vitano vya Bunge kuanzia tarehe ya leo. Pamoja na maelezo hayo, naagiza taarifa yote ya Kamati iingizwe katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa, nikitoa adhabu chini ya Kanuni ya 68(8) nilipaswa kuwapa fursa ya kujadili kama mnaona adhabu hiyo ni ndogo ambayo Mheshimiwa Spika ametoa lakini kwa mujibu wa Kanuni ya 68(9) inatutaka ikiwa tunataka kutumia Kanuni hiyo kufanya mjadala ni lazima mtuhumiwa apewe nafasi ya kujitetea lakini baadaye akishapewa hiyo adhabu aweze kuomba adhabu ipunguzwe. Sasa kwa sababu Mheshimiwa hayupo hapa Waheshimiwa Wabunge nawashawishi tusiingie kwenye Kanuni ya 68(9) mkubaliane na mimi kwenye hiyo adhabu niliyoitoa kwa mujibu ya Kanuni ya 68(8). *(Makofi)*

## TAARIFAYA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE KUHUSU MALALAMIKO YA MHE. HUSSEIN ALI MWINYI (MB) WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA DHIDI YA MHE. SAED AHMED KUBENEA (MB) ALIYELALAMIKIWA KUSEMA MANENO YASIYOKUWA NA UKWELI BUNGENI

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 63 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 imeweka masharti kuhusu utaratibu wa kufuatwa katika nyakati ambapo Mbunge anapokuwa amedaiwa kusema uongo Bungeni. Kwa mujibu wa Kanuni hiyo, suala la kusema uongo Bungeni ni suala linalosimamiwa na Mheshimiwa Spika mwenyewe. Hata hivyo, kwa kuzingatia kuwa Mkutano wa Tatu wa Bunge ulikuwa mahsusi kwa ajili ya vikao vya bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Bungeni, Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 5 na Kanuni ya 72 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambaye ndiye mwenye Mamlaka ya kuhakikisha kuwa utaratibu bora unafuatwa Bungeni, aliagiza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ichunguze malalamiko

yaliyotolewa na Mheshimiwa Hussein Mwinyi (Mb) dhidi ya Mheshimiwa Saed Kubenea kwa niaba yake na kutoa mapendekezo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mujibu wa Kanuni ya 4(3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea kudaiwa kusema Uongo Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**,mnamo tarehe 17 Mei, 2016, uliwasilisha Malalamiko ya Mheshimiwa Hussein Ali Mwinyi (Mb) aliyemlalamikia Mhe. Saed Kubenea (Mb) kukiuka Kanuni ya 63(1) na 64(1)(a) kwa kusema uongo Bungeni wakati alipokuwa akichangia kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## 2.0 CHIMBUKO LA SHAURI LA MALALAMIKO MHE. HUSSEIN MWINYI (MB), WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA DHIDI YA MHE. SAED KUBENEA (MB) KUDAIWA KUSEMA UONGO BUNGENI

**Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Hussein Mwinyi (Mb), Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika malalamiko yake kupitia barua yenye Kumb. Namba AB 98/239/1 ya tarehe 12 Mei, 2016 aliwasilisha malalamiko kwamba tarehe siku ya tarehe 10 Mei, 2016 Katika kikao cha Kumi na Sita cha Mkutano wa Tatu, Mhe. Saed Kubenea (Mb) alipokuwa akichangia kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, alitoa tuhuma nzito dhidi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuwa limeingia Mkataba na Kampuni ya Henan Guiji Industry Investment Co. Ltd ili kutoa ekari za Mraba elfu ishirini na sita sifuri themanini na mbili nukta nane saba(26,082.87) eneo la Plot Namba 1255 Masaki Dar es Salam kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Makazi ya Wanajeshi na kwamba katika mkataba huo, Kampuni tajwa itaendesha mradi kwa miaka 40 na baada ya hapo, eneo litarudi jeshini. Aidha, Mhe. Mwinyi alieleza kuwa, Mhe. Kubenea alisema katika Mkataba huo, yeye atajengewa nyumba binafsi katika Plot Na. 2435/5 eneo la Upanga Dar es salaam, jambo ambalo mhe. Mwinyi analikanusha.

**Mheshimiwa Spika,** Katika barua yake, Mhe. Mwinyi anamtaka Mhe. Kubenea athibitishe na akishindwa achukuliwe hatua stahiki.

**Mheshimiwa Spika**, Wakati Mhe. Mwinyi alipokuwa akifanya majumuisho kuhusu Bajeti ya Wizara yake kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 hata kabla ya kuwasilisha malalamiko yake rasmi kwa Spika alitaka Kiti cha Spika kumtaka Mhe. Kubenea kuthibitisha maneno aliyoyatoa Bungeni kuhusuana na kile alichodai Mkataba ulioingiwa kati ya Jeshi na Wananchi na Kampuni ya Henan Guiji Industry Co.Ltd ukiwa ni Mkataba wa kwanza na Mkataba kati ya

Meshimiwa Hussein Mwinyi Kampuni ya Henan Guiji Industry Co.Ltd ukiwa ni Mkataba wa pili.

**Mheshimiwa Spika,** siku ya tarehe 13 Mei, 2016 Mhe. Naibu Spika alitoa Mwongozo wake wa kumtaka Mhe Kubenea kufuta kauli hiyo ama kuthibitisha. Mhe. Kubenea alikataa kufuta Kauli hivyo alitakiwa kuwasilisha uthibitishio wake ndani ya muda aliokuwa ametakiwa kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelekezo hayo taratibu za kuanza kusikiliza shauri hili zimeanza ikiwa ni pamoja na kukusanya ushahidi dhidi ya mashahidi na kuwaita mashahidi kupitia hati za wito. Katika hati za wito waheshimiwa wote wanatakiwa kufika mbele ya Kamati kujibu kwa nini wasichukuliwe hatua kwa kukiuka Kanuni ya 63 (1) na 64 (1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

## 3.0 HOJA ZA MSINGI (ISSUES)

**3.1 Mheshimiwa Spika,** katika Waraka wa Spika wa kuleta shauri kwa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ulirejea Fasili ya 4(1) (a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Kwa urahisi wa rejea nanukuu Kanuni hiyo:

*4(1) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itatekeleza majukumu yafatayo:-*

*(a) Kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya haki,kinga na madaraka ya Bunge yatakayopelekwa na Spika*;

*(b) Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya wabunge yatakayopelekwa na Spika*

## 4.0 UCHAMBUZI WA KAMATI KUHUSU SHAURI LA KUDAIWA KUSEMA UONGO BUNGENI DHIDI YA JESHI LA WANANCHI WA TANZANIA NA MHESHIMIWA HUSSEIN MWINYI.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu waraka ulioletwa mbele ya Kamati na kwa kuzingatia maudhui yaliyo katika malalamiko ya Mbunge aliyelalamika, Kamati ina jukumu la kuchunguza kwa kujiuliza hoja mbili muhimu,ambazo ni:-

(a) Iwapo Mheshimiwa Saed Kubenea alisema uongo au kutoa taarifa ambazo hazina ukweli kinyume na Kanuni ya 63(1) na 64(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge,Toleo la Januari, 2016 au la!.

(b) Ikiwa hoja (a) itathibitika, ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa na Bunge kwa Mujibu wa Kanuni za Bunge.

**4.1 Mheshimiwa Spika,** katika kufanya uchambuzi wa kina na kujibu kikamilifu kuhusu suala hili, Sekretarieti imefanya rejea ya nyaraka zifuatazo;

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016
(ii) Kumbukumbu Rasmi za Bunge za tarehe 10 na 13 Mei, 2016.

**4.2 Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Hussein Mwinyi alifika Mbele ya Kamati na kueleza kuwa siku ya tarehe 10, Mei, 2016 Mheshimiwa Kubenea alisema Uongo kwa kulituhumu Jeshi la Wananchi kuwa limeingia Mkataba wa Ujenzi wa Nyumba za Makazi ya Askari wa Jeshi la Wananchi na Kampuni ya kichina inayoitwa *Henan Guiji Industry Co.Ltd* na kwamba katika Mkataba huo Jeshi litatoa ekari za Mraba elfu ishirini na sita sifuri themanini na mbili nukta nane saba (26,082.87) eneo la Plot Namba 1255 Masaki, Dar es Salaam kwa ajili ya Ujenzi wa nyumba za Makazi, Kampuni tajwa itaendesha mradi kwa miaka 40 na baada ya hapo eneo litarudi jeshini.

**4.3 Mheshimiwa Spika**, Aidha, Mhe. Mwinyi alieleza Kamati kuwa, Mhe. Kubenea alisema katika Mkataba huo, Mhe. Hussein Mwinyi atajengewa nyumba binafsi katika Plot Na. 2435/5 eneo la Upanga Dar es Salaam, jambo ambalo Mhe. Mwinyi analikanusha.

**4.4 Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Mwinyi alieleza kuwa yeye kama Waziri Mwenye dhamana na Wizara hiyo hana taarifa zozote juu ya uwepo wa Mkataba huo na kwamba hata Kampuni inayotajwa na Mheshimiwa Kubenea aliisikia kwa mara ya kwanza Bungeni. Mheshimiwa Mwinyi aliendelea kuieleza Kamati kuwa kisheria yeye huwa hasaini mikataba yoyote kati ya Jeshi na taasisi nyingine yoyote bali kama Jeshi linakuwa inataka kuingia Mkataba wowote linaomba Power of Attorney kutoka kwake ndipo linaingia Mkataba. Mheshimiwa Mwinyi aliendelea kueleza kuwa, Jeshi haliwezi kuingia Mkataba wowote bila kupata idhibi yake na kwamba hadi muda alipokuwa anatoa utetezi wake mbele ya Kamati, Jeshi lilikuwa halijaomba kibali kwake cha kuingia Mkataba na Kampuni yoyote.

**4.5 Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Mwinyi alieleza kuwa Jeshi kama taasisi nyingine yoyote liko huru kuingia mikataba na kwamba kwa sasa lipo kwenye mchakato wa uboreshaji wa Makazi ya Askari wake na kwamba linataka kushirikisha Sekta Binafsi katika utaratibu wa PPP na kwamba katika kukamilisha kazi hiyo kupitia utaratibu huo, yapo makampuni mengi ya kichina yaliyoomba kushirikiana na Jeshi katika suala la ujenzi wa nyumba za Askari na kwamba hakumbuki kama Kampuni iliyotajwa na Mhe. Kubenea ni miongoni mwa Kampuni zilizoomba kushirikiana na Jeshi la Wananchi**.**

**4.6 Mheshimiwa Spika,** aidha Mheshimiwa Mwinyi alikiri kumiliki kiwanja Na. 2435/5 kilichopo Upanga Dar es salaam, hata hivyo aliieleza Kamati kuwa yeye hajaingia Mkataba na Kampuni yoyote wa kuendeleza kiwanja hicho na kwamba yeye haishi katika nyumba hiyo inayotajwa na Mheshimiwa Kubenea.

Mheshimiwa Kubenea alifika Mbele ya Kamati siku ya tarehe 16 Juni 2016 akiambatana na Mawakili wake ambao ni Mhe. James Millya (Mb) na Wakili mwingine wa kujitegemea**.**

4.7 **Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Kubenea aliomba kuwasilisha nyaraka mbalimbali ambazo alisema ndizo zilikuwa uthibitisho wake kuhusiana na kile alichokisema Bungeni. Nyaraka hizo ni hizi zifuatazo;

(a) Utetezi aliouwasilisha kwa Spika;

(b) Kumbukumbu Rasmi za Bunge za tarehe 10 Mei, 2016, na tarehe 13 Mei, 2016;

(c) Rasimu ya Mkataba Kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Kampuni ya *Henan Guiji Industry Co. Ltd;*

(d) Rasimu ya Mkataba Kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Mhe. Hussein Mwinyi;

(e) Barua ya uthibitisho wa Umiliki wa kiwanja Na. 2435/5 kilichopo Upanga Dar es Salaam pamoja na risiti halisi za malipo ya kufanya uhakiki wa kiwanja tajwa; na

(f) Ramani ya Kiwanja Na.1255;

4.8 **Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Kubenea alieleza kuwa katika maelezo yake Bungeni hakukusudia kulidhalilisha Jeshi la Wananchi wa Tanzania wala Mheshimiwa Hussein Mwinyi na kwamba katika mchango wake hakusema Jeshi limeingia Mkataba bali alisema inawezekana Jeshi limeingia au linataka kuingia na kwamba alikua anafanya hivyo kwa nia njema ya kutoa tahadhari kwa Jeshi la Wananchi kujiepusha kuingia Mkataba mbovu.

4.9 **Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Kubenea aliendelea kueleza kuwa wakati alipokuwa akichangia hakuna Mbunge mwingine yeyote aliyesimama kuomba kuhusu utaratibu kama Kanuni ya 63(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili kumtaka kufuta au kuthibitisha kauli aliyoitoa na kwamba kama hilo lingetokea Bungeni, angeliweza kufuta Kauli yake.

4.10 **Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Kubenea aliendelea kuieleza Kamati kuwa asilimia kubwa ya Wabunge hawaongei ukweli kwa asilimia miamoja kwa hiyo ni kweli kwamba hakuwa na uhakika na taarifa alizozitoa bali alikuwa anatimiza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kama anavyotakiwa kwa Mujibu wa Katiba**.**

4.11 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 63 (1) na 64(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Mbunge yeyote haruhusiwi kutoa taarifa au kusema uongo Bungeni na zinamtaka mbunge kusema au kutoa taarifa ambazo ana uhakika nazo. Kwa urahisi wa rejea nanukuu Kanuni hizo kama ifuatayo;-

"*63(1) Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo, Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au la kubahatisha tu"*

*"64(1)(a)Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-*
*(b) Hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli"*

4.12 **Mheshimiwa Spika**, katika kujibu hoja (a) ambayo Kamati imeiibua, ni vema kuchambua ushahidi wa Mheshimiwa Kubenea, kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Kubenea alipokuwa akichangia Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, alitoa tuhuma nzito dhidi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuwa limeingia Mkataba na Kampuni ya Henan Guijo Industry Investment Co. Ltd

**Mheshimiwa Spika**, katika maelezo ya kuthibitisha kuhusu tuhuma hizo kama alivyotakiwa kufanya alieleza kuwa utaratibu uliowekwa na Kanuni ya 63 haukufutwa. Kanuni ya 63 (3) inaelekeza kuwa ikiwa mbunge yeyote ataona kuwa Kanuni itakiukwa atasimama mahali pake na kusema "kuhusu utaratibu" akiruhusiwa atataja kanuni iliyovunjwa. Anaendelea kusema kuwa wakati anaongea hadi kumaliza hakuna Mbunge au Waziri aliyefanya hivyo. Aidha anaeleza kuwa hakuna kanuni inayoelekeza kupeleka Shauri kwa Spika ikiwa Mbunge ameshindwa kutumia Kanuni ya 63.

4.13 **Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya maelezo ya Mhe. Kubenea anasema:-

"*Kuna taarifa kuwa Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania limeingia Mkataba na Kampuni ya Henan Guijo Industry Investment Co. Ltd. Katika mkataba huu Jeshi litatoa ekari za Mraba elfu ishirini na sita sifuri themanini na mbili nukta nane saba (26,082.87) eneo la Plot Namba 1255 Masaki Dar es Salaam kwa ajili ya Ujenzi wa nyumba za Makazi na Kwamba Katika Mkataba huo, Kampuni tajwa itaendesha mradi kwa miaka 40 na baada ya hapo eneo litarudi jeshini.*

*Mhe. Waziri, ninaomba atueleze kama mkataba huo umesainiwa na kama haujasainiwa, nitaliomba Bunge hili Tukufu lielekeze kwamba mkataba huu ambao unaweza kuwa ukawa wa kinyonyaji upelekwe katika Kamati ya Ulinzi na Usalama ili uweze kupitiwa……………………….kibaya zaidi kwamba Kampuni ya Henan Guiji Industry Co.Ltd ambayo imeingia mkataba na Jeshi la Wananchi, inajifunga mkataba mwingine na waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Dkt.Mwinyi……. katika Mkataba huo, Kampuni hiyo itajenga Nyumba Mhe.Dkt Hussein Mwinyi katika Plot Na. 2435/5 eneo la Upanga Dar es salaam na Kampuni hiyo ndiyo itakayolipia gharama za ujenzi"*

4.14 **Mheshimiwa Spika,** Kwa maelezo ya Mhe**.** Kubenea ni dhahiri kuwa aliongea kitu ambacho hana uhakika nacho na maelezo yake ni ya kubahatisha kwani maneno ambayo ametumia kuwa "kuna taarifa kuwa…." mkataba umesaniwa au haujasainiwa". Aidha, kile alichokiwasilisha mbele ya Kamati ni Rasimu za Mikataba na sio Mikataba kwani haijasainiwa na pande husika. Kwa mujibu wa Sheria ya Ushahidi, uthibithisho wa Nyaraka unapaswa kuwa nakala halisi na zilizotoka katika chanzo cha kuaminika. Ili uweze kujua chanzo cha Mkataba au Wahusika pande zinazohusika.

4.15 **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa amewasilisha rasimu za Mikataba, Kamati haikuweza kuzingatia rasimu hizo kwa kuwa hazijulikani chanzo chake hivyo haiwezi kuamini katika kitu ambacho haijulikani chanzo chake**.** Kwa kuwa masharti ya Kanuni ya 63(1) na 64(1)(a) inamtaka mbunge aongelee kitu ambacho anaamini kuwa ni cha kweli, na kwa kuwa Mheshimiwa Kubenea hakuwa na uhakika na jambo alilokuwa analizungumza, Kamati imeridhika kwamba Mheshimiwa Kubenea alisema uongo Bungeni, hivyo inamtia hatiani.

4.16 **Mheshimiwa Spika,** sasa tujielekeze katika hoja ya pili ambayo ni (b) inayosema ikiwa hoja (a) itathibitika, ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa na Bunge kwa Mujibu wa Kanuni za Bunge.

Katika Kanuni ya 63(8) inaeleza kuwa mbunge aliyetakiwa kutoa uthibitsho kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge au atakataa kujirekebisha kwa kufuta kauli au usemi wake Spika atamwadhibu kwa kumsimamisha Mbunge huyo asihudhurie vikao vya Bunge visivyozidi vitano.

**Mheshimiwa Spika**, Masharti ya Kanuni ya 63(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge yanatoa adhabu ya siku tano kwa Mbunge aliyesema uongo Bungeni. Kwa kuwa Kanuni hiyo haitoi adhabu nyingine yoyote zaidi ya kumsimamisha Mbunge kutohudhuria vikao vya Bunge vitano, Kamati inapendekeza Mheshimiwa Kubenea kusimamishwa kutohudhuria vikao vya Bunge vitano mfululizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepima athari ambazo Jeshi la Wananchi wa Tanzania lililojijengea heshima kubwa ya kuwa miongoni mwa Majeshi yenye Nidhamu kubwa duniani na linalofanya kazi nzuri ya kulinda mipaja ya Nchi yetu pamoja na kushiriki katika misheni za kulinda Amani sehemu mbalimbali duniani, kitendo cha kulihusisha Jeshi letu katika kuingia mikataba yenye utata na yenye harufu ya rushwa ni kulidhalilisha Jeshi letu na kulishushia heshima mbele ya jamii. Aidha, , Kamati imezingatia kuwa uongo uliosemwa na Mhe.Kubenea unatishia na kuathiri usalama wa nchi nchi yetu. Kwa kuzingatia mazingira hayo, Kamati inashauri Bunge lijadili na kutoa adhabu kwa namna litakavyoona inafaa kwa kuwa Kamati imefungwa na Kanuni 63(8) kuhusu adhabu kwa Mbunge anayesema uongo Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha

**Kapt. (Mst) George Mkuchika (Mb)**
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE.**
**22 Juni, 2016**

**Uamuzi wa Spika kuhusu shauri la Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Dhidi ya Mhe. James Kinyasi Millya Aliyelalamikiwa Kusema Uongo Bungeni**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, pia upo uamuzi wa Spika kuhusu shauri la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kumlalamikia Mheshimiwa James Kinyasi Millya kuwa alisema uongo Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya tarehe 24 Mei, 2016 katika kikao cha Ishirini na Saba, Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, nilitoa mwongozo wangu kuhusu ombi la mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama chini ya Kanuni ya 68(7) pamoja na Kanuni ya 64(1)(a) na Kanuni ya 63(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Mwongozo huo uliombwa kutokana na madai ya Mheshimiwa James Kinyasi Millya kumhusisha Mheshimiwa Jenista Mhagama kuwa ni shemeji wa mmoja wa wabia wa Kampuni ya *Sky Associates* aliyodai ilinunua mgodi wa *Tanzanite One* na kwamba ilikuwa ikinyanyasa wananchi. Mheshimiwa Mhagama alieleza kuwa Mheshimiwa Millya alisema uongo na kwamba huyo mtu aliyemtaja siyo shemeji yake na aliomba Bunge limtake Mheshimiwa Millya kuthibitisha madai yake.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuombwa mwongozo huo kufuatia maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mhagama kuhusu ukweli wa jambo lililodaiwa na Mheshimiwa Millya kama ambavyo Kanuni ya 63(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inavyoeleza na kwa kuzingatia Kanuni hiyo nilimtaka Mheshimiwa James Kinyasi Millya afute kauli yake dhidi ya Mheshimiwa Jenista Mhagama au kama ana ushahidi wa kuthibitisha kauli yake autoe kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge. Licha ya Mheshimiwa Millya kupewa fursa ya kufuta kauli yake kutokana na Mheshimiwa Mhagama kulalamika kwamba hayakuwa na ukweli, yeye alikataa kufuta kauli hiyo. Nilimtaka Mheshimiwa Millya kuwasilisha uthibitisho wa maandishi kwa Spika ndani ya siku nne kuanzia tarehe ya uamuzi uliotolewa tarehe 24 Mei 2016. Baada ya Mheshimiwa Millya kuwasilisha ushahidi wake kuhusu madai yake kwa mamlaka niliyonayo niliwasilisha uthibitisho huo katika Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili ifanye uchunguzi kwa niaba yangu chini ya Kanuni ya 5(1) na Kanuni ya 72(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni ya 5(1) na kanuni ya 72(1) sitairudia kuisoma kwa sababu nimeshaisoma kwenye uamuzi uliopita. Hivyo basi, nilielekeza suala hili kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili ilifanyie uchunguzi jambo hili na kuleta mapendekezo kwa mujibu wa Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikutana ikachunguza suala hili pamoja na kuwahoji Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa James Millya. Baada ya uchunguzi wake, Kamati imethibitisha kwamba Mheshimiwa James Millya alisema uongo Bungeni kinyume na Kanuni ya 63(1) na Kanuni ya 64(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwani alishindwa kuthibitisha kama Mheshimiwa Mhagama ana undugu na Ndugu Martin Mhagama aliyedai ni shemeji yake. Kutokana na Mheshimiwa James Millya kushindwa kuthibitisha maneno aliyoyasema Bungeni na kwa mamlaka niliyonayo, chini ya Kanuni ya 63(8) namsimamisha Mheshimiwa James Kinyasi Millya kuhudhuria vikao vitano vya Bunge kuanzia tarehe ya leo. Pamoja na maelezo hayo, naagiza taarifa yote ya Kamati iingizwe katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, maelezo niliyoyatoa wakati nikitoa uamuzi katika suala la Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi na Mheshimiwa Said Kubenea yanatumika pia katika shauri hili kwa maana ya kwamba nawashawishi Wabunge tusiingie kwenye Kanuni ya 63(9) kwa sababu Mheshimiwa Millya hayuko hapa ili tuweze kumpa fursa ya kujitetea. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE KUHUSU MALALAMIKO YA MHE. JENISTA JOAKIM MHAGAMA (MB) WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU DHIDI YA MHE. JAMES KINYASI MILLYA (MB) ALIYELALAMIKIWA KUSEMA UONGO BUNGENI

### 1.0 UTANGULIZI:

**1.1 Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 63 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 imeweka masharti kuhusu utaratibu wa kufuatwa katika nyakati ambapo Mbunge anapokuwa amedaiwa kusema uongo Bungeni. Kwa mujibu wa Kanuni hiyo,suala la kusema uongo Bungeni ni suala linalosimamiwa na Mheshimiwa Spika mwenyewe. Hata hivyo,kwa kuzingatia kuwa Mkutano wa Tatu wa Bunge ulikuwa mahsusi kwa ajili ya vikao vya bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Bungeni, Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 5 na Kanuni ya 72 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambaye ndiye mwenye Mamlaka ya kuhakikisha kuwa utaratibu bora unafuatwa Bungeni, aliagiza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ichunguze malalamiko yaliyotolewa na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu dhidi ya Mheshimiwa James Kinyasi Millya kwa niaba yake na kutoa mapendekezo.

**1.2 Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 4(3) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu shauri la Mhe. James Kinyasi Millya (Mb) kudaiwa kusema uongo Bungeni.

**1.3 Mheshimiwa Spika,** kwa Mamlaka uliyonayo chini ya Fasili ya 4 ya nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliwasilisha malalamiko ya Mhe. Jenista Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu aliyemlalamikia Mhe. James Millya (Mb) kwa kukiuka Kanuni ya 63(1) na 64(1)(a) kwa kusema uongo Bungeni wakati alipokuwa anachangia katika mjadala wa hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

### 2.0 CHIMBUKO LA SHAURI LA MALALAMIKO YA MHE. JENISTA MHAGAMA (MB) DHIDI YA MHE. JAMES MILLYA (MB) KUDAIWA KUSEMA UONGO BUNGENI.

2.1 **Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 20 Mei, 2016 wakati Mhe. James Millya (Mb) alipokuwa akichangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini pamoja na mambo mengine alimtaja Mhe. Jenista Mhagama (Mb) kuwa shemeji wa mmoja wa mbia wa Kampuni ya Sky Associate inayodaiwa kuwanyanyasa wananch huko Mererani Mkoani Arusha. Mhe. Milya alimtaja

mbia huyo kuwa ni Gonga ambaye ameolewa na Martin Mhagama au Yusuph Mhagama.

2.2 **Mheshimiwa Spika**, kufuatia kutajwa huko, Mhe. Jenista Mhagama (Mb), aliomba Mwongozo wa Spika kwa kutumia Kanuni ya 68(7) na Kanuni ya 63(1) na 64(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la januari, 2016. Katika mwongozo wake Mhe. Jenista Mhagama Mb) alieleza kuwa Mhe. Millya (Mb) alisema uongo kwa kuwa huyo mtu aliyemtaja sio shemeji yake, hivyo aliomba Mhe. Naibu Spika amtake Mhe. Millya kufuta au kuthibitisha madai yake kwa ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, alilieleza Bunge kuwa mwongozo huo angeutoa kwa wakati mwafaka.

2.3 **Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 24 mei, 2016, Mhe. Naibu Spika alitoa mwongozo huo na kumtaka Mhe. Milya kufuta kauli yake au kuthibitisha. Mhe. Millya alisema angethibitisha ndipo Naibu Spika alimpa siku nne (4) ili kuthibitisha kauli yake kwa kupeleka uthibitisho huo kwa Mhe. Spika kwa maandishi.

2.4 **Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 27 mei, 2016 Mhe. Millya aliwasilisha uthibitisho wake kwa Mhe. Spika kwa maandishi kama alivyoelekezwa.

2.5 **Mheshimiwa spika**, baada ya Mhe. Milya kuwasilisha utetezi wake, ndipo uliwasilisha shauri hilo katika Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili kuchunguza na kutoa mapendekezo kwa mujibu wa Kanuni.

2.6 **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelekezo yako, Kamati ilianza taratibu za kusikiliza shauri hilo, ikiwa ni pamoja na kukusanya ushahidi na kuwaita mashahidi kwa hati za wito. Katika hati ya wito ya Mhe. James Millya (Mb), alitakiwa kufika mbele ya Kamati kueleza ni kwa nini asichukuliwe hatua kwa kukiuka Kanuni ya 63(1) na 64(1)(a) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

2.7 **Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilimwita Mhe. Jenista Mhagama (Mb), ili kuja kufafanua malalamiko yake dhidi ya Mhe. Milya (Mb).

## 3.0 UCHAMBUZI WA KAMATI KUHUSU MALALAMIKO YA MHE. JENISTA MHAGAMA (MB) DHIDI YA MHE. JAMES MILLYA (MB)

3.1 **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia maudhui ya chimbuko na malalamiko katika shauri hili, Kamati ina jukumu la kuchunguza kwa kujiuliza hoja zifuatazo:-

(a) Iwapo Mhe. James Millya (Mb) alisema uongo au kutoa taarifa ambazo hazina ukweli kinyume na kanuni ya 63(1) na 64(1)(a) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

(b) Ikiwa hoja (a) itathibitika, ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa na Bunge kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

3.2 **Mheshimiwa Spika,** katika kufanya uchambuzi wa kina na kujibu kikamilifu hoja zilizoibuliwa na Kamati kuhusu suala hili, Kamati ilifanya rejea katika nyaraka na ushahidi uliotolewa kama ifuatavyo:-

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

(ii) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

(iii) Kumbukumbu rasmi za Bunge za tarehe 20 Mei, 2016 na tarehe 24 Mei, 2016.

3.3 **Mheshimiwa Spika,** Mhe. Jenista Mhagama (Mb) alifika mbele ya Kamati siku ya tarehe 7, Juni 2016 ili kutoa ufafanuzi wa malalamiko yake dhidi ya Mhe. Millya (Mb). Mhe. Jenista (Mb) aliieleza Kamati kuwa Mhe. Millya alisema uongo alipomtuhumu kuwa ni shemeji wa mmoja wa mbia wa Kampuni ya *Sky Associate* inayomiliki mgodi wa *Tanzanite One* unaodaiwa kunyanyasa wananchi.

3.4 **Mheshimiwa Spika**, Mhe. Mhagama (Mb) alieleza kuwa mtu aliyetajwa kwa jina la Martin Mhagama, au Yusuph Mhagama, hamfahamu wala katika ukoo wao ambako ameolewa wenye jina la Mhagama hakuna mtu wa namna hiyo. Aliendelea kueleza kuwa hata hiyo Kampuni anayoitaja ya Sky Associate haifahamu.

3.5 **Mheshimiwa Spika,** Mhe. James Millya (Mb) alifikika mbele ya Kamati siku ya tarehe 16 juni, 2016 ambapo aliomba kuongezewa muda wa kujiandaa kwa kuwa alichelewa kupata hati ya wito na pia kuomba kuleta mashahidi wanne ambao alidai walimwandikia ujumbe mfupi kwa njia ya simu kuhusiana na alichokisema Bungeni.

3.6 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitafakari kuhusu maombi ya Mhe. Millya na kuridhia ombi la kumuongezea muda wa kujiandaa na ilimuarifu afike tena mbele ya Kamati tarehe 19 juni, 2016. Kamati baada ya kupitia Sheria na Kanuni za Bunge ilikataa ombi la Mheshimiwa Millya la kuleta mashahidi wake.

3.7 **Mheshimiwa Spika**, msingi wa kukataa ombi la Mhe. Millya ni kifungu cha 13 na 14 cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge Sura ya 296, ambavyo vinatoa mamlaka kwa Kamati kuita mtu yeyote kufika mbele ya Kamati na kutoa ushahidi kwa kadri itakavyoona inafaa. Sheria hii inatoa hiari *(desertion)* kwa Kamati kuita shahidi baada ya kupima umuhimu wa ushahidi wa shahidi anayetakiwa kuitwa mbele ya Kamati. Katika kukataa ombi la Mhe. Millya kuleta mashahidi, Kamati lizingatia kuwa shauri lililokuwa mbele yake lilikuwa linamhusu yeye kudaiwa kusema uongo Bungeni jambo ambalo kwa maoni ya Kamati mashahidi walikuwa hawahitajiki.

3.8 **Mheshimiwa Spika,** Mhe. James Millya alifika tena mbele ya Kamati mnamo tarehe 19 Juni, 2016, ambapo kabla ya kusikiliza utetezi wake Kamati ilimtaarifu juu ya uamuzi wake kuhusu ombi lake la kuita mashahidi wane aliodai walimtumia ujumbe kuhusiana na alichokisema Bunge. Katika taarifa hiyo Katika taarifa hiyo Kamati ilimueleza juwa imekataa ombi lake kwakuwa kwa mujibu wa Kanuni anayetakiwa kuthibitisha ni yeye.

**Mheshimiwa Spika,** katika utetezi wake kwa kuegemea katika utetezi wake uliowasilishwa kwa Spika tarehe 27 Mei, 2016. Katika maelezo yake Mhe. Millya (Mb) alieleza kuwa alichokisema Bungeni alinukuu ujumbe mfupi aliotumiwa na mmoja wa wafanyakazi waliosimamishwa na Kampuni ya Sky Associate. Aidha aliendelea kueleza kuwa Mhe. Jenista Mhagama (mb) alikiri kuwa ukoo wa akina Mhagama ni mkubwa hivyo, inawezekana ni huyu aliyemtaja inawezekana ni shemeji yake lakini hamfahamu kutokana na ukubwa huo wa ukoo wa Mhagama.

3.9 **Mheshmiwa Spika,** Mhe. Millya (Mb) aliendelea kueleza kuwa maneno aliyoyatoa Bungeni hayakuwa kwa nia mbaya ndiyo maana alitumia maneno "bahati mbaya mama yetu Mhagama naye anatajwa humu ….". Vilevile alieleza kuwa alichokisema amenukuu kutoka katika ujumbe huo wa simu.

3.10 **Mheshimiwa Spika,** Mhe. Millya alipohojiwa na Kamati kama anawafahamu Martin Mhagama na Asia Gonga ambaye alidai ni shemeji wa Mhe. Jenista Mhagama (Mb) na kama alikwishawahi kuongea nao na kumthibitishia kuhusu uhusiano wao na Mhe. Waziri, Mhe. Millya aliieleza Kamati kuwa hawafahamu na wala hajawahi kuongea nao bali, aliongea na mtoto wao aitwae Yusuph Mhagama. Alifafanua kuwa uhakika wa uhusiano kati ya Waziri na Mbia huyo ameupata kutoka kwa wafanyakazi wa Sky Associate waliofukuzwa kazi ambao mara nyingi humpa taarifa za ukweli na alikuwa anatimiza wajibu wake kama mwakilishi wa wananchi kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 63(2).

3.11 **Mheshimiwa Spika**, katika kuufanyia kazi ushahidi uliowasilishwa mbele ya Kamati ni vema kunukuu sehemu ya mchango wa Mhe. James Millya (Mb) uliolamikiwa na Mhe. Jenista Mhagama (Mb), kwa mujibu wa kumbukumbu rasmi za Bunge, maelezo hayo ni :-

*"Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine Mheshimiwa Profesa, Madini yanaibiwa kila siku na kampuni hii na bahati mbaya mimi nimeahidi mara nyingi nitakuwa mkweli mpaka nitakapokufa. Wanapata wapi kiburi cha kuwafukuza wafanyakazi 201 halafu wamewafukuza baada ya kuwafukuza wanawapeleka Mahakamani hawajawalipa mafao. Na Sheria za kazi zinajulikana* ***bahati mbaya mama yetu Mhagama naye anatajwa humu ndani kwamba ni shemeji wa mmoja wa mbia hapo. Dada anaitwa Asia Gonga ameolewa na Martin Mhagama au Yusuph Mhagama, sasa sijui."***

3.12 **Mheshimiwa Spika,** katika nukuu hiyo pamoja na utetezi wa Mhe. Millya ni dhahiri kuwa, Mhe. Millya aliongea maneno au kauli Bungeni ambazo aliambiwa na watu anaodai kuwa ni wafanyakazi waliofukuzwa na Kampuni ya Sky Associate. Kwa maneno mengine Mhe. Millya hakuwahi kufanya utafiti wa kutosha ili kujiridhisha kuwa taarifa alizopewa zina ukweli kwa kiasi gani kabla hajazitoa Bungeni na katika umma wa watanzania.

3.13 **Mheshimiwa Spika**, Hii inadhihirika pale Mhe. Millya alipoomba kuwaita watu wanne waliomtumia ujumbe mfupi kuhusu tuhuma dhidi yake.

3.14 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni zetu zimeweka wazi ni kauli au maneno yapi yanapaswa kusemwa ndani ya Bunge kama chombo cha Umma. Kanuni ya 63(1) inamtaka Mbunge anaposema Bungeni kuzungumzia jambo ambalo yeye mwenyewe analiamini na ana uhakika nalo. Kanuni hiyo inaeleza:-

"63(1)Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 100 ya katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika bunge, ni marufuku, kabisa kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo, **Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni anawajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au la kubahatisha tu"**

3.15 **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni hii inaweka masharti kwa Mbunge mwenyewe anayezungumza ndani ya Bunge kuwa na uhakika wa jambo analolisema kwa maana ya kulifanyia utafiti na siyo kuegemea kwenye maelezo ya mtu mwingine ambaye hakuzungumza Bungeni bila kulifanyia utafiti ili kujiridhisha na ukweli wa jambo hilo.

3.16 **Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo ndio maana Kanuni zetu hazikusema kuwa Mbunge hatahesabiwa kuwa anasema uongo ikiwa maneno anayoyasema aliambiwa na mtu mwingine ambaye ataweza kuthibitisha kuhusu suala hilo. Kanuni zinamtaka Mbunge kutoa kauli ambazo amezifanyia utafiti na kuwa na uhakika nazo na anauwezo wa kuzithibitisha popote pale na wakati wowote.

3.17 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni zetu hazitoi Kinga kwa Mbunge anayerejea au kusema maneno aliyoambiwa na mtu mwingine, bali Kanuni ya 63(2) zinatoa kinga kwa mbunge anafanya rejea katika suala lililoandikwa au kutangazwa na vyombo vya habari. Kanuniya 63(2) inaeleza:-

***"63(2) Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni hatachukuliwa kuwa amesema uongo iwapo anafanya rejea ya habari kuhusu jambo fulani lililotangazwa au lililoandikwa na vyombo vya habari."***

3.18 **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Sheria ya ushahidi *(The endence Act,)* ushahidi wa kuambiwa haukubaliki. Sheria hiyo inataka ushahidi unaotolewa uwe ni wa moja kwa moja kutoka mtu anayefahamu suala hilo. Hayo yameelezwa katika kifungu kwa cha 62 cha Sheria ya ushahidi. *(The evidence Act)*.

3.19 **Mheshimiwa Spika,** katika Mahakama zetu, ilikwishawekwa wazi kuwa ushahidi wa kuambiwa haukubaliki.

3.20 **Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huo wa ushahidi Sheria na Kanuni, Kamati imejiridhisha kuwa Mhe. Millya alisema uongo Bungeni hivyo, inamtia hatiani kwa kuvunja Kanuni ya 63(1) na 64(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

3.21 **Mheshimiwa Spika,** baada ya kujibu hoja (a) sasa tujielekeze katika hoja kwamba hatua gani za kuchukua. Kanuni ya 63(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inaeleza wazi kuwa Mbunge anayekiuka Kanuni ya 63 atapewa nafasi ya kujirekebisha, akishindwa kufanya hivyo atasimamishwa asihudhurie vikao visivyozidi vitano. Kanuni hiyo inaeleza nanukuu:

*"63(8) Endapo hadi kufikia mwisho wa muda aliopewa Mbunge aliyetakiwa kutoa uthibitisho wa ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake aliyoyatoa Bungeni atakataa au atashindwa kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge na kama atakataa kujirekebisha kwa kufuta kauli au usemi au maelezo yake, basi Spika atamwadhibu kwa kumsimamisha Mbunge huyo asihudhurie vikao vya Bunge visivyozidi vitano ."*

3.21 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kuzingatia athari za uongo uliosemwa Bungeni na Mhe. Millya, Kamati imejiridhisha kuwa uongo huo ni upotoshaji wa jamii na kumchafulia jina Mhe. Jenista Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu.

Hivyo basi, Kamati inapendekeza Mhe. Millya asimamishwe asihudhurie vikao vitano (5) vya Bunge kuanzia siku ya kusomwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Capt (Mst) George H. Mkuchika
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE**
23 Juni, 2016

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tutaendelea na ratiba yetu, Katibu.

**NDG. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:**-

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**NAIBU SPIKA:** Katibu wa Bunge.

**NDG. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 29(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli kwa ajili ya kufanyiwa kazi katika Mkutano wa Tatu wa Bunge zimemalizika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa taarifa hiyo Katibu wa Bunge, Katibu.

**NDG. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:-**

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema kwa kutupatia afya njema ya kutufikisha siku ya leo tunapohitimisha Mkutano wa Tatu wa Bunge lako Tukufu tuliouanza tarehe 19 Aprili, 2016 takribani siku 73 zilizopita. Mkutano huu ulikuwa mahsusi kwa ajili ya kujadili na kupitisha bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Tano pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kazi hiyo tumeifanya kwa tija na kwa ufanisi wa hali ya juu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, naomba nitumie fursa hii ya awali kumpongeza Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kujadili na hatimaye kupitisha bajeti ya Serikali ya makadario ya mapato na matumizi kwa Wizara, Mikoa na Taasisi za Serikali. Aidha, nawapongeza pia kwa kupitisha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa miaka miwili. Napenda kukiri kwamba mijadala ya mkutano huu ilikuwa yenye msisimko na wakati mwingine iliambatana na hisia kali kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Ninaamini hisia za Waheshimiwa Wabunge waliochangia zilikuwa na hoja ambazo zililenga kujenga na kuiletea maendeleo nchi yetu, asanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wabunge kwa ushauri mzuri kwa Serikali ambao tutaufanyia kazi. Aidha, michango yenu Waheshimiwa Wabunge ni chachu katika kuongeza kasi ya kuwawezesha wananchi kupata maendeleo ya haraka hasa wakati huu tunapoanza utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi katika Serikali ya Awamu ya Tano. Tunawashukuru sana kwa michango yenu yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Serikali tuliyoipitisha kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni ya kihistoria, kwa sababu kwa mara ya kwanza, tangu tupate uhuru wetu mwaka 1961, tumeweza kutenga asilimia 40 ya bajeti ya shilingi trilioni 29.5 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Changamoto kubwa na ya jumla tuliyonayo ni jinsi ya kupanua wigo wa kukusanya kodi, kudhibiti matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na kutumia kwa ufanisi fedha zinazokusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa kila shilingi ya Serikali inayokusanywa kupitia kodi za wananchi, mikopo na michango ya Wahisani inatumika katika shughuli iliyokusudiwa na ni lazima thamani ya fedha *(value for money)* ionekane bayana katika utekelezaji wa vipaumbele tulivyojiwekea. Vipaumbele vyetu tulivyokubaliana katika mpango wa mwaka huu, ni pamoja na kutenga fedha nyingi zaidi katika Sekta za Elimu, Afya, Maji, Kilimo, Viwanda, Miundombinu, Uchukuzi, Bandari, Usafiri wa Anga na Majini, Maliasili, Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitimisha Mkutano huu tukiwa tumepata fursa ya kujadili Miswada, Maazimio na Kauli mbalimbali za Mawaziri. Miswada iliyowasilishwa na Serikali ni saba, ambapo Miswada minne ilisomwa kwa Mara ya Kwanza na ifuatayo pia imepitishwa.

Muswada wa kwanza ni wa Sheria ya Fedha za Matumizi ya Serikali wa mwaka 2016, *(The Appropriation Bill),* 2016. Muswada wa pili ni wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2016, *(The Finance Bill,)* 2016 na Muswada wa tatu ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2016, *(The Written Laws (Miscellaneous (Amendments) Bill,)* 2016).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano huu jumla ya maswali 469 ya msingi na mengine 1,365 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Vile vile jumla ya maswali 33 ya msingi na 19 ya nyongeza ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu ya kila siku ya Alhamisi yaliulizwa na kupata majibu yake sawasawa. Aidha, Waheshimiwa Wabunge, waliridhia Mkataba wa Kimataifa wa Udhibiti wa Matumizi ya Dawa za Mbinu za Kuongeza Nguvu Michezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jumla napenda kutoa taarifa katika Bunge lako Tukufu kuwa, shughuli zote zilizopangwa katika Bunge la Tatu zimekamilishwa kwa ufanisi mkubwa. Nawashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge na Wataalam wetu kwa michango yao mizuri iliyofanikisha shughuli za Bunge letu, nawapongeza sana wote kwa ujumla wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo mazuri, kama kawaida ya Mabunge mengi ya kidemokrasia duniani, hakukukosekana purukushani za hapa na pale. Katika Mkutano huu wa Bunge kumekuwa na taswira potevu waliyojaribu kuijenga lakini pia mafanikio baadhi ya wanasiasa wakiwemo Wabunge wa Kambi ya Upinzani, kwa wananchi wetu, kwa Jumuiya ya Kimataifa na kama vile kuna kuminywa kwa demokrasia ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri, wananchi wetu na wadau wa maendeleo wamebaini kuwa, Upinzani katika Taifa letu bado haujakomaa kisiasa kwa sababu si jambo la kawaida kwa Mbunge kuzitoa hoja za Bungeni na kuzipeleka mitaani, eti zijadiliwe na wananchi na kisha zitolewe uamuzi. Iwapo hilo linawezekana basi kusingekuwa na umuhimu wa kuwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sintofahumu inayojitokeza kwa baadhi yetu kuhusu nafasi ya Bunge katika kutunga sheria na kuisimamia Serikali, napenda nitoe ufafanuzi ufuatao kwa mhutasari. Kwanza Ibara ya 100

na Ibara ya 101 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka1977, imetoa haki na kinga kwa Waheshimiwa Wabunge, ili waweze kujadili na kuhoji utendaji wa Serikali kwa uhuru bila mashaka yoyote ya kuweza kushtakiwa wanapotimiza wajibu wao huo wakiwa ndani ya Bunge. Kinga ya aina hiyo haijatolewa kwa mwananchi yeyote yule nchini na kwa maneno mengine Mbunge, hajafungwa mdomo, labda aamue kujifunga mdomo yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Kwa mantiki hiyo, kitendo cha baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kususia vikao vya Bunge, hakitoi picha nzuri kwa wananchi waliotuchangua kuwasilisha matatizo yao katika Bunge hili. Hivyo, natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge hao kutafakari upya uamuzi wao na niwasihi kwa busara zao waingie Bungeni, ili kwa pamoja kwa ushirikiano tuweze kutoa ushauri kwa Serikali yetu ambao utaliletea Taifa letu maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge letu linaongozwa na Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo kila mmoja anazifahamu, hivyo ni vyema tukazifuata ili kuondoa manung'uniko yasiyokuwa ya lazima. Endapo kuna utata katika jambo lolote ndani ya Bunge letu, zipo taratibu tulizojiwekea na kanuni za kufuata ili kupata ufumbuzi wa jambo hilo. Kwa kususa kuingia Bungeni, kunaweza kusiwe na tija kwa tunaowawakilisha na kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba kabla ya kuanza kwa mjadala wa Bajeti wa mwaka 2016/2017, tulipata fursa ya kujadili na kuidhinisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kuanzia mwaka 2016/2017 hadi mwaka 2020/2021. Katika mpango huo yameainishwa maeneo makuu manne (4) ya kipaumbele kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza, ni kukuza na kujenga msingi wa uchumi wa viwanda. Eneo hili litahusishwa kuongeza uzalishaji na tija katika sekta zinazoweza kuchochea na kuharakisha maendeleo ya viwanda ambazo ni pamoja na Sekta ya Kilimo, inayojumuisha kilimo cha mazao, mifugo, uvuvi na misitu lakini pia Sekta ya Madini na Utalii.

Eneo la pili, ni kufungamanisha maendeleo ya uchumi na maendeleo ya watu. Eneo hili litahusisha kupanua fursa za upatikanaji wa elimu bora kwa wote, kuimarisha huduma za afya, upatikanaji wa maji safi na salama, kuboresha mazingira ya kuishi na hifadhi ya jamii.

Eneo la tatu, ni kujenga mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara na uwekezaji. Katika eneo hili Serikali itaimarisha mifumo ya kisheria ili iweze kuwa rafiki na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, kuimarisha miundombinu

na huduma za msingi wezeshi, katika uendelezaji viwanda nchini, hususani upatikanaji wa nishati ya umeme wa uhakika na bei ya chini, upatikanaji wa maji na miundombinu ya uchukuzi, usafirishaji na mawasiliano kama vile reli, barabara, bandari, usafiri wa anga, usafiri wa majini na TEHAMA.

Eneo la nne, ni kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya mpango. Lengo la hatua hii ni kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa wito kwa waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kushirikiana na Serikali na kila mmoja wetu kuwajibika katika nafasi yake wakati wa kuutekeleza mpango huo ili tufikie malengo hayo ambayo tumejiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti mwaka 2016/2017. Kama nilivyowaeleza katika utangulizi wa hotuba yangu, mpango huo umeweka mkazo wa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kutekeleza mpango wa bajeti ya Serikali ambayo imeainishwa kwa kina na kwa ufasaha mkubwa na Waheshimiwa Mawaziri wakati wa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya sekta zao kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, Waziri wa Fedha na Mipango, wakati akiwasilisha Bajeti ya Serikali na pia alipohitimisha hoja yake, alitoa maelezo ya ufafanuzi wa kina kwa hatua za kibajeti na kisera zitakazotekelezwa na Serikali katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niungane na Waheshimiwa Mawaziri ambao wamefanya kazi yao nzuri sana katika Bunge hili la Bajeti, kwa kuweka msisitizo katika maeneo yafuatayo:-

Eneo la kwanza ni kuhusu kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali na umuhimu wa kila mwananchi kulipa kodi na eneo la pili ni kudhibiti matumizi ya fedha za umma. Naomba kuyaelekeza kwa muhtasari maeneo haya mawili niliyoyaainisha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mambo ambayo yamechukua uzito mkubwa katika majadiliano ya Bunge hili, ni mahitaji makubwa ya fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uendeshaji wa shughuli za Serikali ikilinganishwa na kiasi cha fedha kinachoweza kupatikana kwa njia ya kodi. Kama mlivyoona katika majadiliano Bungeni, wakati wote mahitaji yalizidi kiasi cha fedha kinachoweza kukusanywa kwa njia ya kodi na hivyo kutulazimu kuwa na vipaumbele vichache vinavyoweza kuleta msukumo mkubwa katika kukuza uchumi na kuwaletea maendeleo wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hiyo, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwamba, Serikali itaimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kudhibiti mianya yote ya ukwepaji wa kodi na kuchukua hatua kama zifuatazo:-

Kwanza, kuboresha mazingira ya uendeshaji wa biashara na uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuweka mifumo ya kurahisisha usajili wa makampuni ya utoaji wa leseni na urasimishaji wa shughuli zisizo rasmi za wafanyabiashara wadogo ili kupanua wigo wa mapato.

Mbili, tutaimarisha usimamizi wa matumizi ya vifaa na mifumo ya kielektroniki katika maeneo yote ya Mamlaka za Bandari Tanzania, vituo vyote vya Mmlaka ya Mapato Tanzania na katika Taasisi mbalimbali zinazokusanya mapato ya kodi na yasiyo na kodi ikiwemo Serikali za Mitaa na Halmashauri zote nchini.

Tatu, Serikali itaanzisha kikosi maalum cha kufuatilia kwa karibu matumizi ya mashine za kielektroniki *(EFDs)* za kutoa risiti kila mfanyabiashara anapouza bidhaa au huduma na hivyo basi kila mwananchi unaponunua bidhaa yoyote ile dai risiti.

Nne, kuhakikisha kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA)* wanashirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao, *(eGovenment)* kutekeleza mfumo wa kuwa na dirisha moja, yaani *Electronic Single Window System* na pia kudhibiti mizigo yote inayoingia na kutoka katika bandari kavu *(ICDs)* pamoja na kudhibiti kikamilifu taarifa zinazoandaliwa na bandari kavu ili kuzuia ukwepaji kodi.

Tano, kuziwezesha Halmashauri katika kujenga uwezo wa kusimamia ukusanyaji mapato kwa kuboresha mikataba ya mawakala wanaokusanya mapato kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Sita, Serikali itajenga uwezo kwa watumishi wanaohusika na ukusanyaji wa mapato na wale wanaohusika na uchunguzi na ukaguzi wa ndani wa taasisi zinazokusanya mapato. Aidha, Serikali itaimarisha usimamizi na uadilifu wa maadili wa maafisa wote wanaohusika na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hatua hizo nilizozieleza, Serikali itaendelea kuzingatia maoni yenu na ushauri wenu Waheshimiwa Wabunge wa kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato na kupanua wigo wa kodi. Tunaomba ushirikiano wa kodi kwa wadau wote wakiwemo wasomi wa vyuo vikuu na wataaluma kwa maendeleo yetu nchini, wakiwemo wafanyabiashara wakubwa na wawekezaji pia, wajasiriamali mbalimbali, wafanyabiashara wadogo wadogo na wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna ambavyo tutadhibiti Matumizi ya Serikali. Kwa upande wa udhibiti wa matumizi ya Serikali, sote ni mashahidi kwamba, Serikali ya Awamu ya Tano, chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania imeanza kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali na kuepuka matumizi ya siyo ya lazima. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali itachukua hatua zaidi za kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa bajeti ya Serikali, pamoja na matumizi ya fedha za umma. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

Moja, kufanya mapitio ya majukumu ya Wizara na Taasisi za Umma ili kuwianisha majukumu ya vyombo vya Serikali na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji.

Mbili, Wizara, Mikoa na Taasisi zote za Serikali, zitafanyiwa uhakiki wa watumishi wa umma wa mara kwa mara kwa lengo la kudhibiti ulipaji wa mishahara na malipo mengine kwa watu wasiostahili wajulikanapo kama watumishi hewa.

Tatu, viongozi na watendaji wote wa Serikalini, kuhakikisha wanaimarisha na kudhibiti matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia ukomo wa bajeti ya Fungu husika lililoidhinishwa na Bunge hili Tukufu. Aidha, Viongozi wa Bodi na Menejimenti za Mashirika ya Umma na Taasisi za Umma kuhakikisha kwamba, zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria za kuanzishwa kwake. Msajili wa Hazina na Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika na taasisi za umma wanatakiwa kusimamia kikamilifu matumizi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yaendane na majukumu ya misingi ya taasisi hizo, lakini pia uendeshaji huo uwe wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hatua hizo nilizoziainisha, naomba kupitia Bunge lako hili Tukufu, kuwaagiza Watendaji Wakuu wa Wizara, Wakala, Idara zinazojitegemea, Mashirika na Taasisi za Umma, Mikoa na Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa wanasimamia vizuri zaidi ukusanyaji wa mapato na kuwepo kwa udhibiti wa kutosha wa matumizi ya fedha za Serikali. Hatua hii itawezesha kufikia malengo tuliyojiwekea katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ni dhahiri kwamba, mamlaka hizi zina wajibu wa kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu mapato na matumizi ya Serikali pamoja na michango ya wananchi iliyotolewa. Hata hivyo, uzoefu unaonesha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, zina tatizo la kukaa na fedha kwa muda mrefu kabla ya kuzielekeza kwenye matumizi yaliyokusudiwa. Kuchelewesha kutoa fedha zilizotengwa kwa shughuli zilizopangwa ni kuchelewesha kufikia huduma muhimu kwa wananchi. Napenda kuhimiza uzingatiaji na utaratibu wa kutoa taarifa kwa wananchi

kuhusu mapato na matumizi ya hatua za fedha za Serikali katika ngazi zote ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika sekta ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukusanyaji wa Mapato katika Serikali za Mitaa. Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290, inazipa uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoza na kukusanya kodi, ushuru na ada mbalimbali kama vyanzo vya mapato vya Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Sheria hiyo pia inazipa mamlaka hizo kuteua mawakala wa kukusanya mapato hayo kwa niaba ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Hatua ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutumia mawakala ni miongoni mwa mikakati ya kuboresha ukusanyaji mapato na pia kutoa muda mwingi zaidi kwa watumishi wa mamlaka kushughulika na majukumu ya msingi ya Halmashauri na hasa utoaji wa huduma kwa wananchi na usimamizi wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na dhamira nzuri ya hatua hizo, Serikali imebaini changamoto za kiufundi katika kufanya tathmini ya vyanzo vya mapato, ugumu katika kupata mawakala wenye weledi katika ukusanyaji mapato na kubuni vyanzo vipya vya mapato na wakati mwingine watumishi wenyewe kujipa uwakala kinyume na taratibu zinazomzuia mtumishi kufanya biashara na taasisi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili napenda kueleza kwamba tunashuhudia migogoro kama hii katika Halmashauri zetu za Wilaya, watumishi na wakati mwingine hata Waheshimiwa Madiwani kulazimisha Halmashauri zao kuzipa kazi kampuni zao na kupata zabuni, jambo hili halikubaliki. Tunazo taarifa mgogoro uliko pale Nzega, kati ya Waheshimiwa Madiwani, watumishi na Mkurugenzi wao, kutaka zabuni zote zipewe Waheshimiwa Madiwani na watumishi, jambo hili halikubaliki hata kwa kanuni na sheria za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa siyo kila chanzo cha mapato ya Halmashauri zitakusanywa na ufanisi kwa kutumia au kwa kutotumia mawakala, Halmashauri zitaelekezwa kwa waraka ni vyanzo vipi vinahitaji kutumia mawakala na kwa baadhi ya vyanzo katika ukusanyaji wa mapato zitapaswa kukusanywa na Halmashauri zenyewe kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa na Serikali.

Moja ya miongozo hiyo ni kwamba, kuanzia sasa aidha, kutumia mawakala au Halmashauri zenyewe, ni lazima fedha zinazokusanywa ziwekwe kwenye akaunti ya Halmashauri husika na kutumia mifumo ya kielektroniki ili kupunguza au kumaliza kabisa masuala ya *cash transactions*. Aidha, Halmashauri zikubaliane na wakala kiasi gani cha asilimia ya makusanyo kitalipwa kwa wakala na malipo yafanyike baada ya kukusanywa na kuingizwa kwenye akaunti ya Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuziagiza Halmashauri zote nchini kwamba, kuanzia tarehe 1 Julai, 2016, zihakikishe zinatumia mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato yao, kulipa, kuweka na kutekeleza kikamilifu mikakati madhubuti ya kuboresha makusanyo, iwe yanakusanywa na Halmashauri au na Mawakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwajibikaji na uadilifu. Hili ni eneo muhimu sana ambalo tutalitilia mkazo. Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea kuimarisha uwajibikaji na maadili ya viongozi, watendaji na watumishi wa umma ili kujenga imani ya wananchi kwa viongozi wao na Serikali yao pia. Hatua hiyo inakusudia kuhakikisha kuna matumizi mazuri ya rasilimali za umma, kudhibiti mianya ya ukiukwaji wa maadili na rushwa na kujenga ujasiri wa kusimamia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viongozi pia wanatakiwa kuepuka vitendo vya rushwa, mgongano wa maslahi, kushindwa kutoa tamko la rasilimali za madeni au kutoa tamko la uongo, unyanyasaji wa kijinsia, kuomba, kupokea kushawishi na kujipatia maslahi kifedha yasiyostahili na kukiuka miiko ya uongozi. Serikali ya Awamu ya Tano haitasita kuchukua hatua stahiki kwa viongozi wa umma au watumishi watakaokiuka maadili ya utumishi wa umma, hivyo kuzingatia maadili siyo suala la hiari bali ni lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Makosa ya Rushwa na Ufisadi. Serikali ya Awamu ya Tano, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kurejesha imani ya wananchi kwa Serikali yao, kutokana na hatua madhubuti zinazochukuliwa na Serikali katika kupambana na vitendo vya rushwa na ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipoanza mapambano haya baadhi ya watu walidhani ni nguvu za soda tu, si kweli hata kidogo. Napenda kulitaarifu Bunge hili Tukufu kuwa, zoezi hili ni endelevu na tangu mwezi Novemba, 2015, Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani mapambano hayo yamechukua sura ifuatayo:-

Kwanza, uchukuaji wa hatua za kinidhamu dhidi ya mtumishi yeyote wa umma anayetuhumiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa na ufisadi kwa kuwasimamisha kazi na kuendesha uchunguzi ili hatua stahiki za kisheria na za kiutawala ziweze kuchukuliwa. Mbili, kutengua uteuzi na madaraka kwa viongozi wa juu walioshindwa kutekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine kubwa iliyochukuliwa ni kuanzishwa kwa Mahakama Maalum ya kushughulikia Makosa ya Rushwa na Ufisadi. Itakumbukwa kuwa wakati wa kampeni za uchaguzi Mkuu wa Mwaka

2015, aliyekuwa mgombea urais wa CCM, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli aliahidi kuanzisha Mahakama hiyo na sasa ahadi hiyo kaitimiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutimizwa kwa ahadi hiyo ndani ya kipindi cha miezi isiyozidi sita, inaonesha dhamira ya dhati ya Serikali kushughulikia makosa ya rushwa na ufisadi kwa utaratibu wa kudumu. Hivyo, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mahakama hiyo sasa itaanza rasmi kazi zake tarehe 1 Julai, 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya faida ya kuwa na Mahakama hii Maalum ni kama ifuatavyo:-

Moja, mashauri ya rushwa na ufisadi yatasikilizwa kwa muda mfupi zaidi na hivyo haki kutendeka kwa pande zote mbili, yaani upande wa watuhumiwa na upande wa Jamhuri.

Mbili, Majaji watakaosikiliza mashauri haya, watakuwa na uelewa mpana zaidi kuhusiana na sheria za kushughulikia masuala ya rushwa na ufisadi.

Tatu, uwepo wa Mahakama hii utaimarisha zaidi taasisi za uwajibikaji nchini zinazohusika na mapambano dhidi ya rushwa, mathalani Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa Nchini *(PCCB)*.

Nne, Mahakama itawafanya watu waliozoea rushwa na ufisadi kujiuliza mara mbili kabla ya kuufanya uhalifu huo yaani kwa kuwa *deterred*. Sambamba na kuanzishwa Mahakama hiyo, Sheria ya Kuzuia na kupambana na rushwa nchini namba 11 ya mwaka 2007 inafanyiwa marekebisho ili kuongeza ukubwa wa adhabu zitakazotolewa hivi sasa. *(Makofi)*

Tano, kuhamasisha watoa taarifa za rushwa na ufisadi, yaani *whistle blowers* kwa kuwa Serikali imebaini kuwa, ili Mahakama hiyo ifikie malengo ya kuanzishwa kwake, budi iwepo sheria madhubuti ya kuwalinda wananchi wetu wanaotoa taarifa. Hivyo, Serikali ipo katika mchakato wa kuipitia upya sheria husika ili kuwahakikishia usalama wao wanapotoa taarifa za kiutendaji kwa makosa ya rushwa na ufisadi na kuwapa ujasiri wa kutoa ushahidi Mahakamani bila uoga wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia mwisho, ni kuhamasisha wafanyabiashara kufanya biashara zao bila mashaka, umuhimu kwao ni kulipa kodi kwa wale waliokuwa wanakwepa kulipa kodi. Pia kuwapa imani wafadhili wetu kwamba fedha wanazochangia za maendeleo nchini kwetu zitatumika bila matatizo. Zoezi hilo linaendelea ili kuhakikisha kwamba hakuna fedha ya Serikali inayopotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapenda kuwashukuru wananchi wote waliotoa taarifa zilizosaidia kubaini watumishi wa umma na raia ambao wanajihusisha na vitendo vinavyokiuka maadili na kuisababishia Serikali hasara. Ni kweli kwamba Serikali haiwezi kufanikiwa peke yake katika vita dhidi ya ufisadi na maovu mengine. Kama wananchi na wadau wengine hawataiunga mkono Serikali, katika jitihada zake za kupambana na vitendo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivy, naendelea kutoa rai kwa wananchi wote na wadau wengine wapenda maendeleo wenye uchungu na nchi yao, hususani Asasi Zisizokuwa za Serikali na Asasi za Kijamii kuendelea kutoa ushirikiano ipasavyo ili kufanikisha mikakati ya kupambana na rushwa na ufisadi na vitendo vingine visivyo vya kiadilifu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ni jukumu la kila mwananchi nchini kote kuhakikisha anatimiza wajibu wake kwa kufanya kazi kikamilifu kuanzia ngazi ya familia. Tabia ya baadhi ya vijana kuacha kazi na kujiingiza kwenye unywaji pombe au kucheza *pool* kwa siku nzima, iachwe mara moja. Aidha, kwa upande wa uwajibikaji wamiliki wa maeneo ya starehe, baa na *pubs*, wazingatie sheria na muda unaotakiwa kufungua biashara hizo. Kinyume cha hapo, hali hiyo ikiachiwa iendelee hivyo, nguvu kazi kubwa ya Taifa ambayo ni vijana, itapotelea kwenye ulevi na hivyo kushindwa kutoa mchango wake kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhibiti hali hiyo, nawaagiza Wakuu wa Mikoa wote na Wakuu wa Wilaya wote ambao jana mmeshateuliwa, kuhakikisha vijana wanawajibika ipasavyo kwenye maeneo yenu na kufanya kazi halali na kuhakikisha kwamba maeneo ya starehe baa na *pubs* hayafunguliwi wakati wa muda wa kazi ili vijana na watu wote waende kufanya kazi kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla, elimu kwa umma iendelee kutolewa na usimamizi uendelee kuimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa chakula nchini. Uchambuzi wa awali wa taarifa ya chakula nchini, uliofanywa mwezi Mei wa mwaka huu wa 2016, unaonesha kwamba hali ya chakula nchini ni ya kuridhisha na matarajio ya uzalishaji kwa msimu huu wa kilimo wa 2015/2016 ni mzuri pia. Kati ya Halmashauri 174 zilizofanyiwa tathmini, Halmashauri 52 sawa na asilimia 30 zitakuwa na ziada ya chakula. Halmashauri 116 sawa na asilimia 66, zitakuwa na utoshelevu wakati wote na katika Halmashauri saba sawa na asilimia nne katika Mikoa mitano ya Iringa, Kilimanjaro, Dodoma, Mwanza na Pwani zitakuwa na upungufu wa chakula kutokana na sababu mbalimbali kama vile mafuriko na upungufu wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, hali halisi itadhihirika baada ya kukamilika kwa tathmini ya uzalishaji wa mazao ya chakula, iliyomalizika tarehe

30 Juni, 2016. Tathmini hiyo itabainisha kwa undani zaidi viwango vya uzalishaji, mahitaji na utoshelevu wa chakula nchini. *NRFA* ikiwa ni Taasisi inayoshughulikia chakula. ijipange vizuri kununua mahindi hayo, kama nilivyoagiza kwa kuanzisha vituo vya ununuzi karibu na wananchi kwenye maeneno yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 1 Julai, 2015, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, ulikuwa na akiba ya nafaka tani 353,702 katika kipindi cha mwaka 2015/2016. Wakala uliendelea na ununuzi wa nafaka katika Kanda ya Songea, Makambako na Sumbawanga. Akiba hii imewezesha Serikali kukabiliana na uhaba wa chakula uliokuwa umejitokeza sehemu mbalimbali nchini, katika mwaka wa 2015/2016, ambapo jumla ya tani 31,666 zilipelekwa kwenye sehemu za uhaba wa chakula nchini, hivyo, akiba ya chakula katika maghala hadi tarehe 9 Juni, 2016 tuna tani 62,312 kama akiba. Aidha, Wakala unatarajia kufunga mwaka tukiwa tuna kiasi cha tani 50,000 za nafaka katika mwaka ujao 2016/2017. Wakala umepanga kunua kiasi cha tani 10,0000 za nafaka kutoka katika maeneo yenye ziada kubwa ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa sukari nchini; katika siku za hivi karibuni, nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya upatikanaji na usambazaji wa sukari, kutokana na ukweli kwamba mahitaji ya sukari ni makubwa kuliko uzalishaji. Kutokana na hali hiyo, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Serikali imetoa vibali vya kuingiza sukari nchini Tani 80,000 ili kufidia pengo lililopo. Hadi kufikia tarehe 9 Juni, 2016, jumla ya tani 23,874.6 za sukari zilikuwa zimeingizwa nchini. Aidha, taarifa zilizopo zinaonesha kuwa, hadi tarehe 30 Juni, 2016, tayari tani 63,000 za sukari zimeingizwa na kusambazwa maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana, pamoja na kuingizwa sukari nchini, kwa kiasi hicho kikubwa katika kipindi kifupi, bado soko la sukari limeendelea kuyumba kutokana na hisia tu kuwa sukari iliyopo haitoshi. Matokeo yake ni kwamba, sukari imeendelea kuuzwa kwa bei ya rejereja ya kati ya Sh. 2,500 na 3,000 kwa kilo, katika Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya. Serikali itaendelea kusimamia kushuka kwa bei hiyo, ili mlaji wa chini amudu kuinunua kwa gharama ndogo zaidi na kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, njia pekee na endelevu ya kuondokana na uhaba wa sukari ambao umekuwepo miaka yote, ni kuongeza uzalishaji wa sukari yetu wenyewe. Hivyo, Serikali inakamilisha Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Sukari kwa Miaka Mitano ijayo mwaka 2016/2017 - 2020/2021. Lengo kuu la Mpango Mkakati huo, ni kuongeza uzalishaji kama ifuatavyo:-

Moja, ni kufanya tathmini upya ili kujua mahitaji halisi ya sukari nchini kwani pamoja na kiwango kilichoingia cha tani 63,000 bado kuna upungufu mkubwa.

Pili, kuongeza uzalishaji wa sukari katika viwanda vilivyopo hadi kufikia tani 459,503 kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 kwa kuimarisha tija katika uzalishaji miwa na kuongeza ufanisi wa viwanda hivyo.

Tatu, kuanzisha viwanda vipya vya sukari, ambapo vitaanzishwa viwanda vya kati vitatu, katika Wilaya za Kilosa, Mvomero na Kilombero pamoja na kuanzisha viwanda vikubwa katika maeneo ya Bagamoyo, Rufiji, Kigoma na Kidunda. *(Makofi)*

Nne, kuongeza tija na uzalishaji wa miwa inayolimwa na wakulima wadogo, kwa kuboresha upatikanaji wa pembejeo, miundombinu ya umwagiliaji na kuboresha mfumo wa uendeshaji wa Vyama vya Wakulima wa Miwa.

Tano, kufanya marekebisho ya Sheria ya Sukari ya mwaka 2001 na Kanuni zake ili kuweka wigo mpana zaidi wa kusimamia na kuboresha hatua za udhibiti katika tasnia ya sukari.

Sita, kupunguza gharama za uzalishaji kwa kuwajengea wakulima na wazalishaji wa sukari uwezo wa kitaalam ili waweze kuendesha kilimo na kuzalisha miwa kwa tija na kuwafunza kanuni bora za uzalishaji miwa na sukari, kuboresha huduma za utafiti, mafunzo na ugani kwa wakulima wote wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa ujenzi wa Uchumi wa Viwanda. Dhima ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa Mwaka 2016/2017 – 2020/2021 ni kuanza ujenzi wa Taifa lenye Uchumi wa Kati, unaoendeshwa na viwanda ifikapo mwaka 2025. Ili kufikia azma hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, imeandaa Mpango Kazi wa kutekeleza malengo hayo katika kipindi cha miaka mitano (2015 - 2020). Mpango huo utahusisha sekta zote za uchumi na huduma ili kutekeleza jukumu la kuongeza mchango wa sekta ya viwanda katika pato la Taifa na kuongeza ajira kwa umma hususan kwa vijana na wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huo unakusudia kuendeleza viwanda vinavyotumia malighafi za ndani na hususan kwenye sekta ya kilimo na maliasili; viwanda vinavyozingatia fursa za kijiografia; viwanda vinavyotumia nguvu kazi zaidi kwa kuzalisha ajira; lakini viwanda vinavyoendana na ukuaji wa miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huo unakusudia pia kuanzisha viwanda, vitakavyozalisha bidhaa kukidhi mahitaji ya kibiashara ndani na nje ya

nchi na kuwekeza zaidi kwenye rasilimali watu na viwanda vinavyozaa viwanda vingine. Viwanda vinavyolengwa ni vya mbolea na kemikali zitokanazo na mafuta jamii na petroli na gesi asilia, chuma, nguo na mavazi. Usindikaji mazao ikiwemo mafuta ya kula, ubanguaji wa korosho, matunda, maziwa na bidhaa zitokanazo na maziwa pamoja na ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno mengine, msingi wa maendeleo yetu kutoka sasa ni Sekta ya Viwanda. Serikali imechukua uamuzi huo kwa sababu imejiridhisha kuwa, kutokana na uzoefu na historia ya nchi yetu, ujenzi wa uchumi wa viwanda utaliweka Taifa letu katika kundi la Mataifa yanayozalisha bidhaa bora zaidi na zenye ushindani wa soko la Kimataifa, badala ya kuwa chanzo cha malighafi na soko la bidhaa kwa viwanda vya Mataifa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha muhimu hapa ni Watanzania kubadili mtazamo na kujenga utamaduni unaolenga kuwa na Taifa lenye uchumi wa viwanda. Hivyo ni pamoja na kila mmoja wetu kwa uwezo wake, kulenga kuwekeza katika viwanda na kupenda kununua bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto tulizojifunza kutokana na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Viwanda vya Msingi *(Basic Industrialization Strategy)* miaka ya 1980, ambapo viwanda vingi vilivyoanzishwa chini ya usimamizi wa Serikali, vilikufa kutokana na sababu mbalimbali, zimeifanya Serikali ya Awamu ya Tano katika kutekeleza Mpango huo, kuendelea kuipa sekta binafsi jukumu la ujenzi na uendeshaji viwanda na biashara nchini na Serikali ibaki na jukumu la kuweka mazingira wezeshi na rafiki ya kufanya biashara na uwekezaji. Huo ndiyo mwelekeo katika ujenzi wa sekta ya viwanda unaohamasishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelazimika kutoa ufafanuzi huo wa kisera kwa sababu katika siku za karibuni, kumekuwepo na upotoshwaji kwa baadhi ya watu kudhani sasa Serikali itajiingiza moja kwa moja katika ujenzi wa viwanda na kufanya biashara. Napenda kuihakikishia sekta binafsi kuwa, itaendelea kuenziwa kwa sababu ni injini pekee ya kukuza uchumi na maendeleo ya viwanda katika karne hii. Aidha, Wizara husika zimejipanga vema katika kuhakikisha Watanzania wanashirikishwa ipasavyo katika kujenga uchumi wa viwanda.

Ili kuhakikisha mafanikio yaliyokusudiwa yanapatikana, ni lazima kuzingatia mambo yafuatayo:-

Kwanza, kuhakikisha viwanda vilivyopo vinafanya kazi kwa uwezo mkubwa na bidhaa kutoka nje zinatozwa ushuru, zinatozwa ushuru stahiki na kukidhi viwango vya ubora ili kudhibiti ushindani usio halali nchini kwetu.

Mbili, kuhimiza na kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vitakavyotumia malighafi ipatikanayo nchini, mathalani viwanda vya saruji, *gypsum* na makaa ya mawe ambayo tayari yanapatikana hapa nchini kwetu kwa wingi zaidi. *(Makofi)*

Tatu, kuondoa vikwazo vinavyopunguza uwezo wa kiushindani kwa viwanda vyetu kwa uboresha wa mazingira ya uwekezaji ili Tanzania iwe kivutio kwa wawekezaji wa nje na wa ndani ya nchi. Mathalani kuhakikisha kunakuwepo na umeme wa kutosha na wa uhakika, maji, uchukuzi, na usafirishaji wenye ufanisi, urahisi wa taratibu za udhibiti na usimamizi kwa kupunguza mlolongo wa taratibu na uwingi wa tozo.

Nne, kuhamasisha wawekezaji wakubwa wa ndani na nje ya nchi, kuwekeza katika sekta ya viwanda katika ngazi ya Kanda na Taifa.

Tano, kuhakikisha kuwa viwanda vyote vilivyobinafsishwa vinafanya kazi kwa ufanisi, ama kwa kuwataka wawekezaji wa viwanda husika kufanya uwekezaji mpya ndani ya miezi 12, watakaoshindwa kunyang'anywa ili wapewe wenzao wenye uwezo wa kuwekeza kwenye uwekezaji mpya na wenye uwezo.

Sita, Maafisa Biashara wote wa Mikoa, kupewa jukumu mahsusi la kuwa kiungo kati ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, katika kusimamia na kuhamasisha uwekezaji wa viwanda, katika mikoa na pia biashara na masoko.

Saba, kila Mkoa kutenga maeneo mahsusi ya uwekezaji viwanda, yatakayowekewa miundombinu ya msingi ili kumwondolea mwekezaji usumbufu wa kutafuta eneo la uwekezaji ambao hivi sasa huchukua nafasi kubwa, hata miaka mitatu kabla ya uwekezaji haujaanza. Badala yake tunataka mwekezaji mwenye fedha aweze kuanza ujenzi wa kiwanda, ndani ya mwezi mmoja na huo ndiyo mkakati wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuwasaidia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, ambao wanakusudia kuwekeza katika viwanda ili kunufaika na mchango wake katika uchumi ukiwemo uzalishaji wa ajira kwa Watanzania. Pia natoa wito kwa wananchi na Watanzania wote kutambua fursa zilizopo kwa kubaini sehemu ambayo kila mmoja anaimudu katika mnyororo wa manufaa wa ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika Hotuba yangu ya Bajeti ya 2016/2017, nilielekeza kwamba Mamlaka za Mikoa na Wilaya lazima zitenge maeneo kwa shughuli za viwanda na biashara. Chini ya utaratibu huo, Mamlaka za Mikoa zitawajibika kutenga maeneo ya ujenzi wa viwanda na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji itawajibika kutoa ushauri wa kitaalam. Aidha, Wizara na taasisi zinazohusika na ujenzi wa miundombinu wezeshi, zitawajibika kuhakikisha maeneo hayo yanapatiwa huduma hizo muhimu. Mamlaka za Serikali za Mitaa, zitabeba gharama za kutenga maeneo katika Kata, Tarafa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ngazi ya Kitaifa, tutaendeleza jitihada za kutenga na kuboresha maeneo maalum ya kiuchumi ili kurahisisha uwekezaji mkubwa katika sekta ya viwanda. Kipaumbele cha kwanza ni kuhakikisha kwamba fidia inalipwa kwanza kwa maeneo yaliyotengwa katika siku za nyuma. Taarifa zilizopo zinaonesha kuwa hadi sasa, Halmashauri 10 tayari zimeshatenga jumla ya ekari 64,348 na katika Mikoa kumi ya Mara, Tanga, Ruvuma, Mtwara, Mwanza, Pwani, Arusha, Shinyanga, Iringa na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa Halmashauri nyingine kutenga maeneo ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa viwanda. Aidha, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, zihakikishe kuwa Halmashauri zote nchini zinazingatia mahitaji ya viwanda, kwa kutenga maeneo maalum, katika mipango miji yake. Vile vile, nazitaka taasisi za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, zianze kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kuitaka Mifuko hiyo, iwekeze kwenye viwanda badala ya kujikita zaidi kwenye ujenzi wa majumba makubwa katikati ya miji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Ushirika Nchini; ushirika nchini umeendelea kuwa sekta muhimu katika maendeleo ya jamii, kujenga uchumi wa wanachama na kuchangia Pato la Taifa. Umuhimu huu umetokana pia na kuwaunganisha wakulima na wanachama katika uzalishaji, ukusanyaji mazao na upatikanaji wa masoko. Pia ushirika umedhihirisha umuhimu wake wa kujitokeza katika sekta mbalimbali za kiuchumi nchini zikiwemo sekta ya kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda, nyumba, usafirishaji, huduma ya madini na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali imeendelea kufanya uhakiki na kubaini uhai wa vyama vya ushirika ikiwa ni pomaja na kuboresha daftari la vyama vya ushirika nchini. Hadi kufikia Juni, 2016 uhakiki huo umebaini kuwa idadi ya vyama vya ushirika vilivyo hai ni vyama 8,766 ikiwa ni ongezeko la vyama vya ushirika 878 sawa na ongezeko la asilimia 11.1 ikilinganishwa na vyama 7,888 vilivyokuwepo kufikia mwezi Machi, 2015. Ushirika umechangia kutoa ajira za kuduma katika jamii ambapo kwa wastani kila chama huajiri takribani watendaji watano sawa na ajira 43,830 kwa idadi ya vyama vilivyopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za ushirika ni pamoja na ushirika nchini kuendelea kuwa sekta muhimu katika maendeleo ya jamii na imekumbwa na changamoto nyingi sana kama ifuatavyo:-

(i) Rasilimali nyingi za ushirika kuvamiwa na watu na Taasisi mbalimbali,

(ii) Vyama vya ushirika kuwa na madeni makubwa yasiyolipika,

(iii) Kuna ubadhilifu mkubwa sana na wizi wa kutisha katika vyama vya ushirika.

(iv) Baadhi ya rasilimali za ushirika kutoendelezwa na kukosa hati miliki.
(v) Kesi nyingi za vyama vya ushirika huchukua muda mrefu kutolewa maamuzi.

(vi) Mapungufu katika usimamizi na matumizi ya mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani kwa baadhi ya mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hatua zilizochukuliwa katika kukabiliana na changamoto hizi: Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imechukuwa hatua zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Moja; Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeandaa utaratibu wa kuzitambua mali za ushirika na kuweka mpango wa kuziendeleza kupitia mkutano ulioshirikisha Wenyeviti na Watendaji Wakuu wa Vyama Vikuu na Mabenki pamoja na Warajisi Wasaidizi wa Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbili; pia kupitia mkutano uliofanyika Dodoma na Vyama Vikuu vya Ushirika uliwekwa utaratibu wa kuhakikisha madeni ya vyama vya ushirika yanapungua na kuisha kabisa. Aidha, Tume kwa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi itakutana na Mabenki na Taasisi nyingine za fedha kujadiliana na kuweka utaratibu rafiki wa kuhakikisha kuwa madeni haya yanakwisha na utaratibu wa kutotengeneza madeni tena nao utaimarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tatu; Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeanza kuwaondoa viongozo wote wabadhirifu, wezi wakiwemo Warajisi Wasaidizi wanaosaidia wizi huo kwenye vyama vya ushirika na kuwachukulia hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nne; Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika inawasiliana na ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuhakikisha kwamba, kesi zote za vya vyama vya ushirika zinashughulikiwa kwa haraka zaidi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tano; Serikali itaendelea kurekebisha tozo za mazao mbalimbali nchini ili kukidhi matumizi ya mfumo ya stakabadhi ghalani kwa mazao kama korosho, pamba, tumbaku na mfumo wa stakabadhi ghalani utaendelea kutumika pamoja na mrekebisho ya tozo yaliyofanywa kwa mazao baadhi na yale ambayo yataendelea kufanywa ili kuhakikisha kwamba, wananchi wanapata tija kupitia mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha ushirika nchini, Serikali itahakikisha kuwa Sheria ya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 ambayo inaimarisha usimamizi wa ushirika nchini na kuainisha hatua kali ambazo zitachukuliwa dhidi ya wale wote watakaokiuka sheria hiyo, inatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa mabasi yaendayo haraka; sote tunafahamu kuwa Jiji la Dar es Salaam kwa muda mrefu limekuwa linakabiliwa na changamoto ya usafiri kutokana na ukosefu wa miundombinu ya barabara, msongamano wa magari na wingi wa abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002 inaonesha kwamba, Jiji la Dar es Salaam lina watu wapatao milioni 4.3 ambao wamekuwa wakipoteza muda mwingi njiani kutokana na msongamano wa magari, hali hiyo imewaathiri sana kiuchumi na kijamii. Kutokana na hali hiyo, Serikali mwaka 2002 ilibuni mradi wa mabasi yaendayo haraka *DART* ambao utatumia mabasi yanayobeba abiria wengi kwa wakati mmoja na ambayo yatatumia muda mfupi kusafirisha abiria kutoka sehemu moja hadi nyingine na kwa gharama nafuu. Mradi huo unajengwa kwa awamu sita na utahusisha barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa 130.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya awamu ya kwanza inayojumuisha barabara za zenye urefu wa jumla kilometa 20.9 umekamilika. Maeneo yaliyokamilika ni pamoja na Barabara Kuu kutoka Kimara mwisho hadi Kivukoni, barabara ya Kawawa kuanzia Morocco hadi Magomeni Mapipa na barabara ya Msimbazi hadi Kariakoo Gerezani. Ujenzi wa barabara hizo unajumuisha pia njia maalum za mabasi, njia za magari mchanganyiko, na njia za waendesha baiskeli na waendao kwa miguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, vituo 27 vimejengwa katika barabara maalum ya mfumo wa *DART* na Vituo Vikuu vitano, yaani *bus terminals* vimekamilika. Vituo mlisho vinne, yaani *feeder bus stations,* karakana moja ya mabasi *deport* pamoja na madaraja ya watembeao kwa miguu katika maeneo ya Kimara, Ubungo na Morocco yamekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya awamu ya kwanza, Serikali iliamua apatikane mtoa huduma ya mpito *(interim service provider)* ili miundombinu hii ianze kutumika. Mabasi

hayo yalianza kutoa huduma tarehe 10 mwezi Mei, mwaka huu wa 2016 na idadi yake kwa sasa ina mabasi 140. Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa wananchi wengi wamejitokeza kupanda mabasi hayo, lakini pia hata viongozi wa Serikali nao wanatumia mabasi hayo na wanayafurahia na wanasafiri bila bugudha yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Viongozi Wakuu nao wamepanda mabasi hayo akiwemo Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili na Mama Mwinyi, lakini pia Makamu wa Rais pia Waziri Mkuu wote wameingia kwenye mabasi hayo wamejionea huduma nzuri inayotolewa kwenye mabasi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo maradi huo unakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo mfumo usiokuwa na kasi ya kutosha ambao unasababisha msongamano wa abiria wakati wa utoaji tiketi nyakati za asubuhi na joini wakati mtandao unapokuwa umeelemewa. Abiria kugombania kupanda mabasi, kuwahi kupata viti, kutokupanga foleni wakati wa kukata tiketi na wakati wa kupanda mabasi, abiria kutofuata njia zinazobainishwa kuingia na kutoka kwenye vituo kama madaraja ya miguu, vivuko vya pundamilia na kutumia milango ya vituo vidogo na ajari zinazotokana na vyombo vingine vya usafiri kutumia kimakosa barabara za *DART* ikiwemo bodaboda, baiskeli, magari, daladala, na waenda kwa miguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuzipatia ufumbuzi wa haraka changamoto hizo, Serikali imetoa maelekezo yafuatayo:-

(1) Kila njia iwe na alama maalum kwa mfano, namba au rangi ambayo itatumiwa na mabasi yaendayo haraka ikiwa ni alama inapofanya safari yake kupitia njia hiyo ili iwe rahisi kwa abiria kutumbua kwamba, alama ile ni basi liendalo eneo fulani, inaweza kuwa ni alama au rangi kwenye mabasi hayo.

(2) Abiria kujali usafi ndani ya mabasi na kwenye vituo vya abiria. Aidha, walinzi kwenye vituo vya abiria pamoja na majukumu yao ya ulinzi na usalama wafanye pia kazi ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira katika vituo vya abiria vya mabasi hayo, kuhakikisha kuwa milango yote ya vituo inafungwa wakati wote. Usafiri huu ni wa Kimataifa na umeanza kutoa sura kama ambayo wenzetu wanatumia kule nje ya nchi. *(Makofi)*

(3) Muda wa kuanza safari alfajiri sasa uanze saa kumi na moja alfajiri ili kuruhusu abiria kuanza safari zao mapema.

(4) Maduka ya kununua kadi yatambulishwe haraka ili Wananchi waanze kumiliki kadi hizo zitakazojulikana kwa jina la *DART card.*

(5) Kuweka taa maalum za barabarani kwenye makuno hatari ya barabara ili kuzuia magari mengine yasipite wakati mabasi yaendayo haraka yakiwa yanapita. Lengo ni kuepusha ajari na mabasi hayo kutopata vikwazo katika safari yake.

(6) Marufuku kwa chombo au mtu yoyote kutumia njia za mabasi hayo ya *DART*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia mabasi hayo yakitumia muda mfupi zaidi usiozidi dakika 45 kwa safari ya kutoka Kivukoni hadi Kimara na kuwezesha abiria kuwahi kwenye shughuli zao za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya mradi huo kuanza safari ya aina hiyo ilikuwa inatumia zaidi ya masaa mawili. Aidha kumekuwepo kwa faida za kiuchmi na kijamii kwa wakazi wanaoishi karibu na barabara ya *DART* ambao wameanza kuacha magari yao binafsi na kuanza kupanda mabasi hayo na kwa kufanya hivyo, wameweza kuokoa fedha nyingi sana za kununua mafuta ya magari yao ikiwemo huduma bora kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza mchakato wa mpango wa ujenzi wa awamu ya pili na tatu katika barabara zitokazo katikati ya Jiji mpaka Mbagala na katikati ya Jiji mpaka Gongolamboto ili wananchi wa maeneo hayo waanze kufaidi huduma hizo za mabasi yaendayo haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwaomba wananchi na wakazi wote wa Dar es Salaam ambao wamepata fursa ya kutumia huduma hii kutoa ushirikiano katika uendeshaji wa mradi huo. Tumeanza vizuri, naomba tushirikiane kutunza miundombinu iliyopo, ikiwa ni pamoja na kulinda mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, vyombo vingine vya usafiri haviruhusiwi kutumia miundombinu ya mabasi yaendayo haraka kwa sababu vitayasababishia ajali mabasi hayo. Vyombo vya dola vihakikishe kuwa wale wanatumia barabara hizo kinyume na utaratibu uliopo wachukuliwe hatua kali zaidi ili iwe fundisho kwa wengine wanaotaka kutumia barabara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya umeme vijijini; tarehe 23 mpak 27 mwezi Mei, mwaka huu 2016 nilipata fursa ya kumwakilisha Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, kwenye Mkutano wa Mwaka wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* uliofanyika Lusaka, Zambia, Kaulimbiu ya Mkutano ule ilikuwa inasema, *Light up Africa, using centralized and decentralized mini-grid solutions*, inaakisi azma ya Serikali yetu kusambaza nishati ya umeme nchini katika ngazi zote hadi vijijini. Hivyo, miongoni mwa maazimio ya Mkutano huo

ilikuwa kuzitaka nchi za Afrika kutekeleza kaulimbiu hiyo kwa vitendo. Katika utekelezaji wa kaulimbiu hiyo:

Moja, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuyapatia maeneo yaliyo nje ya Gridi ya Taifa nishati bora ikiwa ni pamoja na maeneo ya visiwa. Wakala wa Usambazaji wa Umeme Vijijini *(REA)* inakamilisha taratibu za uendeshaji kwa waendelezaji wa *mini-grids.* Taratibu hizi zinategemewa kukamilika mwezi Julai, 2016 ili kuweza kushindanisha waendeshaji wa *mini-grids*, *micro-grids* na *solar home systems*. Aidha, Serikali za Sweden na Uingereza pia zimechangia katika Mfuko wa Nishati Vijijni ili kuendeleza mifumo hiyo. *REA* imeanzisha utaratibu wa kutoa mikopo, yaani *credit facility,* kwa ajili ya kukopesha waendelezaji wa nishati jadidifu *(renewable energies)* maeneo ya vijijini. Wakala pia imeanzisha Mfuko wa Ruzuku, *(Revolving Fund Facility)* kwa waendelezaji nishati jadidifu ambao utachangiwa na wadau mbalimbali wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *REA* itashirikiana na kampuni tanzu ya *TANESCO* na *Tanzania Geothermal Development Company Limited,* ili kuvipatia nishati bora vijiji vilivyo katika maeneo ambapo miundombinu ya jotoridi itajengwa.

Mheshmiwa Naibu Spika, mpango wa tatu wa miradi ya *REA*; Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, Ibara ya 43(c) (iii), inaielekeza Serikali kutekeleza Awamu ya Tatu ya Mpango wa *REA* ambao utalenga kuongeza wigo wa usambazaji umeme kutoka *REA* I na II zilipoishia, kufikisha umeme kwenye huduma za jamii kama vile shule zote za sekondari, shule zote za msingi, hospitali na vyanzo vya maji, kuongeza idadi ya vijiji ambavyo vinafikiwa na umeme, na kupeleka umeme maeneo yote ambayo siyo tija kwa *TANESCO* kuwekeza. Ili kutekeleza mipango hiyo, Serikali itatekeleza mambo yafuatayo:-

Moja, ule mradi wa *Densification* kwa ajili ya kuongeza miundombinu ya nishati ya umeme kwenye maeneo ambayo *REA* I na II imepita, lakini vijiji vingine havijapewa huduma ya umeme. Serikali za Norway na Sweden zimechangia fedha katika Mfuko wa Nishati Vijijini ili kutekeleza mpango huu, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mbili, Kufikisha huduma ya nishati bora kwa vijiji vyote ikiwa ni pamoja na maeneo ya vijiji vilivyo nje ya Gridi *(Off-Grid)*, lengo likiwa ni kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii na hatimaye kuongeza pato la mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla wake, lakini;

Tatu, kutenga kiasi cha shilingi bilioni 534.4 za ndani na shilingi bilioni 500 toka Benki ya Dunia, kwa muda wa miaka mitano, ili kuendeleza nishati vijijini. Wakala unaendelea kuhamasisha sekta za umeme na binafsi ili zishiriki katika uendelezaji wa miundombinu ya nishati bora maeneo ya vijijini ambayo hayana tija kwa *TANESCO* kuwekeza kulingana na Sheria ya Nishati Vijijini ya mwaka

2005 na Sheria ya Umeme ya Mwaka 2008, zinatoa fursa na miongozo ya jinsi sekta hizi zitakavyoweza kushiriki katika kutoa huduma hii muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mpango wa elimu bila malipo; Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ilianza utekelezaji wa ahadi ya utoaji wa elimu bila malipo kuanzia elimu ya awali hadi Kidato cha Nne kwa shule za umma kuanzia mwezi Januari 2016. Hii ni ahadi ambayo Mheshimiwa Rais pamoja na Makamu wa Rais waliitoa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Aidha, ahadi hii inazingatia Kifungu cha 52(a) cha Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, kinachohimiza uandaaji wa mfumo, mwenendo na taratibu nyumbufu za kutoa Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi bila malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, wadau mbalimbali pamoja na wananchi kwa kuunga mkono utekelezaji wa mpango huu. Aidha, niwashukuru wananchi ambao wametoa mwitikio chanya unaojidhihirisha kwa ongezeko kubwa na la kihistoria la uandikishaji wanafunzi katika ngazi mbalimbali. Kwa mfano, hadi mwezi Machi, mwaka 2016 wanafunzi wa elimu ya awali 971,717 waliandikishwa nchini kote, sawa na ongezeko la asilimia 10.74 ya wanafunzi 877,489 walioandikishwa mwaka 2015. Aidha, wanafunzi 1,896,584 wameandikishwa darasa la kwanza, sawa na ongezeko la asilimia 36.7 ikilinganishwa na wanafunzi 1,387,499 walioandikishwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila jambo jema halikosi changamoto, na ndivyo ilikuwa katika mpango huu. Hivyo, katika kuutekeleza mpango huo kumekuwapo na changamoto kadhaa ikiwemo upatikanaji wa miundombinu, samani pamoja na uelewa wa jamii juu ya wajibu wao kuhusu dhana ya elimu bila malipo. Katika kukabiliana na changamoto hizo, kati ya mwezi Desemba, 2015 hadi mwezi Mei 2016, Serikali imepeleka moja kwa moja katika ngazi zetu za shule jumla ya shilingi bilioni 94.2 kwa ajili ya fidia ya ada, michango holela mbalimbali na ruzuku ya uendeshaji wa shule. Aidha, kuanzia mwezi Julai, 2016 shule zenye idadi ndogo ya wanafunzi zitaanza kupelekewa kiwango maalumu ili kutosheleza uendeshaji wa shule hizo kwa uwiano sawa na shule zenye idadi kubwa ya wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na upatikanaji wa miundombinu mbalimbali shilingi bilioni 46.2 zimetengwa kupitia mipango na bajeti za Halmashauri kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu spika, changamoto ya upatikanaji wa madawati; jitihada za upatikanaji wa madawati zinaendelea vizuri kutokana na ushirikiano na michango kutoka kwa wadau mbalimbali. Mafanikio yaliyopatikana

yametokana na kutumia fedha za makusanyo ya ndani ya Halmashauri, wadau, kuchangia kwa hiari, harambee na uhamasishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zilizokusanywa hadi kufikia tarehe 17 Juni, 2016 zinaonesha kuwa madawati mapya 552,630 yamepatikana kwa njia ya michango mbalimbali. Hatua hii ilifanya shule za msingi kuwa na madawati 2,632,397 sawa na asilimia 77 ya mahitaji. Hivyo bado kuna upungufu wa madawati 792,949 sawa na asilimia 23. Shule za sekondari zimefikisha madawati 1,395,138 sawa na asilimia 93 ya mahitaji. Hivyo bado kuna upungufu wa madawati 112,785 sawa na asilimia saba. Ni dhahiri kuwa kazi iliyofanyika ni kubwa na ya kutia matumaini sana ambayo imewezesha Halmashauri 25 kukamilisha mahitaji ya madawati kutoka Mikoa 13 kwa madawati ya shule za msingi na Halmashauri 46 kutoka mikoa 19 kwa shule za sekondari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukae kidogo niweze kuongeza muda. Tafadhali naomba ukae kidogo!

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 28 (2) ninaongeza nusu saa ili tuweze kumalizia shughuli zilizobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa kazi iliyofanyika ni kubwa na ya kutia matumaini sana ambayo imewezesha halmashauri 25 mpaka sasa kukamilisha mahitaji ya madawati yote kutoka Mikoa 13 kwa madawati ya shule za msingi, na halmashauri 46 kutoka kwenye Mikoa 19 kwa shule za sekondari yameweza kukamilisha idadi ya mahitaji ya madawati yanayohitajika. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza sana wadau mbalimbali kwa jitihada zao za kuhakikisha kwamba agizo la Mheshimiwa Rais la kuhakikisha madawati ya kutosha yanapatikana shuleni linatekelezwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako hili Tukufu, napenda kuwapongeza sana wale wote waliochangia upatikanaji wa madawati ambao ni pamoja na Mheshimwa Rais mwenyewe na Baraza lake la Mawaziri, Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge wenyewe kwenye maeneo yenu, Makatibu Wakuu wa Wizara, Benki Kuu ya Tanzania na wafanyakazi wake wote wa Benki Kuu ya Tanzania ambao walikubali kutoa fedha zao kuchangia madawati, *CRDB Bank, NMB, TANAPA,* wafanyabiashara na wenye viwanda wakiongozwa na Dkt. Reginald Mengi, vikundi vya vijana, mafundi seremala, msanii Naseeb Abdul Juma maarufu kama *Diamond* na mafundi magari wa Gereji ya Tegeta. Niwapongeze pia Kamati ya Sherehe ya Harusi ya Ofisi ya TAMISEMI ambao wamejiwekea utaratibu wa kila harusi kutoa michango ya harusi kuweka kwenye madawati,

hongera sana, naomba wengine waige mfano huo. Kama kila harusi, zote hizi za kifahari tukichomoachomoa kununua madawati tunaweza tukafika mbali sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *Tanzania China Peoples Friendship Promotion Association* na wengine wengi ambao wamejitokeza kuchangia, tunatambua michango yao, huu ni mwamko mzuri wa kipekee ambao unaonesha kuwa jamii nzima imeweza kufanya vizuri, bila kusahau Taasisi ya *HMT (Hassan Maajar Trust)* ambayo ilijitoa kwa miaka mitatu mfululizo kuchangia madawati nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI inakamilisha taarifa kamili ya utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alilolitoa tarehe 15 Machi mwaka 2016 kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa kuhakikisha kwamba wanamaliza tatizo la madawati ifikapo leo Juni 30, 2016. Napenda taarifa hiyo ikamilike kabla ya tarehe 15 ili Serikali iweze kutoa kauli juu ya maeneo ambayo hayajakamilisha madawati. Wale ambao wanaendelea na jitihada hizi nitoe wito kwa wananchi, wadau, taasisi, wasamaria wema, mashirika mbalimbali ya kimataifa na kitaifa kwa ujumla kuendelea kuchangia kwa hiari madawati ili tatizo hili liishe kabisa na watoto wetu wapate kukaa. *(Makofi)*

Kuhusu mgao wa madawati ya Bunge kwa Waheshimiwa Wabunge, taratibu za mwisho zinakamilishwa ili mgao huo uweze kusambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwenye maeneo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu kuzungumzia suala la ugatuaji wa madaraka. Madhumuni ya kupeleka madaraka kwa wananchi ni kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi, pia unazipa mamlaka Serikali za Mitaa kuhusu kufanya maamuzi mbalimbali yahusuyo utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuwashirikisha katika kujiletea maendeleo na ustawi wao kwa ujumla wake. Hivyo, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatakiwa kutoa huduma za jamii kwa kuzingatia Ibara ya 143 na ya 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria za Serikali za Mitaa, Sura ya 287, na Sura ya 288, endapo mamlaka zitakwenda kinyume chake, Serikali Kuu inao wajibu wa kikatiba na kisheria kuingilia kati na kuchukua hatua stahiki dhidi ya mamlaka hizo. Nitoe wito kwa Wakuu wa Wilaya wote ambao wameteuliwa kutimiza wajibu katika maeneo yao kwa mujibu wa Katiba ili wananchi waweze kunufaika na rasilimali zinazoelekezwa katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa tija inapatikana katika madaraka ya kisiasa, majukumu, rasilimali fedha, rasilimali watu na muda, Serikali itaendelea kuelimisha wananchi juu ya Sera ya kupeleka madaraka kwa

wananchi *(D by D)* na kufanyia kazi sera na sheria zinazoendana na *D by D* ili kuzihuisha kulingana na mahitaji. Napenda kuziagiza Wizara husika za kisekta na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuweka mfumo wa utaratibu wa kuwa na vikao vya kazi za pamoja kufanya uchambuzi, tafsiri na tathmini ya utekelezaji wa majukumu kwa kuzingatia sera, sheria na hati idhini ya kila Wizara kwa lengo la kupata ufanisi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Serikali imeendelea kuimarisha mfumo wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, sambamba na kushughulikia changamoto mbalimbali zilizopo katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Ili kuhakikisha utoaji wa mikopo hii unafanywa kwa ufanisi mkubwa, Serikali itabadilisha utaratibu wa kupanga na kutoa mikopo ili kuwafikia wanafunzi wote wenye uhitaji zaidi wakiwemo yatima na wenye uwezo mdogo kiuchumi bila kujali aina ya programu wanazozisoma. Kupitia Bunge lako Tukufu napenda kuipongeza sana Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi kwa jitihada kubwa za kubaini ubadhirifu wa fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ulioweza kujitokeza. Serikali itaendelea kufanya uhakiki wa kina wa wanufaika wa mikopo na wote watakaobainika kujinufaisha binafsi watachukuliwa hatua kali zaidi za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu hivi sasa kuwahudumia walengwa unajengwa na fedha zinazotengwa kila mwaka katika mipango ya bajeti pamoja na marejesho ya mikopo iliyoiva kutoka kwa wanaonufaika. Serikali inaendelea kufanya maboresho ya mfumo wa kisheria ili kuimarisha urejeshwaji wa mikopo na lazima ikumbukwe kila mkopaji ni lazima arejeshe. Napenda kutumia nafasi hii kuwaagiza waajiri wote nchini kutekeleza wajibu wao wa kuingiza makato ya marejesho ya mikopo ya wanufaika kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa baada ya kuwasiliana na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi na udhibiti wa ubora wa elimu. Serikali inatambua kwamba elimu bora ni msingi wa ujenzi wa uchumi wa kisasa wa Taifa hili linalojitegemea. Ili kukidhi azma hii, Serikali imeweka kipaumbele katika kusimamia ubora wa elimu na kuhakikisha Kuwa Sera, Sheria, Kanuni, miongozo na viwango vya utoaji elimu nchini vinazingatiwa ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuimarisha kaguzi za mara kwa mara kwa kuimarisha Idara ya Ukaguzi iliyoko Wizara ya Elimu. Natoa wito pia kwa watendaji hususan Wakurugenzi wa Halmashauri na wadau wote wa elimu nchini kupokea maoni na ushauri unaotolewa na wadhibiti ubora wa elimu na kuyafanyia kazi kwa wakati. Serikali inaendelea na mkakati wa kuimarisha Idara hii ya Ukaguzi ili iweze kukagua na kudhibiti vizuri shule zote na kutoa ushauri ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi kifupi nchi yetu imepata mafanikio makubwa sana ya kuongezeka kwa fursa za upatikanaji wa elimu nchini kutokana na kuongezeka kwa shule za awali, shule za msingi, sekondari, vyuo vya ufundi pamoja na vyuo vikuu. Ili kuhakikisha kwamba ukuaji wa Sekta ya Elimu unaambatana na ubora stahiki wa kukidhi mahitaji ya sasa, Serikali itafanya mapitio na kuhuisha Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* na vyuo vikuu nchini kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa Udahili wa Pamoja *(Central Administration System)* pamoja na kuendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kuchukua hatua kali kwa taasisi zote za elimu zinazokiuka taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie hali ya usalama nchini. Kwa ujumla hali ya usalama wa raia na mali zao ni shwari, hata hivyo, katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Mei 2016, kumekuwepo na matukio ya mauaji ambayo yameleta hofu kubwa kwa wananchi. Matukio hayo yametokea katika Mikoa ya Tanga, Geita, Mwanza, Mara na Dar es Salaam. Moja ya matukio hayo ni tukio la tarehe 18, mwezi Mei, 2016 lililotokea Ibanda Relini, Mtaa wa Utemini, Wilaya ya Nyamagana, ambapo watu wapatao 15 wakiwa na mashoka, mapanga, visu na majambia walivamia Msikiti wa Masjid Rahman na kuwashambulia waumini waliokuwa wakiswali ndani ya msikiti huo. Wavamizi hao waliwaua kwa kuwakatakata mapanga watu watatu na kumjeruhi mwanafunzi mmoja wa Shule ya Msingi ya Kiislamu ya Jabaal.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio mengine ya mauaji makubwa ni yale yaliyotokea katika Mkoa wa Tanga mapema mwezi Aprili na mwishoni mwa mwezi Mei 2016. Katika tukio la kwanza, kundi la majambazi wakiwa na silaha mbalimbali zikiwemo za moto walivamia *Supermarket* ya *Central Bakery* iliyopo Mtaa wa Swahili Jijini Tanga na kupora fedha ambapo watu watano walipigwa risasi na kufariki dunia papo hapo na mmoja kujeruhiwa. Aidha, tukio la pili lilitokea tarehe 31 Mei usiku katika Kitongoji cha Kibatini, Kata ya Mzizima, Tarafa ya Chumbageni ambapo watu wasiofahamika wakiwa na visu na mapanga waliwavamia wakazi wa eneo hilo lenye idadi ya nyumba 30 na kuua watu wanane kisha kutokomea katika msitu uliopo karibu na Mapango ya Amboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama ikiwemo Jeshi la Polisi, imechukua hatua za haraka kwa kufanya operesheni maalum zilizowezesha kubainika na kukamatwa kwa baadhi ya watuhumiwa na wengine kuuawa baada ya mapambano na Polisi kwa risasi za moto. Aidha, baadhi ya silaha zilizokamatwa katika operesheni hizo na wote waliokamatwa wamefikishwa mbele ya vyombo vya sheria ili sheria ichukue mkondo wake. Nitumie fursa hii tena kuwapa pole viongozi na waumini wa Msikiti wa Masjid Rahman, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu waliouawa katika matukio yote ya mauaji kwa ujumla wao, Mungu alaze roho zao mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutumia vyombo vya usalama inaendelea na hatua za kuwatafuta wahusika wa matukio yote hayo waliokimbia ili wakipatikana wafikishwe kwenye vyombo vya dola kwa hatua zaidi za kisheria. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba matukio hayo ya kinyama kamwe hayatavumiliwa, ni mwanzoni mwa juma hili tu ambapo kwa ujasiri mkubwa Polisi wameweza kupambana na kiongozi wa wauaji wa raia kule Mwanza na Tanga na kufanikiwa kumuua. Serikali itawasaka wote waliohusika mpaka wapatikane ili sheria ichukue mkondo wake. Hata hivyo, ili kuwakamata wahusika, tunahitaji ushirikiano wa karibu kutoka kwa wananchi wenye mapenzi mema na nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba matukio ya mauaji ya raia wasio na hatia hayakubaliki kabisa katika Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Nitumie fursa hii kuwakumbusha wananchi na Watanzania wote kwamba jukumu la ulinzi na usalama wa nchi yetu ni la kila Mtanzania kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo basi, sote tunao wajibu wa kuzuia uvunjifu wa amani na uhalifu mahali tunapoishi au mahali tunapofanyia kazi. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, Wanasiasa wote na Viongozi wa madhehebu ya dini kutumia majukwaa ya siasa, mikutano ya dini na makongamano kusisitiza umoja wa kitaifa na hivyo kuungana na Serikali katika mapambano dhidi ya uhalifu unaoendelea kujijitokeza nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasihi pia wanahabari wote kutumia kalamu zao na vyombo vya habari nchini kote, kuandika habari zenye nia ya kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuendelea kuifanya nchi yetu idumu kama kisiwa cha amani badala ya habari zenye kuleta hofu na uchochezi miongoni mwa jamii. Imani yangu ni kwamba tukifanikiwa kuleta amani kwenye nchi yetu, maendeleo yetu yatakua kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha hoja yangu, napenda kusisitiza maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, tumepitisha bajeti ya Serikali ambayo inategemea sana ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa wafadhili kutoka nje. Tuongeze juhudi za kukusanya na za kupanua wigo wa kutoza kodi ili mapato yaongezeke na hivyo kukusanya kodi ya kutosha. Aidha, tushirikiane kwa dhati kubaini wakwepaji kodi na kuziba mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni, pamoja na juhudi za kukusanya kodi tujenge utamaduni wa kudai risiti kila tunaponunua bidhaa yoyote dukani. Natambua changamoto zilizopo kwa wafanyabiashara ndogondogo ikiwa ni pamoja na wanaofanya biashara sokoni na katika minada ya wazi,

tutaendelea kujenga uwezo wa watumishi wanaohusika na ukusanyaji wa mapato ili kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumedhamiria kujenga uchumi wa viwanda ili kuongeza mchango wa viwanda katika pato la Taifa na kuongeza ajira hususan kwa vijana na wanawake. Tuisaidie Serikali katika kubaini maeneo mazuri ya kuwekeza viwanda na kushiriki katika mnyororo wa uchumi kwa manufaa ya wananchi wote. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitenge maeneo maalum ya wafanyabiashara wadogo wakiwemo wamachinga na mama Lishe ili wafanye shughuli zao bila bughudha badala ya utaratibu wa sasa wa kuwaona kama wahalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, tunao Mradi mzuri sana wa mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam, ninawaomba wananchi na wakazi wote wa Dar es Salaam kutoa ushirikiano katika kutunza miundombinu ya mradi huo, na kushiriki katika kutunza mazingira. Aidha, kwa waendesha pikipiki, baiskeli, na waenda kwa miguu, wanaombwa kuwa waangalifu na kuacha kabisa tabia ya kupita kwenye barabara ya mabasi yaendayo haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, bado tunalo jukumu la kila mwananchi kushiriki katika masuala ya ulinzi na usalama wa nchi yetu. Tushirikiane kubaini matukio yoyote yanayoashiria uvunjifu wa amani na usalama wa raia wetu kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, na sita, kwa watumishi wa Umma, tuendelee kuhimiza umuhimu wa maadili katika sehemu zetu za kazi. Wote kwa pamoja tujenge utamaduni wa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu katika utumishi wa Umma na tujiepushe na vitendo vyovyote vya kukiuka taratibu za utumishi katika maeneo yetu ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijahitimisha, naomba uniruhusu nizungumzie matokeo ya uchunguzi wa maabara kuhusu ugonjwa usiojulikana hapa Mkoani Dodoma katika Wilaya za Chemba na Kondoa. Tarehe 19, mwezi Juni, mwaka huu, Serikali ilitoa taarifa kuhusu kuwepo kwa ugonjwa usiofahamika katika Wilaya za Chemba na Kondoa, Mkoani Dodoma ambapo jumla ya wagonjwa 21 na vifo 7 vilitokea. Hadi jana tarehe 29, mwezi huu, idadi ya wagonjwa ilikuwa imefikia 38 na vifo vimeongezeka mpaka 10. Aidha, jumla ya wagonjwa 35 wamepatiwa huduma za matibabu katika Hospitali za Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ugonjwa huu, Serikali imepeleka jopo la wataalam wa afya kwenye maeneo yaliyoathirika ili kutambua kiini chake. Aidha, sampuli mbalimbali zimekusanywa na kupelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, Maabara ya Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TDFA),* Maabara

ya Taifa ya Magonjwa ya Binadamu na Maabara ya Hospitali ya *KCMC*. Hadi sasa, ni sampuli ya aina moja tu ya nafaka (hususan mahindi) ambayo matokeo yake yameonesha kuwepo kwa uchafu wa sumukuvu *(aflatoxin)*. Uchunguzi wa sampuli za aina nyingine bado unaendelea na tunatarajia kuzipeleka pia nchini Marekani kwa uchunguzi zaidi. Tangu kujitokeza kwa ugonjwa huo hadi sasa, Serikali imechukua hatua nyingi tu ikiwemo na hizi zifuatazo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Moja, kukusanya sampuli, kama nilivyoeleza na kuziwasilisha kwa uchunguza kwenye maabara mbalimbali; Mbili, kutoa matiba kwa wananchi walioathirika na ugonjwa huo; Tatu, tumeendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya njia sahihi za uandaaji wa chakula utakaosaidia kupunguza kiasi cha *aflatoxin.* Njia hizo ni pamoja na kuchambua na kuondoa nafaka zilizoharibika yaani zilizooza, zilizovunjika, na zilizoharibika kama vile kwenye mchele, mahindi na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuwapa pole wote walioathirika na ugonjwa huu na tunawaombea waweze kupona haraka. Aidha, nawapa pole ndugu na jamaa wote waliopoteza ndugu zao, tunamuomba Mwenyezi Mungu alaze roho zao mahali pema peponi, lakini Serikali inaendelea kufanya jutihada za kuhakikisha kwamba ugonjwa huu unatokomezwa kabisa. Kwa namna hiyo, nawaagiza watendaji wanaohusika kuhakikisha kwamba matokeo ya sampuli zilizokusanywa yanapatikana mapema ili tuweze kukijua chanzo cha ugonjwa huo na tuweze kukidhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda niseme tu kwamba wakati tunahitimisha Mkutano huu leo, nitumie nafasi hii pia kumpa pole Mheshimiwa Spika na kumtakia apone haraka na arudi tuendelee kufanya kazi za kuwahudumia wananchi hapa kwetu. Mpaka jana, anaendelea vizuri, tumepata nafasi ya kuzungumza naye baada ya kuwa amefanyiwa tiba na kwa kweli tunaaza kupata faraja kuona kwamba hata sauti yake ni sauti ya mtu ambaye ana nguvu kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikushukuru wewe binafsi na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kusimamia vizuri na kwa weledi mkubwa vikao hivi vya Bunge, na hasa Mkutano huu ambao tunahitimisha leo. Niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu. Niwashukuru pia Watendaji wa Serikali kwa kusaidia Mawaziri, Manaibu Mawaziri katika kujibu hoja za Wabunge. Niwashukuru madereva wote ambao mmeshiriki kuwakimbizakimbiza Mawaziri, Wabunge na watendaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninamshukuru Katibu wa Bunge na timu yake kwa kutuwezesha kukamilisha mkutano huu bila vikwazo, natambua kazi kubwa inayofanywa na Watumishi wa Bunge kukimbia huku na huko kuwezesha mkutano huu kuendelea kufikia hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunahitimisha mkutano huu leo na kuelekea katika Majimbo yetu, nitumie muda huu kumwomba Mwenyezi Mungu awalinde wote, awaongoze katika safari zenu za kurejea nyumbani. Aidha, tunapokaribia kuumaliza mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani, napenda niwatakie Waislam wote na waumini wote kwa ujumla Idd - El - Fitr njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya mengi lakini yenye msingi, napenda kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi tarehe Sita Septemba, mwaka 2016, siku ya Jumanne, Saa Tatu asubuhi litakapokutana tena katika ukumbi huu hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono na Wabunge wote kasoro wachache tu, ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba hii na hoja ya kuahirisha Bunge. Waheshimiwa Wabunge kabla sijawahoji ninayo matangazo machache, kuna tangazo la wageni ambao waliingia baada ya wale tuliowatangaza asubuhi. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 133 wa Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao ni wanafunzi wa mwaka wa nne kutoka Chuo Cha Udaktari cha Hurbert Kairuki Dar es salaam wanaofanya mafunzo kwa vitendo yaani *interns* katika hospitali ya Mirembe Dodoma, Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Stanslaus S. Mabula ambao ni Viongozi wa shirikisho la Machinga Tanzania (SHIUMA) kutoka Makao Makuu yao Nyamagana Mkoa wa Mwanza na huyu ni Ndugu Matondo Masanja ambaye ni Mwenyekiti wa Shirika la Machinga Tanzania na Ndugu Denis Lekela ambaye ni Makamu Mwenyekiti na Ndugu Mwenge Fyeka ambaye ni Mjumbe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Wageni wanne wa Mheshimiwa Richard P. Mbogo ambao wameongozwa na Ndugu Lucy Mwamcheta ambaye ni Mke wake, karibu sana, ameambatana na watoto wake watatu ambao ni Ndugu Yasinta Richard, Alvin Richard na Jayden Richard karibuni, sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Hassan Elias Masala ambao ni familia yake wameongozwa na Mke wake ambaye ni Ndugu Paula Katenda ameambatana na watoto zake ambaye ni Lilian Hassan na Zawadi Hassan na Lulu Hassan pia wapo ndugu zake Mheshimiwa Hassan Elias Masala ambao ni Ndugu Mwasuma Shabani na Ndugu Alfred Mchinamnamba, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo na huyu ni Padri Innocent Sanga kutoka Kanisa la Katoliki Jimbo la Mbeya ambaye pia ameambatana na waumini wake wawili ambaye Ndugu January Kirumba na Ndugu Linus Sanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Profesa Mbarawa anawatangazia Wabunge wote ambao watasafiri na treni kesho kwamba watatakiwa kuwa kituo cha safari saa moja kamili asubuhi, muda wa treni kuondoka ni saa mbili kamili asubuhi, mnaombwa kufika katika kituo cha Dodoma *Railway station* ndiyo safari itakapoanzia. Nawasikia wengi kama wakishangaa nadhani wengine hawakujiandikisha majina, kwa hiyo kama hawakujiandikisha labda wamuone Profesa kama bado ana nafasi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club* anawatangazia kwamba viongozi mbalimbali wa mchezo wa mpira wa kikapu yaani *basketball* na mpira wa wavu yaani *volleyball* wameshapatikana. Na mpira wa kikapu Kapteni ni Mheshimiwa Ritta Kabati na Mwalimu ni Mheshimiwa Eng. Ramo Makani, na mpira wa wavu yaani *Volleyball* Kapteni ni Mheshimiwa Saumu Sakala, Mwalimu ni Ndugu Chacha Nyakega, kwa hiyo, hawa ndiyo viongozi wa hizi timu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia lipo tangazo lingine, leo Watumishi wawili wa Bunge ni siku yao ya kustaafu kazi na wapo humu ndani kwa hiyo tutawatambua rasmi mmojawapo ni Ndugu John Joel ambaye ni Naibu Katibu wa Bunge shughuli za Bunge. Ahsante sana ndugu John Joel kwa utumishi wako…*(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika, tunaomba aongezewe muda!

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Ndugu John Joel kwa Utumishi wako uliotukuka nadhani hayo makofi umeyaona Wabunge wanakushukuru sana kwa utumishi wako. Mtumishi Mwingine wa Bunge anayestaafu leo ni Ndugu Abdallah Suleiman ambaye ni Mhudumu wa Ukumbini, ahsante sana Ndugu Abdallah Suleiman nadhani umeyasikia hayo makofi tunakushukuru sana kwa utumishi wako wa muda mrefu na uliotukuka, Wabunge watakukumbuka sana ndiyo maana wanasikitika kwamba muda wako umekwisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshazileta salamu za Mheshimiwa Spika, na mimi nisingependa kuzirudia kwa sababu amezifikisha muafaka kabisa lakini niwasihi tu jambo moja kwamba anawashukuru sana kwa maombi yenu na anaomba mnapotawanyika leo muendelee kumuombea na huko mnakoenda anahitaji sala zenu ili aweze kurejea mapema kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyosema. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge ninayo taarifa ya Spika kabla ya kuwahoji, Waheshimiwa Wabunge mnamo tarehe 23 Aprili 2016, nililetewa ombi kutoka Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC)* kuhusu kuunda Kamati ndogo kwa mujibu wa Kanuni ya 117(18) kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa agizo la Kamati la *PAC* katika Bunge la 10 kwa Jeshi la Polisi lililotolewa tarehe 23 Oktoba, 2014 kuhusu utekelezaji wa mradi wa ki-*electronic* wa utambuzi wa alama za vidole yaani *automated finger print identification system*. Agizo hilo lilijengwa katika msingi wa hoja za ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Fungu 28 Jeshi la Polisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kilichohojiwa katika agizo hilo ni kutokamilika na kutokufanya kazi ipasavyo kwa mradi wa utambuzi wa alama za vidole ambao kwa kifupi unaitwa *AFPIS*.

Kazi hiyo ilitokana na mkataba uliokuwa umeingiwa kati ya Jeshi la Polisi ambaye alikuwa ni mnunuzi na Kampuni ya Lugumi *Enterprises Limited* ambaye alikuwa ni mzabuni. Baada ya majadiliano ya kina kuhusu hoja hiyo, Kamati ya *PAC* ilitoa agizo la utekelezaji kwa Afisa Masuuli wa Fungu namba 28 - Jeshi la Polisi. Agizo hilo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameendelea kufuatilia utekelezaji wake katika kaguzi za miaka iliyofuata. Agizo la Bunge lilimtaka Afisa Masuuli wa Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba mfumo wa *AFPIS* unafanya kazi katika kipindi cha miezi sita kwa kusema yafuatayo:-

Nanukuu; "Afisa Masuuli aliagizwa kuhakikisha kuwa mtambo wa *AFPIS (Automatic Finger Print Identification System)* unafanya kazi ndani ya miezi sita" Mwisho wa kunukuu. Katika kikao cha Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) cha tarehe 05 Aprili, 2016 kikao kilichojadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Fungu 28 - Jeshi la Polisi kwa mwaka wa fedha ulioisha 30 Juni, 2014 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, aliripoti tena utekelezaji wa agizo husika kwa Kamati. Katika maoni ya *CAG* ilielezwa kuwa mfumo wa *AFPIS* unafanya kazi katika vituo 14 tu kati ya vituo 108, kwa maana hii agizo la Kamati halikuwa limetekelezwa kikamilifu.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ilimtaka Afisa Masuuli wa Fungu Na. 28 ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuleta kwa Kamati taarifa ya utekelezaji wa mradi wa *AFPIS,* taarifa iliwasilishwa tarehe 18 Aprili, 2016 ambapo ilibaini kuwa vifaa vya mfumo wa *AFPIS* vimefungwa katika vituo 153 pamoja na Makao Makuu ya Polisi. Taarifa hiyo ilionyesha utofauti wa

takwimu ukilinganisha na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali, hivyo Kamati iliazimia kumuomba Mheshimiwa Spika, idhini ya kufanya uhakiki wa vifaa vya *AFPIS* kama vipo katika vituo vya Polisi vilivyotajwa na Afisa Masuuli. Vilevile, Kamati ilitaka kujiridhisha na sababu za kuchelewa kutekelezwa kwa mradi husika.

Waheshimiwa Wabunge, Spika alielekeza kuundwa kwa Kamati ndogo kwa mujibu wa Kanuni ya 117(18) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili iweze kufanya uhakiki kwa mujibu wa hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hivyo kamati ndogo ilipewa hadidu ya rejea moja kama ifuatavyo: "Kamati ifanye uhakiki iwapo vifaa vilinunuliwa na kufungwa" Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ndogo imekamilisha kazi yake ya uhakiki na imewasilisha taarifa yake kwenye Kamati ya *PAC*, aidha Kamati ya *PAC* imeipitia taarifa hiyo na kukamilisha majukumu yake na kuikabidhi kwa Spika kama inavyotakiwa na Kanuni. Baada ya kuipokea taarifa husika na kuangalia maudhui yake na kwa mujibu wa matokeo ya uhakiki uliofanywa na Kamati ndogo na baada ya kamati ya *PAC* kuridhia matokeo ya uhakiki huo na kuthibitisha kwamba vifaa vipo ukiacha kasoro zilizojitokeza na kwa kuzingatia kuwa jambo hili siyo jipya lililotokana na hoja ya ukaguzi wa miaka ya nyuma, kilichokuwa kimebaki ni vifaa hivyo kufanya kazi iliyokusudiwa ambayo ndiyo msingi wa hoja ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(17) kwa ajili ya kumbukumbu nitawasomea. Spika ataweka utaratibu wa kujadili taarifa za Kamati na endapo Kamati yoyote katika kutekeleza majukumu yake itaona kuwa kuna mambo ya utekelezaji ambayo yanahitaji kurekebishwa inaweza kutoa taarifa maalum ya ushauri kwa Waziri mwenye dhamana juu ya mambo hayo ili Waziri aweze kuchukua hatua zinazostahili.

Kwa mujibu wa Kanuni hiyo ambayo nimekwisha kuisoma, nimekabidhi matokeo ya uhakiki yaani maoni, ushauri, mapendekezo ya namna ya kutatua changamoto zilizoainishwa na taarifa ya Kamati ya *PAC*. Aidha pamoja na maagizo hayo yaliyokabidhiwa Serikalini ninaagiza sasa kwamba Serikali ihakikishe mfumo huu unafanya kazi ndani ya miezi 3 kuanzia leo, ili kuboresha uwezo wa Jeshi la Polisi kuwa na utambuzi wa haraka wa wahusika wa matukio ya kihalifu katika vituo vyote nchini.

Pili, masuala yote yaliyobainika kuwa na dosari za kiutendaji yapatiwe ufumbuzi haraka. Aidha, nimeelekeza Kamati ya *PAC* ihakiki maelekezo niliyoyatoa na baada ya uhakiki huo Kamati itoe taarifa Bungeni wakati ikiwasilisha taarifa yake ya mwaka. Nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya *PAC* ninatarajia kuwa suala hili sasa litafikia mwisho na Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa Hesabu za Serikali atafunga hoja yake baada ya kujiridhisha na utekelezaji wa maagizo niliyoyatoa. Hiyo ndiyo taarifa ya Spika kuhusu jambo hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri ya kuahirisha Bunge mpaka tarehe Sita Septemba, 2016.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hapa Wimbo wa Taifa uliimbwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba tukae, sasa natangaza kwamba Bunge limeahirishwa mpaka tarehe aliyoitaja Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambayo ni tarehe 6 Septemba, 2016, saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.37 Mchana Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne,*
*Tarehe 6 Septemba, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*